

SWALA LA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI:  
WAANDISHI WA KIKE KATIKA NJIA-PANDA.

KATW'IWA MULE

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya  
mahitaji ya shahada ya 'Master of Arts' katika  
Chuo Kikuu cha Kenyatta.

1991.


Mule, Katwina  
*Swala la mwanamke  
katika tamthilia ya*




91/197922


UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa  
kwa mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu kingine.

  
\_\_\_\_\_  
KATWINIWA MULE  
(MTAHINIWA).

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu  
kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu.

-   
1. PROF. CHACHA NYAIGOTTI-CHACHA  
EGERTON UNIVERSITY, NJORO.

-   
2. BI. CATHERINE MWIHAKI NDUNGO.  
KENYATTA UNIVERSITY, NAIROBI.

(i)

YALIYOMO

UKURASA

Yaliyomo .....	(i)
Kutabaruku .....	(iv)
Shukurani .....	(v)
Muhtasari .....	(vi)

1:0 SURA YA KWANZA- Utangulizi wa somo la Utafiti

1:1 Utangulizi .....	1
1:2 <i>Suala</i> Somo la Utafiti .....	4
1:3 Madhumuni ya Utafiti .....	5
1:4 Upeo wa Utafiti .....	7
1:5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili .....	9
1:6 Sababu za kulichagua somo hili .....	15
1:7 Msingi wa Nadharia .....	16
1:8 Njia za Utafiti .....	20

2:0 SURA YA PILI- Mwachofi na Ryanga

2:1 Utangulizi .....	22
2:1:1 A.K. Mwachofi: <u>Mama Ee</u> ; Hadithi Kwa Ufupi .....	22
2:1:2 Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	28
2:1:3 Mtazamo wa Mwandishi .....	39
2:2 S.A. Ryanga: <u>Zinduko</u> .....	48
2:2:1 Hadithi kwa ufupi .....	48
2:2:2 Taswira ya Mwanamke .....	50
2:2:3 Mtazamo wa Mwandishi .....	54
2:3 Kimalizio .....	58

3:0	<u>SURA YA TATU</u> - Waandishi wawili wa kike wa Tanzania Chogo na Muhando wa Awali	
3:1	Utangulizi .....	61
3:2	Waandishi .....	61
3:3	Mazingira ya Waandishi .....	64
3:4	Angelina Chogo: <u>Kortini Mtu Huyu</u> .....	65
3:4:1	Hadithi kwa ufupi .....	65
3:4:2	Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	67
3:4:3	Mtazamo wa Mwandishi .....	74
3:5	Penina Muhando: <u>Hatia</u> .....	83
3:5:1	Hadithi kwa Ufupi .....	83
3:5:2	Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	84
3:5:3	Mtazamo wa Mwandishi .....	91
3:6	Penina Muhando: <u>Pambo</u> .....	97
3:6:1	Hadithi kwa Ufupi .....	97
3:6:2	Maudhui kwa Ufupi .....	98
3:6:3	Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	100
3:6:4	Mtazamo wa Mwandishi .....	103
3:6:5	Kimalizio .....	110
4:0	<u>SURA YA NNE</u> - Penina Muhando 1982-1984	
4:1	Utangulizi .....	112
4:2	Penina Muhando: <u>Nguzo Mama</u> .....	113
4:2:1	Hadithi kwa Ufupi .....	113
4:2:2	Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	116
4:2:3	Mtazamo wa Mwandishi .....	122
4:3	Penina Muhando: <u>Lina Ubani</u> .....	126
4:3:1	Hadithi kwa Ufupi .....	126

4:3:2	Kusawiriwa kwa Mwanamke .....	128
4:3:3	Mtazamo wa Mwandishi .....	133
4:4	Kimalizio .....	139
5:0	<u>SURA YA TANO</u> -Hitimisho	
5:1	Utangulizi wa Hitimisho .....	142
5:2	Kazi kwa Jumla .....	150
5:3	Matatizo na Mafanikio .....	152
5:4	Mapendekezo ..... <i>Recommendations</i>	153
MAREJELEO	.....	154

KUTABARUKU

Kwa wazazi wangu

David Mule na Esther Kalondu  
walionilea nikawa nilivyo sasa

Kwa dadangu

Agnes Munyiva,  
aliyenisaidia kwa hali na mali

Kwa mke wangu mpendwa

Lucy  
aliyenitia moyo, ari na ilhamu  
ya kuikamilisha kazi hii

Kwa watoto wangu wapendwa

Mueni na Mule  
ambao kila nikiondoka  
waliniaga kwa vilio.

SHUKRANI

Kazi kama hii haikamiliki bila usaidizi na ushirika wa watu wengine. Ninawashukuru wale wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine kuikamilisha kazi hii. Ni vigumu kuwataja wote kwa majina. Hata hivyo, shukrani zangu zimwe-ndee Profesa Chacha Nyaigotti - Chacha ambaye mbali na kuwa mlezi wangu kimasomo ameisimamia kazi hii. Bila ushauri na mwongozo wake labda ningeyumba au kuzama njiani.

Kwa Bi. Catherine Mwihaki Ndungo pia ni shukrani nyingi sana kwa kuisimamia kazi hii. Ushauri na mwongozo wake ulinifaa sana.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu mabwana Gwachi, J.M.O., Furaha J.H., Maitaria J.N., Chacha D.M. na Bi. Momanyi, C. kwa kunitia moyo nilipokuwa ninaifanya kazi hii.

Nakishukuru Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuyagharamia masomo yangu.

Siwezi kumsahau Profesa Euphrase Kezilahabi wa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye alinitumia nakala ya tamthilia ya Muhando ya Heshima Yangu kwa gharama yake.

Usaidizi kama huu pia niliupata kutoka kwa Dkt. Ciarunji Chesaina na Bw. Gachanja wa Kiai, wote wa Idara ya Literature, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Shukrani zangu kwao hazisemeki, na zaidi kwa msaada wa kimawazo walionipa tangu mwanzo wa kazi hii. Kwa R.M. Wafula, pia ni shukrani kubwa.

MUHTASARI

Tasnifu hii ni uhakiki wa swala la mwanamke kama linavyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa kike. Tunachunguza taswira zinazojitokeza katika kila mojawapo ya kazi tulizozishughulikia. Kutokana na taswira hizi, tunauchambua msimamo wa mwandishi kuhusu swala la ukombozi wa wanawake. Uchunguzi huu umeibuka kutokana na imani kwamba wanawake ni kundi linalodhulumiwa katika jamii ya sasa kwa msingi ya uana wao. Tunaamini kwamba lazima swala la ukombozi wao lianze nao. Uchunguzi wetu basi unajaribu kuchunguza iwapo waandishi hawa ni watetezi halisi wa maslahi ya wanawake.

Sura ya kwanza ni utangulizi. Hapa, tunazingatia somo la utafiti, madhumuni yake na upeo wa utafiti huu. Pia tumezungumzia kwa ufupi yale yaliyoandikwa kuhusu mada hii na kuelezea kwa muhtasari nadharia tunayoitumia kuzitathmini kazi tulizozichagua. Hatimaye tunatoa sababu zilizotufanya kulichagua somo hili na kuonyesha njia tulizotumia kuufanya utafiti huu.

Sura ya pili inawachambua waandishi wawili wa kipekee wa Kenya. Hawa ni Sheila Ali Ryanga na Ari Katini Mwachofi. Tumeonyesha kuwa waandishi hawa wanatofautiana kimaudhui, uendelezaji wa wahusika na kimtazamo. Hata hivyo, kwa njia moja au nyingine, wanaonekana kutokuwa na msimamo thabiti kuhusu swala la mwanamke.

Sura ya tatu inazichunguza tamthilia mbili za Penina MUhando alizozindika kati ya 1972 na 1974 na tamthilia moja ya Angelina Chogo aliyozindika 1976. Hawa ni waandishi wa Tanzania. Tumeonyesha athari za siasa ya ujamaa kwa uchotaji na uendelezaji wa maudhui, wahusika na masuluhisho wanayoyapendekeza kwa matatizo yanayoikumba jamii yao; swala la mwanamke likiwemo.

Sura ya nne ni Uchambuzi wa tamthilia mbili za Penina Muhando alizozindika katika miaka ya themanini. Tumeonyesha jinsi mwandishi huyu anavyobadilika na kupevuka kimtazamo katika kazi hizi zikilinganishwa na zile nyingine za mwanzo.

Sura ya tano ndiyo hitimisho ya kazi hii. Hapa, tunatoa muhtasari wa kazi yetu kwa jumla na kujadili kwa ufupi mambo muhimu yanayojitokeza katika kazi hizi. Pia tumetoa mapendekezo yetu kuhusu utafiti zaidi ambao ungefanywa kuwahusu waandishi hawa.

1:0

SURA YA KWANZA

1:1 UTANGULIZI

Katika utafiti huu, tumelihakiki swala la mwanamke katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake tukitumia mtazamo wa ujamaa (wa) kike. Ujamaa (wa) kike katika muktadha huu unamaanisha 'socialist feminism'. Kunao waandishi wachache sana wa kike katika Bara la Afrika hasa ikilinganishwa na wanaume. Hali hii ni mbaya zaidi tunapo-waangalia wale waandikao katika lugha ya Kiswahili. Hapa Kenya, wale tuwajuao kufikia sasa ni Sheila Ali Ryanga (1986) ambaye ameandika Zinduko na Ari Katini Mwachofi (1987) ambaye ameandika Mama Ee. Nchini Tanzania, Mwandishi aliyeandika kwa wingi sana ni Penina Muhando ambaye kufikia sasa ameandika tamthilia tisa tuzijuazo; mbili kati ya hizi akiwa ameshirikiana na wengine. M.L.B. Matteru (1984) naye ameandika Ayubu akishirikiana na Paukwa Theatre group na Harakati za Ukombozi (1981) akishirikiana na Muhando na Amandina Lihamba. Angelina Chogo (1976) ameandika Kortini Mtu Huyu. Kuna uwezekano kuwa kuna waandishi wengine wa kike wa Tanzania ambao hatuwajui. Jambo la muhimu zaidi kuzingatia ni kwamba waandishi hawa ni wachache sana.

Wahakiki kama vile Brown (1981), Taiwo (1984), Davies na Graves (1986), Chesaina (1987) na Kieti (1991) wamejaribu kutoa sababu ambazo zimewafanya wanawake wengi kutojiingiza katika ulimwengu wa uandishi wa kisanaa licha ya ukweli kwamba kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kuwa katika jamii kongwe za

kiafrika, walishiriki kikamilifu katika uzalishaji wa fasihi simulizi. Kwa maoni ya Davies (1986:1), hii ni ithibati kuwa ubunifu wa kisanaa (artistic creativity) sio milki ya wanaume pekee.

Wahakiki hawa wanaonelea kuwa upungufu wa waandishi wa kike unatokana na athari za kikoloni. Katika enzi za ukoloni Barani Afrika, wanaume walipendelewa katika utoaji wa nafasi za elimu ya kikoloni na ijapokuwa katika nchi nyingi huru za kiafrika hali hii imebadilika, wanawake bado hawapati nafasi sawa na wanaume kutokana na sababu za kiuchumi na masalia ya tamaduni kongwe ambazo humweka mwanaume mbele katika karibu kila nyanja ya maisha. Brown (1981:4) anatueleza:

Idadi ya wanawake wanaoandika katika Afrika imekuwa ndogo tangu zamani hasa ikilinganishwa na ya wanaume...hadi miaka ya hivi karibuni, wanawake hawakuwa wanapata nafasi sawa za elimu na wanaume, kwa hivyo wachache sana walijua kusoma na kuandika, sembuse elimu ya chuo kikuu, ambayo imekuwa jambo la kimsingi katika uandishi wa fasihi ya Kiafrika katika lugha za Ulaya.

Sababu nyingine ni ugawaji wa kazi na majukumu ya kijamii baina ya wanaume na wanawake. Kulingana na Davies (1986:2), ugawaji huu wa majukumu uliendeleza dhana kuwa elimu ya kimagharibi ilikuwa kikwazo kwa majukumu ya wanawake kama wazazi na mabibi na kwa jumla kuwafanya wasifikie upeo wa maisha yao kwa vigezo vya jamii zao.

Hali hii ya 'ukame' wa kimaandishi imekuwa na athari mbili; kwanza, kumekosekana kile ambacho tunaweza kukiita 'sauti ya kike' (the feminine voice) katika uwanja huu wa

tamthilia. Akizungumza juu ya riwaya ya kiafrika, Palmer (1983:38) anasema:

Riwaya ya Kiafrika, imekuwa, hadi miaka ya hivi karibuni ikisifika kwa kukosekana kwa kile ambacho kinaweza kuitwa mtazamo wa kike.

( The African novel has until recently been remarkable for the absence of what might be called the feminine point of view).

Kutokana na uhaba wa waandishi wa kike, maswala ya kike, kama yanayowakilishwa katika fasihi ya Kiafrika kwa jumla yameachiwa waandishi wa kiume. Kutokana na hali hii, wahakiki waliojishughulisha na uchambuzi wa taswira ya mwanamke katika fasihi wametoa hoja kuwa taswira zinazojitokeza katika maandishi ya kiume ni zile zilizoundwa na kuendelezwa na jamii watokamo waandishi hao (tazama Ndungo 1985, Chesaina 1987, Matteru 1987 na Lugano 1989). Hata hivyo, kulingana na Chesaina, wapo waandishi wachache wa kiume ambao wametambua kuwa mwanamke ana nafasi duni katika jamii kongwe na jamii ya sasa na ijapokuwa wamejitahidi kumkomboa mwanamke kutokana na hali hii, wameshindwa kwa kiasi fulani kulielewa swala hili ipasavyo. Kwa jumla, taswira zinazopatikana mara nyingi ni zile za mwanamke kama mzazi, chombo cha kumfurahisha mwanaume, mtumwa, mali ya mwanaume na mlaumiwa kwa maovu yote ya kijamii. Falsafa kuu imekuwa kwamba mwanamke mzuri ni yule anayekubali kukaa jikoni akimtumikia mumewe kwa uaminifu na utiifu. Waandishi wengi wa kiume wamejaribu kuonyesha jinsi mwanamke alivyoridhika na nafasi hii. Katika baadhi ya maandishi haya ya kiume, uhuru wa mwanamke unaonekana kuwa kinaya, lau sivyo ndoa inaonekana kuwa suluhisho la matatizo ya wanawake.

Pili, uhakiki wa maandishi ya wanawake haujashughulikiwa sana (Brown 1981:3). Ni wahakiki wachache ambao wamejitokeza kulihakiki swala la mwanamke kama linavyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Tasnifu hii basi imejishughulisha na baadhi ya maandishi haya ya kitamthilia ambayo yameandikwa baina ya 1972 na 1987; takribani miaka ishirini na tano baada ya uhuru.

## 1:2 SOMO LA UTAFITI

Utafiti wetu umejishughulisha na swala la mwanamke katika baadhi ya tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake.. Tumezichambua taswira za mwanamke ambazo zimejitokeza katika kila mojawapo ya tamthilia tulizozichagua. Ili kufikia lengo hili, tumewahakiki baadhi ya wahusika kama wahusika binafsi. Hapa, tumewatazama baadhi ya wahusika wa kike na wa kiume katika tamthilia tulizozichambua. Kwa upande mwingine, tumewatazama wahusika hawa katika hali halisi ambamo wamesawiriwa. Wahusika hawa tumewachukulia kuwa wawakilishi wa fikra, maoni na mitazamo ya maandishi tuliojishughulisha nao kuhusu swala la mwanamke. Hili tumefanya kwa kubaini kuwa fikra za mwandishi kuhusu jamii kwa jumla hujazwa katika wahusika. Kulingana na Eagleton (1986:104), mwanatamthilia wa kike, kama mwanatamthilia mwingine ye yote yule, hasimami jukwaani na kutoa maoni yake bali kupitia kwa wahusika anaowaumba huwasiliana na hadhira yake.

Uandishi wote wa kifasihi una kipengee cha uana. Neno 'uana' katika muktadha huu linamaanisha 'gender'. Wahakiki wengi waliojishughulisha na swala la kusawiriwa kwa mwanamke

katika fasihi wametoa hoja kuwa taswira mbaya na za kupotosha tunazozipata katika fasihi zinatokana na hali kwamba waandishi wengi ni wa kiume ambao kwa kiasi kikubwa huwakilisha itikadi za jamii zilizowakuza kuhusu wanawake. Tumelihakiki swala la mwanamke katika tamthilia zilizoandikwa na wanawake kwa lengo la kubainisha jinsi wanavyowasawiri wahusika wao. Lengo kuu limekuwa ni kutalii iwapo wanawasawiri tofauti na waandishi wa kiume.

Katika tasnifu hii, tumeonyesha kuwa ijapokuwa waandishi tuliwashughulikia ni wanawake wanaoandika kwa mtazamo wa kike kuhusu swala la mwanamke, hawana mitazamo inayolingana juu ya swala hili mbali na ukweli kwamba wote hawaonekani kuwa na uamuzi kamili kuhusu mwelekeo ambao ukombozi wa mwanamke unapaswa kuchukua; yaani wako katika njia panda.

Kwa sababu utafiti wetu umejihusisha na swala la mwanamke katika kazi za fasihi zilizoandikwa na wanawake, tumewahakiki wahusika wa kike kwa mtazamo wa kifasihi na kuonyesha jinsi walivyosawiriwa huku tukitoa maoni yetu kuhusu jukumu na nafasi waliyopewa na waandishi hawa kama kielelezo cha mitazamo ya waandishi wenyewe kuhusu swala hili.

### 1:3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika tasnifu hii, kuna mambo kadha wa kadha ambayo tumbainisha. Kwanza, tumezichambua taswira za mwanamke zinazojitokeza katika kila kazi tuliyoishughulikia. Kupitia kwa taswira hizi, tumehakiki mitazamo na misimamo ya waandishi tuliowachagua kuhusu swala la mwanamke na ukombozi wake kama

lilivyowakilishwa katika tamthilia hizo. Ili kutimiza lengo hili, tumechukulia mwandishi wa kike, mwenyewe kama mwanamke, kuwa mwakilishi wa maswala ya kike mbali na maswala mengineyo. Tumezingatia jinsi wanavyoyashughulikia maswala haya. Wao kama wanawake hawana budi kuwakilisha matatizo ya wadhulumiwa wenzao. Chambilecho Monteith (1986:1).

Mwandishi ambaye pia ni mdhulumiwa hana budi kufichua matatizo ambayo yanatokana na hisia za kutotendewa haki...

(Tafsiri hii na nyinginezo katika kazi hii ni zetu).

Ikiwa mwandishi ataupuuza wajibu huu, basi atakuwa amelisaliti kundi au tabaka lake.

Katika kufikia lengo letu hili, tumeongozwa na imani kuwa lazima swala la ukombozi wa mwanamke lianze na mwanamke mwenyewe. Reed (1970:8) ameendeleza hoja kama hii anaposema kuwa wakandamizwaji wote, wakiwemo wanawake, wamelazimika kuandika na kuziandika upya historia zao na kusahihisha picha za kupotosha ambazo zimekuwa zikiendelezwa kuwahusu. Mathalani, katika tasnifu hii, tumeona baadhi ya waandishi hawa hawazisahihishi taswira hizi za kupotosha.

Pili, tumetathmini iwapo waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wa kike ni watetezi halisi wa maslahi ya kike au bado wako katika hali ya kuyumbayumba. Utafiti wetu umehakiki kwa jumla jamii zilizowakuza waandishi wa kike kama zilivyowakilishwa katika kazi hizi, hatua ambazo waandishi wanaonelea zinapasa kuchukuliwa ili kumwoposha mwanamke na janga anamojikuta kwa kuwa ni mwanamke na falsafa zao kuhusu wanawake

kwa jumla. Lengo hili tumelitimiza kwa kuhakiki jinsi wanavyo-  
wasawiri wahusika wao hasa katika harakati zao za kukabiliana  
na matatizo yanayowakumba.

Utafiti wetu umejijhusisha na waandishi ambao mazingira  
yao yanatofautiana. Kwa hivyo, madhumuni mengine yamekuwa ni  
kulinganisha namitazamo ya waandishi hawa na kutathamini ni  
kwa kiwango gani waandishi hawa wameathiriwa na mazingira yao.  
Waandishi hawa wote wameandika baada ya nchi zao kujirejeshea  
uhuru wao. Hata hivyo, Kenya imechukua mkondo wa kiuchumi wa  
kibepari ilhali Tanzania, kupitia Azimio la Arusha imechukua  
mkondo wa kijamaa katika harakati za ujenzi wa taifa.?

Dhima ya fasihi nzuri katika jamii ni kuangazia au  
kuashiria ujenzi wa jamii mpya ambapo amali za kibinadamu  
zinaheshimiwa na pia kuashiria muundo mpya wa jamii ambao  
utaleta afueni kwa wanaodhulumiwa. Madhumuni mengine basi  
yamekuwa ni kuonyesha vile ambavyo waandishi hawa wanayaona  
mabadiliko ya kijamii na nafasi ya mwanamke katika jamii hiyo  
mpya. Jambo hili limeweza kubainika kupitia kwa wahusika;  
katika muktadha huu wahusika wa kike katika maingiliano yao  
na wahusika wa kiume.

#### 1:4 UPEO WA UTAFITI

Tumezichambua tamthilia zifuatazo katika tasnifu hii:

Kenya:

Ari Katini Mwachofi (1987) Mama Ee (Nairobi, Heinemann).

Sheila Ali Ryanga (1986) Zinduko (Nairobi, Oxford  
University Press).

Tanzania:

Penina Muhando (1972) Hatia (Nairobi, East African Publishing House).

(1975) Pambo (Nairobi, East African Publishing House).

(1982) (Nguzo Mama (Dar es Salaam Dar es Salaam University Press).

(1984) Lina Ubani (Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press).

Angelina Chogo (1976) Kortini Mtu Huyu, (Nairobi, Foundation Books).

Penina Muhando ameandika tamthilia nyinginezo

zifuatazo:

Tambueni Haki Zetu (Dar es Salaam, Tanzania Publishing House 1974).

Heshima Yangu (Nairobi East African Publishing House 1974).

Talaka Si Mke Wangu (Nairobi, East African Publishing House 1974).

*Mwaka??* Harakati za Ukombozi (Muhando, Lihamba na Balisidya, Dar es Salaam, Tanzania Publishing House).

Hatukujishughulisha na kazi hizi kwa sababu zile tulizozichagua zinawakilisha kikamilifu mtazamo wa mwandishi huyu kuhusu swala la mwanamke.

Waandishi hawa tumewachagua kwa sababu wote ni waandishi wa kike ambao wamewapa nafasi muhimu wahusika wa kike katika

kazi tulizozichagua. Kazi hizi tunaonelea zitatosheliza mahitaji yetu. Pia, tunaonelea kuwa kazi tulizozichagua zinaendeleza maoni yetu kuwa Waandishi wa kike wa tamthilia ya Kiswahili wako katika njia panda kuhusu swala la mwanamke; yaani wanaonyesha kutokuwa na uamuzi na msimamo thabiti kuhusu swala hili.

1:5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kuna wahakiki wachache ambao wamejishughulisha na swala la mwanamke katika tamthilia za kike na pia katika maandishi ya kike kwa jumla. Miongoni mwa kazi zilizoandikwa kuhusu swala la mwanamke katika tamthilia ni ile ya Chesaina (1987). Chesaina amehakiki jukumu na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiafrika. Katika kazi yake, ameshughulikia tamthilia zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. Hakujobainisha na maandishi wa kike wala wa kiume bali amewachukua baadhi ya maandishi wa pande zote mbili na kuwalinganisha huku akitoa hoja kwamba maandishi wa kike na wa kiume wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika jinsi wanavyo-wasawiri wahusika wa kike. Hoja yake kuu ni kwamba wanaume wanapoandika juu ya maswala ya kike wanakumbana na vikwazo kadhaa na hawawezi kuipenya nafsi ya mwanamke. Ijapokuwa baadhi yao wameonyesha kuyajali maslahi ya mwanamke, wanashilia kuonyesha jinsi ambavyo wanawake hawawezi kujikomboa kutokana na hali hii. Miongoni mwa kazi tulizozichambua, Chesaina amechambua kwa ufupi usawiri wa wahusika wa kike katika Hatia (1972) na Nguzo Mama (1982). Hata hivyo, kutokana na wingi wa kazi alizozishughulikia, Chesaina hakuzichambua kazi

hizi kwa undani sana. Utafiti wetu umezichambua kwa undani zaidi baadhi ya kazi hizi mbali na nyinginezo kuhu tukimlinganisha Muhando na baadhi ya waandishi wengine wa kike. Aidha, Chesaina hakumshughulikia mwandishi ye yote wa kike wa Kenya aandikaye kwa lugha ya Kiswahili. Kama tulivyotaja awali, huku Kenya kuna waandishi wawili ambao hawana budi kushughulikiwa. Hili ni pengo ambalo utafiti wetu umejaribu kuliziba. Juu ya hayo, Chesaina ameipinga nadharia ya 'Feminism' kama nadharia ya uhakiki huku akidai kuwa nadharia hii si ya Kiafrika na haina umuhimu wowote katika mazingira ya Kiafrika. Maoni yetu ni tofauti na ya Chesaina. Nadharia tuliyoitumia ni ya ujamaa wa kike ambayo tunaiona kuwa nadharia ya kipekee inayolishughulikia swala la mwanamke kwa marefu na mapana yake. Hata hivyo, utafiti wake umetufaa sana katika kuendeleza hoja zetu.

Naye Lugano (1989) amehakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya nne za Euphrase Kezilahabi. Katika utafiti wake, Lugano anatoa hoja kuwa Kezilahabi, mbali na kuwa mwitifaki wa nadharia ya utamaushi, ni mwandishi wa kiume ambaye anakatisha tamaa kuhusu ukombozi wa mwanamke. Kwa maoni ya Lugano, Kezilahabi anaendeleza falsafa za jamii yake kongwe kuhusu wanawake; falsafa ambayo inamchukulia mwanamke kuwa kiumbe duni aliye chini ya utawala wa mwanaume. Kwa hivyo, anakatisha tamaa kuhusu ukombozi wa Wanawake kama afanyavyo kwa wanyonge wale wengine katika jamii anayoizungumzia. Katika utafiti wa Lugano, hoja kwamba mwanaume anakumbana na vikwazo ambavyo hawezi kuvimudu kama mwandishi inajitokeza. Utafiti wetu umejifunga kuwatazama waandishi wa kike. Vikwazo

vinavyodaiwa kuwalemaza waandishi wa kiume haviko kwa wanawake. Kwa hivyo, tumezichambua taswira za wanawake wanazozieleza katika kazi zao.

Kazi nyingine imefanywa Ndungo (1985). Utafiti wake unahusu jinsi ambavyo taswira ya mwanamke imebadilika katika vipindi na mazingira mbalimbali ya kihistoria. Ndungo ameichambua taswira ya mwanamke katika Utendi wa Mwanakupona (1860) kama kiwakilishi cha taswira ya mwanamke 'wakati wa Umwinyi na katika mazingira ya Kiislamu'; Kaburi Bila Msalaba (1969) kuwakilisha taswira ya mwanamke katika kipindi cha ukoloni; mathalani kipindi cha vita ya ukombozi ya MauMau na jinsi mwanamke alivyoathiriwa na vita hiyo na Utengano (1980) kuwakilisha taswira ya mwanamke baada ya uhuru. Utafiti wa Ndungo umejifunika kuonyesha jinsi ambavyo taswira ya mwanamke imebadilika kuambatanana na vipindi mbalimbali vya kihistoria. Amewachambua waandishi wawili wa kiume na mmoja wa kike. Kazi alizozichambua si za kitamthilia. Juu ya hayo, kauli aitoayo ni kuwa ukombozi wa tabaka la chini utategemea kuangushwa kwa mfumo wa kibepari na kuanzishwa kwa ujamaa. Tunatofautiana na Ndungo kimtazamo. Kwa maoni yetu, kuangushwa kwa mfumo wa kibepari na kuanzishwa kwa ujamaa hakumaanishi kuwa mwanamke atakuwa amekombolewa kama mwanamke. Ukombozi wa wanyonge wote kwa jumla haumaanishi kuwa uhusiano baina ya wanaume na wanawake utakuwa wa usawa; yaani wanawake watakuwa wameacha kudhulumiwa kwa misingi ya uana wao. Nadharia wanayoitumia Ndungo na Lugano imejishughulisha sana na mfumo wa uzalishaji mali. Kulingana na nadharia hii, ukombozi wa wanawake utaletwa na ukombozi wa wanawake kiuchumi. Nadharia hii hupuuza mifumo na itikadi nyinginezo zipatikanazo

katika jamii na ambazo zinaendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke.

Mbughuni (1982) ameandika makala kuhusu taswira ya mwanamke katika maandishi ya kiriyaya ya Tanzania. Katika makala yake, Mbughuni anatoa hoja kuwa taswira inayoendelezwa kuhusu mwanamke katika riwaya ya Kitanzania ina uwili.

Taswira ya mwanamke inayopatikana sana ni ile ya Hawaa; ambapo mwanamke husawiriwa kama mlaghai na mhalifu katika jamii.

'Hawaa' wa Bibilia hutumiwa katika uhakiki kumaanisha mwanamke ambaye anawakilisha uovu wote katika jamii; mchoyo, mlaghai, mvuruga amani, shetani na kadhalika. Taswira nyingine inayojitokeza kulingana na Mbughuni ni ile yakumweka mwanamke jikoni huku akiwa ametawaliwa na mwanaume. Katika taswira za namna hii, mwanamke mzuri ni yule anayeridhika na hali hii na kuikubali pasipo na malalamiko. Hii ni taswira anavyoita ya 'Maria Mtakatifu.' 'Maria mtakatifu' wa Bibilia hutumika katika uhakiki wa fasihi kumaanisha mwanamke mzuri, mpole, mtiifu kwa mumewe, bikira na kadhalika.

Katika taswira zote mbili, mwanamke amebaki kuwa kiumbe duni. Sawia na Chesaina na Lugano, Mbughuni pia anaiendeleza hoja kuwa taswira mbaya tunazozipata katika fasihi zinatokana na hali kwamba zinasawiriwa na maandishi wa kiume. Kwa hivyo, kulingana naye, wanawake tunaowapata wanawakilisha uovu wa kijamii au wanakuwa wanawake wa kinyumbani ambao wameridhika na hali hiyo. Tofauti na utafiti wetu, tumewahakiki wahusika wa kike katika maandishi ya wanawake ili kutathmini kama maandishi hawa wameendeleza taswira tofauti na maandishi wa kiume; hoja ambayo imeendelezwa na baadhi ya wahakiki tuliowataja hapo juu.

Kazi ya Brown (1981) ndiyo kazi ambayo kwa kiwango kikubwa imejishughulisha na uandishi wa kike. Kulingana na Brown, idadi ya waandishi wa kike wa kiasfrika ni ndogo sana ikilinganishwa na ile ya waandishi wa kiume. Kutokana na haya, uhakiki wa fasihi ya kiasfrika umekuwa finyu kwa vile ambavyo umetingwa na ubaguzi ambao unapendelea kazi za kiume. Katika hali hii, waandishi wa kike wamekuwa wakipuuzwa. Athari ambayo imetokana na hali hii ni kwamba badala ya kuwashughulikia waandishi wa kike kama waandishi, wahakiki wengi wamediriki kuwashughulikia wahusika wa kike katika fasihi. Hapa, jambo muhimu limekuwa ni kuchambua jinsi wahusika wa kike walivyo-sawiriwa na waandishi wa kiume. Kauli muhimu anayotoa Brown ni kwamba mchango wa wanawake katika fasihi haupatikani tu katika kipindi cha sasa. Wanawake wamekuwa wakitekeleza jukumu muhimu katika fasihi simulizi kama watamba hadithi, waimbaji na waigizaji. Majilio ya elimu na utamaduni wa kimagharibi yamesababisha kuondoka kwa wanawake kutoka kwa jukumu hili muhimu katika fasihi.

Hata hivyo, kuna waandishi wa kike ambao wamejitokeza ijapokuwa wamekuwa wakipuuzwa kiasi kwamba tunapongea juu ya fasihi ya kiasfrika, inaelekea kuwa tunazungumza juu ya fasihi ya wanaume pekee. Hali hii ni mbaya zaidi tunapowachunguza waandishi wa kike waandikao katika lugha ya Kiswahili. Katika kuwachambua waandishi mbalimbali, Brown anatoa hoja kwamba taswira za mwanamke kwa jumla katika fasihi zinatofautiana kwa kuwa baadhi ya taswira hizi zinajitokeza katika kazi za wanaume na kazi za wanawake. Kazi ya Brown imewashughulikia

waandishi wa riwaya waandikao katika lugha ya kiingereza. Tofauti na utafiti wetu, Brown hakujishughulisha sana na usawiri wa wahusika wa kike. Amewashughulikia waandishi hawa kwa ujumla. Sisi tumewahakiki kwa undani wahusika wa kike na mitazamo ya waandishi katika kazi tulizozichagua.

Taiwo (1984) anatoa rai kuwa waandishi wa kike hujaribu kuwasilisha hali ilivyo kwa njia ambayo inawakilisha maslahi na mtazamo wa Mwanamke. Waandishi hawa, anasema, wametoka sehemu mbalimbali za Afrika na kwa hivyo wanatumia mazingira yao kuwasilisha maoni yao. Kama Brown, anatoa hoja kuwa wasanii wa kike walitekeleza jukumu muhimu katika fasihi simulizi za jamii zao kongwe. Hoja nyingine muhimu anayotoa ni kwamba wanaume katika maandishi yao wameichora picha ya mwanamke ambayo inapaswa kuangaliwa upya kulingana na mazingira ya kitamaduni na ya dunia ya sasa; hasa mazingira ya kiuchumi. Kama Brown, Taiwo anawashughulikia waandishi wa riwaya waandikao kwa lugha ya kiingereza. Amejifunga zaidi katika upande wa maudhui kuliko usawiri wa wahusika. Hata hivyo, kazi hizi mbili zimechangia utafiti wetu kwa vile ambavyo zimewashughulikia waandishi wa kike.

Kazi ya Senkoro (1982) imewahakiki wahusika wa kike katika riwaya ya Kezilahabi ya Dunia uwanja wa fujo. Uhakiki wake na wa Lugano unatoa hoja zinazolingana. Vile vile Senkoro (1987) anagusia kwa ufupi usawiri wa wahusika wanawake katika fasihi ipatikanayo katika mfumo wa kibepari. Anatoa rai kuwa fasihi ipatikanayo katika mfumo huu daima humwonyesha mwanamke kama pambo la kutamaniwa na wanaume au kama kiumbe

duni ambaye jukumu lake kuu liko kitandani. Senkoro katika kitabu hiki hakuichambua kazi yoyote ya fasihi. Tofauti na uchambuzi wetu, tumewaangalia wahusika katika kazi maalumu.

#### 1.6 SABABU ZA KULICHANGUA SOMO HILI

Tumeamua kuchunguza swala la mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili kwa sababu kadhaa. Kwanza, zimetolewa hoja kuwa taswira mbaya za mwanamke zinazoendelezwa katika kazi nyingi za fasihi zinatokana na hali kwamba wengi wa waandishi hawa ni wa kiume. Kwa hivyo, kazi zao zimesheheni taasubi za kiume ambazo zinaendelezwa na jamii zao. Juu ya hayo, waandishi wa kiume wamesemekana kuwa wameshindwa kumsawiri mwanamke ipasavyo kwa sababu ni wanaume. Kwa kiasi fulani, maoni haya yanaoana na yetu, lakini pia tumeonyesha kuwa baadhi ya waandishi wa kike wanaendeleza taswira ambazo hatuwezi kusema zinaelekea kumletea mwanamke afueni (Tazama Chesaina 1987; Ndungo 1985 na Lugano 1989).

Sababu ya pili ni kwamba hakujakuwepo na tamthilia nyingi zilizoandikwa na wanawake hasa katika lugha ya Kiswahili. Hali hii imesababisha kukosekana kwa 'sauti ya kike' katika fasihi ya Kiswahili; zaidi ya ukweli kwamba wanawake kama waandishi wamepuuzwa. Tahakiki juu ya maandishi ya wanawake zimekuwa haba sana (Brown 1981 na Chesaina 1987). Kutokana na hali hii, kumekuwepo na pengo hasa kuhusu jinsi waandishi wa kike wanavyoichora picha ya mwanamke katika kazi zao. Tamthilia tulizozihakiki tumezichukulia kuwa kiwakilishi cha sauti ya kike katika maswala ya mwanamke.

Zaidi ya hayo, tumewahakiki waandishi hawa kama waandishi wa kisasa. Hapa, tunamaanisha kuwa waandishi hawa wanaandika baada ya nchi zao kujirejeshea uhuru. Uhuru ulitarijiwa kuleta afueni kwa watu wote; wanaume kwa wanawake. Hilo halijapatikana. Madhila ya ukoloni-mamboleo yameendelea kuwazongazonga wanyonge asilani. Katika hali hii, mwanamke anadhulumiwa maradufu. Kiuchumi, anaamwa jasho; kitamaduni itikadi za kijadi zimeendelea kumweka mwanamke chini ya utawala wa mwanaume. Tunatazamia kuwa mitazamo ya waandishi hawa itaashiria ujenzi wa jamii mpya. Je, katika jamii hii, mwanamke ana nafasi gani? Hawa ni waandishi wanaoandika katika mazingira yaliyojaa madhila katika viwango hivyo viwili tuli-vyovitaja. Kwa hivyo, uchambuzi wa wahusika wa kike umetuwezesha kuelezea juu ya maisha yao kama watu binafsi miongoni mwa wanajamii wengine kama yalivyowakilishwa katika tamthilia hizi.

#### 1.7 MISINGI WA NADHARIA

Utafiti wetu umejikita katika maisha ya wanawake. Wanawake hawapatikani wala kuishi nje ya jamii. Kwa hivyo, nadharia tunayoitumia haina budi kuwaangalia wanawake kama wanajamii. Vile vile, wanawake katika jamii wana nafasi waliyotengewa na jamii kama 'wanawake'. Kutokana na itikadi zinazoendelezwa na jamii ile, wanawake wananyanyaswa kwa misingi ya uana wao. Kuna kazi walizotengewa na ambazo zinachukuliwa kuwa duni na jamii. Mielekeo ya jamii kuhusu wanawake ni hasi. Kipengee cha uana kinamweka mwanamke katika

kitengo fulani. Nadharia tunayoitumia haina budi kuwa ile itakayofichua waziwazi madhila wayapatayo wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama 'wanawake'; yaani kama kikundi cha jamii.

Nadharia ni kigezo cha kutathmini jambo. Nadharia itakayotufaa sana ni ile ya ujamaa (wa) kike. Nadharia hii ni nadharia changamano ambayo ina misingi yake katika mawazo ya Marx na Engels na pia katika falsafa ya vikundi vya waitifaki wa ukombozi wa wanawake waitwao 'Feminists.'

Kulingana na Ruthven (1984:28), mtazamo wa kimarx huashiria ubepari (nyenzo za uzalishaji mali na umilikaji wa mali hiyo) kama kitovu na chanzo cha matabaka ya kijamii na kuwa chanzo cha dhuluma zote. Pia, nadharia ya Marx hupendekeza kuwa dhuluma dhidi ya wanawake zitaisha pale ambapo dhuluma dhidi ya wanyonge wote zitakuwa zimeondoshwa baada ya mfumo wa ubepari kuangamizwa (Reed 1970). Kulingana na nadharia hii, kugandamizwa kwa wanawake si jambo la kipekee lililo na historia na chanzo tofauti na kugandamizwa kwa wanyonge wengine kwa jumla ( tazama Engels 1972).

Hata hivyo, waitifaki wa mtazamo wa 'ki-feminist' hawaafikiani na mtazamo huu wa kimarx kuhusu kukombolewa kwa wanawake. Eisenstein (1975:5) anatueleza kwamba ugandamizwaji wa mwanamke na mwanaume ulikuwepo hata kabla ya majilio ya mfumo wa kibepari. Ugandamizwaji huu umeendelezwa kwa hali mbaya zaidi na mfumo wa sasa wa kibepari. Waasisi wa mtazamo huu wanashikilia kuwa lazima muundo wa jamii ya sasa uchambuliwe

ipasavyo iwapo dhuluma dhidi ya mwanamke zitaangamizwa.

Kundi la wanawake waitifaki wa mtazamo huu lenye siasa kali la New York ndilo linaloelezea msimamo wao waziwazi wanaposema:-

Hatuamini kuwa mfumo wa kibepari au mfumo mwingine wowote ule wa kiuchumi ndio chanzo cha ugandamizwaji dhidi ya wanawake wala hatuamini kuwa ugandamizwaji utatokomea kutokana na mapinduzi ya kiuchumi pekee (Ruthven 1984:7-8).

Ni dhahiri kuwa kila mojawapo ya mitazamo hii ina udhaifu wake kuhusiana na swala la ugandamizwaji wa mwanamke. Nadharia ya ujamaa (wa) kike (Socialist-feminism) kulingana na Eagleton (1986) huangazia udhaifu wa nadharia za kimarx kuhusu wanawake kwa lengo la kuzibadilisha. Nadharia hii huchukulia kipengee cha uana kuwa kiungo muhimu cha kazi yoyote ile ya kisanaa. Katika mkabala huu, fasihi inaweza kutupa mwangaza kuhusu tofauti za kiuana na kitabaka kama zipatikanavyo katika jamii. Kwa hivyo, pale ambapo Umarx unalenga usawa wa kitabaka kwa msingi ya kiuchumi, mtazamo wa 'ki-feminist' unaashiria usawa wa kiuana katika misingi ya kitamaduni.

Nadharia ya ujamaa (wa) kike huzingatia misingi ya ugandamizwaji katika tabaka la kiuchumi na pia katika mfumo wa utamaduni wa kuumeni (Patriarchal culture) unaomtwa mwaname na kumtweza mwanamke. Katika upembuzi wa namna hii, mfumo wa kibepari na mfumo wa kuumeni haitenganishwi wala kuchukuliwa kuwa kitu kimoja (Eisenstein 1979:22). Kwa hivyo, nadharia hii hushikilia kuwa kukandamizwa kwa mwanamke hakuna misingi yake tu katika uchumi: Lazima mhakiki azingatie mfumo

wa kuumeni kimuundo na kiitikadi. Kwa mtazamo huu, unyonyaji (exploitation) na unyanyasaji (oppression) ni dhana mbili tofauti zinazotegemeana. Unyonyaji huashiria hali halisi ya kiuchumi katika mfumo wa kibepari unaoendeleza matabaka ili hali unyanyasaji huashiria wanawake kama wanavyoelezwa katika mfumo wa kuumeni. Unyanyasaji basi hujumlisha unyonyaji na ugandamizaji.

Kwa jumla, nadharia hii husisitiza kuwa lazima kipengee cha uana, mbali na kipengee cha kiuchumi, kizingatiwe katika kulichambua swala la mwanamke katika fasihi. Kutokana na msisitizo huu, nadharia hii hupendekeza kuwa mbali na majukumu mengine ya fasihi yanayopendekezwa na nadharia za Ki-marx za fasihi ( tazama kwa mfano Ngugi 1981, Ngara 1985, na wengineo), fasihi inayojali kipengee cha uana itimize majukumu yafuatayo:

- a) Lazima kazi yoyote ya fasihi itumike kama jukwaa kwa mwanamke. Hivi ni kumaanisha kwamba kazi hiyo ieleze kwa uaminifu tajriba ya mwanamke ili kusaidia mtu yeyote yule kuielewa tajriba hiyo.
- b) Isaidie kuleta usawa wa kitamaduni na kiuana. Waitifaki wa nadharia hii husisitiza kuwa hawapigani nafasi zaidi kwa mwanamke katika muundo wa jamii ya sasa. Wanapigania muundo mpya wa jamii ulio na misingi yake katika amali za kibinadamu baadhi yazo zikiwa ni za kike za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.

- c) Iwasawiri wahusika ambao wanaweza kuigwa (provide role models) kwa kuwaonyesha wanawake ambao hawawategemei wanaume ili kujitambulisha au kufikia upeo wa maisha yao.
- d) Ikuze na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Kulingana na Chafe (1977:3) mbali na tabaka, uana ni mojawapo ya mambo muhimu ambapo mahusiano ya kijamii yanajengeka. Maisha yetu ya baadaye yanategemea kama tunazaliwa wanaume au wanawake.
- e) Izindue na kuanzisha mwamko kwa wanawake kwa kuonyesha hali halisi kuhusu heba ya mwanamke; jinsi anavyojiona, uhusiano wake na watu wengine na kadhalika.  
(Eagleton: 1986:172-173).

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu umejikita katika njia mbili maalumu. Njia ya kwanza tuliyotumia ni maktabani ambapo tulisoma mambo yanayohusiana na nadharia ya fasihi kwa jumla, nadharia za wanawake kwa jumla na pia tukazisoma kwa undani tamthilia ambazo tumezichambua.

Njia ya pili imekuwa ni kuhojiana na baadhi ya waasisi wa nadharia ya 'feminism' hapa nchini mwetu. Hawa wametupa mwangaza kuhusu nadharia hii kwa jumla na hasa jinsi inavyo- husiana na matatizo ya wanawake Barani Afrika.

2:0

SURA YA PILI

WAANDISHI WA KIKE WA KENYA

2:1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunatarajia kuwashughulikia waandishi wa Kenya. Hawa ni Ari Katini Mwachofi ambaye ameandika Mama Ee na Sheila Ali Ryanga ambaye ameandika Zinduko. Madhumuni yetu ni kuonyesha jinsi ambavyo waandishi hawa wanasawiri wahusika wao wa kike, mitazamo yao na jinsi ambavyo wanatofautiana kimawazo na kimtazamo.

Ili tuweze kubainisha na kutofautisha mitazamo ya waandishi hawa kikamilifu, tutawachambua kila mmoja baada ya mwingine.

2:1:1 A.K. MWACHOFI: MAMA EE.

HADITHI KWA UFUPI

Mama Ee ni mchezo ambao unazungumzia harakati za ukombozi wa wanawake. Ni mchezo ambao unatuonyesha wanawake katika harakati za kupigana vita dhidi ya yale yanayowadhalilisha, kuwagandamiza na kuwanyanyasa katika maisha yao ya kila siku. Harakati hizi zinaelezwa kupitia kwa mhusika mkuu Mwavita katika uhusiano wake na mumewe Kinaya na jamaa zao. Kupitia kwa mhusika huyu, dadake Tenge na mamake, mwandishi anajaribu kutuchorea picha halisi ya dhiki za namna mbalimbali zinazowakumba wanawake katika jamii ya kisasa.

Mchezo huu umegawanyika katika sehemu tatu muhimu:- utangulizi, sehemu ya kwanza na sehemu ya pili. Sehemu ya kwanza ni ile ambayo mwandishi ameiita utangulizi. Katika sehemu hii, mchezo unapoanza, jukwaani kumejaa fujo, mayowe na

vilio vya wanawake. Hawa ni wanawake ambao wako katika dhiki. Ibainike kuwa mmoja wa wanawake hawa ni mtoto mbichi wa kama miaka 16 hivi (uk.v). Hivi kuonyesha kuwa dhiki za wanawake zinatanda wanawake wa umri wa viwango vyote.

Mwanamke wa pili ana mtoto mchanga mkononi na amevaa vizuri ilhali wa tatu ana mtoto mgongoni, kikapu kikuu kuu begani na tita la kumi kichwani. Maelezo haya aliyotutolea mwandishi ni taashira ya dhiki za wanawake wa matabaka, umri na hali mbalimbali katika jamii. Wanawake hawa hawakupewa majina maalumu bali wanaitwa mke I, II na III. Hapa, imekusudiwa wawe wawakilishi wa wanawake wote katika matabaka, umri na hali zao. Lengo la mwandishi ni kuonyesha kuwa, mwanamke, pasipo kujali tabaka au hali yake ya kijamii ni mdhulumiwa.

Sehemu hii ambayo inawasilishwa kishairi ni sehemu ambayo tunaweza kuiita muhtasari wa mchezo mzima kwa jumla. Jambo linalokaririwa hapa ni kuwa wanaume ndio wanaoimiliki dunia na kila kitu kilichomo. Kutokana na hali hii, maisha ya wanawake ni biwi kubwa la takataka na hawana nafasi ya kupumua. Haya ni kinyume cha matarajio katika kipindi hiki cha historia, mathalani baada ya uhuru kwani katika harakati za kudai na kupigania uhuru walishirikiana bega kwa bega na wanaume, waka-mpiga vita na kumwondoa mkoloni kutoka nchi yao. Hata hivyo, baada ya uhuru kupatikana, wanaume wamewaweka wanawake katika nafasi ya pili na kuwatumikisha. Sasa wanawake wako katika njia-panda. Hali hii haiwezi kuvumilika tena. Ni lazima waungane na kupambana ili kuibadilisha hali ilivyo kama wasemavyo mke I na II:-

Haki tutapigania, hadi mwisho wa ulimwengu  
vipi wao wamilikia, raha za ulimwengu,  
Dini pia na sheria, mrututu twala uchungu  
Patupu twaambulia ila taabu na dhiki  
(Kwa sauti ya juu)  
Tumechoka, tumechoka, mzigo huu kuubeba  
na sasa twawatwika, vijana na kina baba  
Wapate nao kuchoka, wajue tabu kubeba  
Huku ukitukanwa, kunyonywa na kunyanyaswa  
Mizigo tuliyopewa, haya yetu maumbile  
Siyo ya kuongezewa, vibaya itukalile  
Mimba, wana kuzaliwa, miezi ya uwele  
Si mchezo, si masihara, ni mzigo mzito kubeba,  
(Kwa kelele)  
Wanawake tuungane, mabibi tuungane  
Haki zetu kuzidai, tusikubali kunyonywa...  
(uk. vii).

Dondoo hili linaonyesha kuwa wanawake wameamua kukataa dhuluma. Baadhi yao kama vile mke I na II walikuwa wamekata tamaa. Hata hivyo, mke III ambaye ni mwakilishi wa wanawake wa tabaka la wanaoishi mashambani bado hajakata tamaa na anawahimiza na kuwatia ari wanawake wenzake waipige vita hali ilivyo.

Sehemu ya pili ya mchezo huu ni ile mwandishi anayoiita sehemu ya kwanza. Sehemu hii inaonyesha taabu na dhiki za wanawake kama zinavyowakilishwa na Mwavita, Tenge na mama yao. Mchezo unaanzia pale ambapo Kinaya, Mumewe Mwavita, anafika nyumbani saa tisa za usiku (au labda tuseme asubuhi). Inabainika kuwa Mwavita amezunguka siku nzima akimtafutia mwanawe Juma dawa. Mtoto ameshikwa na ugonjwa wa ghafula. Mwavita amejaribu kumpigia mumewe simu kazini pasipo mafanikio. Kila mara anaambiwa hayuko ofisini. Mtoto amemlilia usiku mzima na hivi sasa ndipo anaanza kulala. Mwavita naye anajaribu angalau kupata lepe la usingizi. Kabla hajawahi, Kinaya anafika kwa fujo, matusi, dharau na vita huku amelewa

chakari. Hapa, inabainika kuwa Kinaya anamdharau mkewe sana. Zaidi ya kushuku kuwa ana mwanaume mwingine ndani, amejaa matusi:-

KINAYA: Jike gani hili nililooa? Kunifungulia mlango taabu na hata niingiapo linani- tazama kama niliyetapakaa mavi(uk.2).

Zaidi ya hayo, Kinaya anadai apewe chakula saa tisa za usiku; jambo ambalo Mwavita analikataa potelea mbali. Hii ni ishara kuwa wanawake wameamua kukataa dhuluma dhidi yao. Ugomvi unaanza baina yao na hapa ndipo tunapofahamu Kinaya hana lolote analotekeleza pale nyumbani. Ameitupa familia yake mkono. Hata chakula anachodai kwa vita hajui kitokako. Hawanunulii jamaa yake nguo wala halipii taa na maji. Mwavita, mkewe, ndiye aliyewachiwa mzigo huu. Kinaya anadai anafanya hivi kwa sababu amelipa mahari na kwa hivyo alichonacho Mwavita (hata yeye mwenyewe) ni mali yake. Zaidi ya hayo, Kinaya si mwaminifu katika ndoa. Amewahi kumwambukiza Mwavita ugonjwa wa zinaa ambao ameupata kutoka kwa wanawake wa mjini. Isitoshe, amejaribu kuwashawishi waajiri wa Mwavita wamwachishe kazi bila mafanikio. Haya yote yanaishia kwa Kinaya kumpiga Mwavita vibaya sana mpaka anamng'oa meno mawili na mimba aliyo nayo inaharibika.

Wakati huo huo, Tenge, mdogo wake Mwavita, amefukuzwa shule kwa kuwa ana mimba ya George; mwanafunzi mwenzake. George anapofahamu kuwa Tenge ana mimba, anamkwepa na kumkana. Tenge afikapo nyumbani, anakuta ku <sup>moto</sup> moto. Babake na kakake wanamwadhibu vikali sana. Mamake pia anaadhibiwa kwa kutomfunza bintiye. Ni Kinaya kuwa kakake Tenge anampiga kwani yeye

mwenyewe amewatia mimba wasichana watatu pale kijijini lakini hajapatilizwa kwa njia yoyote ile. Hatimaye Tenge anafukuzwa nyumbani na kuambiwa arudishe pesa zote alizolipiwa karo.

Mwavita atokapo hospitalini, anaenda kwa wazazi wake na hili linatuingiza katika hatua nyingine muhimu katika mchezo huu. Baraza la wazee, likiongozwa na mzee wa kijiji, linakutana ili kuwaamua Mwavita na Kinaya. Huu ni mkutano unaofuatia mwingine uliofanywa mwezi mmoja awali na ambao ulivunjika baada ya Kinaya kumtukana na kumpiga Mwavita mbele ya mama yake na kuwaita hao wazee "primitive". Katika mkutano huu, inabainika kuwa Mwavita amekosana na Kinaya juu ya ulevi, uasherati, matusi na kupigwa. Hata hivyo, mtoto wake Juma ameachwa kwa Kinaya na hili ndilo linalomshawishi kurudiana na Kinaya. Kinaya anafainiwa shilingi elfu tatu, ng'ombe, fahali, tembo na chai ya kina mama kwa makosa aliyoyafanya. Inaamuliwa Mwavita akae kwa mkazake mpaka Kinaya alipe faini hiyo yote. Hata hivyo, kutokana na dhiki ya moyo ya kutengana na mwanawe, Mwavita anarudi kwa Kinaya kabla masharti aliyowekewa hayajaitimizwa; jambo ambalo linawaudhi sana wazee. Anaporudi, mambo hayabadi- liki kabisa. Kinaya habadilishi tabia yake hata chembe. Mwishowe anampiga Mwavita baada ya ugomvi unaozuka anapokuta kuwa Mwavita hajajitayarisha kuandamana naye shereheni na kwamba nguo zake za sherehe hazijapigwa pasi. Ijapokuwa Mwavita ni mgonjwa sana, Kinaya hajali. Anachukulia kuwa Mwavita hakutaka kuandamana naye shereheni. Ugomvi huu unaishilia kwa Mwavita kupigwa sana mpaka mimba nyingine aliyo nayo inatoka. Hapa ndipo Mwavita anapofanya uamuzi wa mwisho wa kuachana na Kinaya pasipo kurudi nyuma.

Sehemu ya tatu na ya mwisho inahusu maisha ya Mwavita baada ya kuachana na mumewe na ya Tenge baada ya kufukuzwa shule. Usiku Mwavita anapoondoka kwa Kinaya, anaripoti kwa polisi lakini polisi wanamwambia kuwa hawajiingizi katika mizozo ya kinyumbani. Kuanzia hapa, anakabiliwa na wakati mgumu. Anasengenywa na kutengwa na wanawake wenzake; Kinaya hakomi kumsumbua Mwavita ambaye hata napo kanisani anatengwa. Juu ya hayo, Padre anakuja mara kwa mara kumshawishi arudiane na Kinaya akidai kuwa talaka ni kinyume cha sheria ya dini. Mwishowe, Mwavita anaamua kwenda mahakamani kutaka talaka na hifadhi ya mtoto wake. Kesi hii inasikizwa na hakimu ambaye ni rafiki ya Kinaya. Uhusiano huu unamnyima hakimu nafasi ya kutenda haki. Ijapokuwa talaka inatolewa na Kinaya kuzuiliwa kwa amri ya mahakama kwenda kwa Mwavita, hifadhi ya mtoto inapewa Kinaya. Mwavita hawezi kukata rufani wala kuongea na waandishi wa habari kwa kuhofu kuwa atapatikana na hatia ya kuivunjia heshima mahakama.

Uamuzi huu wa mahakama hauleti afueni kwa Mwavita kwani Kinaya hakomi kwenda kumsumbua nyumbani kwake. Inayumkinika kuwa Kinaya amepata cheo kipya na kwa hivyo polisi hawawezi kumshika. Mwishowe, akishirikiana na dadake Tenge, wanamkabili Kinaya na kumpiga vibaya sana na kumvua nguo zake; kitendo ambacho ni taashira kuwa mwanaume na wanawake ni binadamu sawa. Yale mengine <sup>ni</sup> na vinyago (masks) wanavyovalishwa na jamii ambavyo vinaficha utu wao halisi.

Tenge kwa upande wake anaanza maisha mapya. Anapata kazi na anaendelea kusoma ili kuimarisha ujuzi wake. Anatokea

mwanaume mwingine maishani mwake; Kheri ambaye ni tofauti sana na wanaume wale wengine na amekusudiwa kuwa kielelezo cha mwanaume mzuri kama inavyobainika katika maneno yafuatayo:-

MWAVITA: Yeye(Kheri) hana fikra za wanaume wa kikwetu. Ajiheshimu na naona awaheshimu sana wanawake. Hukumbuki tulipokuwa shule alivyokuwa akimfanyia mamake kazi zote hata zile ziiitwazo "za kike"---Ni mwanaume ndiyo lakini hana ubwana. Ndiyo tofauti yake kubwa na Kinaya... Yule ni mwanaume tangu utotoni mwake (uk. 86).

Kheri anachumbiana na Tenge. George pia anajitokeza tena maishani mwa Tenge huku akijaribu kumshawishi warudiane wamlee mtoto wao Jasiri. Hata hivyo, Tenge hayuko tayari kufanya hivyo. Anamzomea na kumsuta hadharani. Mchezo unaishia pale ambapo Mwavita na Tenge wanaamua kuwazindua na kuwaelimisha wanawake wenzao ili wajitolee na kupigania uhuru wao baada ya kugundua kuwa chama cha umoja wa kina mama hakitekelezi wajibu huu. Badala yake, ni chama cha wanawake wa mabwanyenye ambao wameukubali utumwa wa kimwili na kiroho. Malengo ya chama hiki hayana uhusiano wowote na matakwa ya wanawake wa kawaida ambao maisha yao ni ndoto moja kubwa.

## 2:12 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Katika kuichambua taswira ya mwanamke katika Mama Ee, tutawagawanya wahusika wa kike katika vitengo viwili; wanawake wazee wanaoshikilia na kuendeleza itikadi za kijadi kuhusu jukumu na nafasi ya mwanamke katika jamii na wanawake vijana ambao wana mawazo ya kisasa na ya kimapinduzi. Kwa kuzingatia

matatizo wanayokumbana nayo katika maisha yao ya kila siku na jinsi wanavyoyakabili, tutaweza kuuainisha mtazamo na msimamo wa mwandishi kuhusu swala la mwanamke.

Mojawapo ya taswira zinajitokeza katika tamthilia hii ni ile ya mwanamke kama 'mke' katika ndoa. Ndoa katika tamthilia hii ni za aina mbili. Kuna ndoa za kijadi kama vile ndoa baina ya mzee Tembo na Mamake Mwavita na Baba Kinaya na Mamake Kinaya. Aina ya pili ni ile ambayo tunaweza kuiita ndoa ya kisasa. Hii ni ndoa baina ya Kinaya na Mwavita. Ndoa ya kisasa kama inavyowakilishwa na ndoa baina ya Kinaya na Mwavita ina uwili. Kwanza, ada za ndoa ya Kiafrika zinatekelezwa kisha ada za ndoa za Kikristo zinafuatia. Kwa sababu jamii huwa na matarajio maalumu kwa mwanamke ye yote anayeolewa, inajitwika jukumu la kuwatayarisha na kuwafunza wasichana majukumu yao katika ndoa. Kulingana na Mbiti (1969:135), wasichana hufunzwa jinsi ya kutayarisha chakula, tabia kwa waume wao, jinsi ya kuwatunza watoto, jinsi ya kuwatunza waume wao na shughuli nyinginezo za kinyumbani. Wavulana, kwa upande ule mwingine hufunzwa kazi za 'kiume' kama vile kuchunga ng'ombe, jinsi ya kujipatia mali ambayo baadaye watakuja kuitumia kulipia mahari kwa wasichana watakaowao na majukumu yao kama viongozi wa familia. Kwa mujibu wa malezi ya namna hii, mwanaume anatarajiwa kutekeleza jukumu la kuipa jamaa yake chakula, kuwa mlinzi wao na hata kuwa mpatanishi baina ya bibiye, watoto wake, Mungu, pepo na mababu (Mugambi na Kirima 1976:49). Hili ni jukumu ambalo mamake Mwavita anajaribu kulitekeleza ipasavyo kwa mabinti zake wawili Mwavita na Tenge kama inavyodhihirika

katika maneno yake mwenyewe:-

MAMA: ...Tenge mwanangu, nimekufunza siku  
nyingi...dadako amekuonya na kukuonyesha  
mfano bora...ungekuwa ukinisikiza mimi  
bila komango masikini haya yasingetokea.  
Sikukuonya mimi? Eeeeh? Mara gapi nili-  
kukalisha chini nikakufunda? (kur. 10-11).

Katika jamii nyingi za Kiafrika, mafunzo haya huwa yanalengwa sio  
kumtayarisha mtoto wa kike kwa wajibu wake wa ndoa bali pia  
kumkinga asipate mimba kabla ya ndoa. Taswira hii ya mwanamke  
kama mke inaendelezwa kupitia kwa mamake Mwavita na Mwavita  
mwenyewe. Inavyodhihirika ni kwamba mwanamke anapaswa kuwa  
mtiifu kwa mumewe na kumridhia kwa mambo yote. Asipotekeleza  
jukumu hili, mwanaume ana haki ya kumpatiliza; wakati mwingine  
kwa kumpiga. Mugambi na Kirima wanaeleza hali hii vizuri wana-  
posema kuwa ikiwa mwanamke alikuwa mvivu, au aliwatesa watoto,  
mumewe alikuwa na haki ya kumpiga. Hali hii ndiyo anayohofia  
mamake Mwavita bintiye Tenge anapokuja nyumbani akiwa mjamzito:

MAMA: Ewe mtoto wa kike-umeniletea balaa  
na beluwa. Nitafanya nini? Nitaenda  
wapi? Ole wangu! Najuta kukuzaa...  
Leo ndiyo babako atatuchinja sote!  
(uk.10). (Msisitizo wetu).

Hauptiti muda mrefu kabla haya hayajatokea. Mzee  
Tembo anamkuta mama na bintiye njiani wakiomboleza hali ya  
bintiye na kuwapiga wote wawili barabara. Hili ni dhihirisho  
kuwa mwanamke analaumiwa na kuadhibiwa kwa kosa ambalo si lake.  
Kwa mfano, ijapokuwa jukumu la kuwatunza watoto linapasa kuwa  
la wazazi wote wawili, mtoto anapofanya makosa mamake ndiye  
anayelaumiwa. Jambo lingine linalobainika ni kwamba mwanamke  
katika jamii hii hana usemi dhidi ya mumewe.

Ndoa baina ya Mwavita na Kinaya, iwapokuwa ni ndoa ambayo inatarajiwa kuwa ya kisasa, ndiyo inayotudhihirishia taasubi za kiume zinazofungamanishwa na ndoa katika jamii anayoizungumzia mwandishi. Hii ni ndoa ambayo tungetarajia iwe kielelezo cha ndoa ya kisasa ambapo usawa baina ya mume na mke ungeheshimiwa. Kinaya na Mwavita ni watu ambao wamesoma sana. Mwavita amesoma hadi kidato cha sita na ana cheo kikubwa kazini. Kinaya naye amesoma hadi ng'ambo naye pia ana cheo kikubwa na mshahara mzuri kazini. Zaidi ya hayo, watu hawa wanaishi mjini. Miji katika muktadha wa Kiafrika inaambatanishwa na usawa na 'ustaarabu' (Little 1973). Kinyume na haya, Kinaya amesheheni taasubi za kiume za kijadi. Anamtarajia mke wake amnyenyekee, kumtii, na kumtumikia. Kwake, bibi ni mtumwa naye ni bwana. Asemalo sharti bibi yake alitii pasipo kuuliza maswali:-

KINAYA: Mimi ni mume wako na ndiye mwenye amri katika nyumba hii yangu. Lazima ufanye nisemalo. Usifikiri hiyo elimu yako na kazi ya mshahara imekufanya mume sawa na mimi. Tangu zamani mabibi zetu waliwatii mababu zetu. Vivyo hivyo, lazima nawe unitii mimi... Nilichoomba ni heshima na utif kwangu nikiwa mume wako wa ndoa (uk.3)(Msisitizo wetu).

Ni kinaya kuwa Kinaya anamtazamia mkewe kutekeleza wajibu wa kijadi wa ndoa ilhali yeye mwenyewe hayuko tayari kutekeleza wajibu wake kama mume. Kama tulivyotangulia kusema hapo awali, mwanaume ana jukumu kubwa la kutekeleza katika ndoa za kijadi. Ndiye anayewalisha, kuwalisha na kuwalinda mke na watoto wake. Kinaya kamwe hatekelezi haya. Yeye ni mume na baba tu kwa jina. Kwa mfano, hajui mkewe na mtoto wake wanakula

au kuvaa nini. Halipii taa wala maji. Pesa zake azipatazo anazitumia ulevini. Mkewe ndiye anayelichukua jukumu la mume katika nyumba yao. Kwa falsafa ya kijadi, angepasa kuwa ndiye 'mume' katika nyumba ile. Kinaya kama jina lake linavyomaanisha ni kinaya kikubwa.

Jambo lingine linalodhihirika hapa ni kuwa mwanamke kama mke huchukuliwa kuwa sehemu ya mali ya mumewe. Hili ni swala linalozuka kutokana na ada za jamii nyingi za Kiafrika kuhusu ndoa zinazomtaka mwanaume alipe mahari kabla ya kumwoa msichana. Wanaelimu-jamii wamejaribu kuutetea mfumo huu wa kulipa mahari kabla ya ndoa. Wengi wao hudai kuwa kulipa mahari si sawa na kumnunua mwanamke bali mahari huwa ni zawadi wanayopewa wazazi wa msichana kwa kazi nzuri waliyofanya. Kwa mfano Mugambi na Kirima (1976:49) wanasema:-

Mahari inapasa kuchukuliwa, sio kama ada ya ununuzi bali kama kitu kinachobadilishanwa na bibi arusi ambacho ni ridhaa kwa familia ya bibi arusi kwa kumpoteza na kupoteza huduma zake. Ilikuwa ishara ya shukrani kwa kupata zawadi ya bibi na mama.

Maelezo ya mahari kama haya yana utata. Waasisi wa mtazamo huu wanakubali kuwa mahari ni ridhaa kwa 'huduma zitakazokosekana' kutokana na kuolewa kwa msichana. Katika baadhi ya jamii za Kiafrika kama vile jamii ya Mayombe ya huko Congo, kiwango cha mahari kiliwekwa kutegemea kazi na majukumu mwanamke na watoto ambao angewazaa waliyotarajiwa kutekeleza (Mugambi na Kirima 1976). Ni maoni yetu kuwa mahari ilikuwa njia moja ya kumfunga mwanamke kwa mumewe. Mahari yote au sehemu yake ilipaswa kurudishwa ndoa ilipovunjika. Juu ya hayo, katika jamii nyingine,

mahari inamfungua mwanamke kiasi kwamba mumewe afapo, inamlazimu kuolewa na ndugu zake. Huwa anamilikiwa kama sehemu moja ya mali ya mumewe.

Mwachofi katika mchezo huu haonekani kutambua ukweli huu. Hili ni jambo mojalinaldtufanya tuseme kuwa yeye, kama mwandishi wa kike, yuko katika njia panda. Kupitia kwa mhusika wake mkuu Mwavita, anawambia:-

KINAYA: ...Wanawake wengine hawazioni ingawa wafanya kazi - wapewa na mabwana zao za kutosha kununua chakula tu. Zilizobaki afutika bwana maana alilipa mahari...mwanamke hana chake. Akishaolewa kila kitu hata yeye ni mali ya bwanake. Ndiyo sheria ya kikwetu. Wacha uzungu hapa.

MWAVITA: Mbona mababu zetu hawakufikiria hivyo? (uk.4).

Mtazamo wa Kinaya kuhusu mahari ndio unaowakilisha falsafa ya jamii kongwe kuhusu mahari. Waandishi wengine wa kike wa Kiafrika wameiona ada hii kama bei. Kwa mfano, Efua Sutherland katika The Marriage of Anansewa (1987) anaichukulia ada hii kama njia ya kujitajirisha kwa mababa ambao mabinti zao wamefikia umri wa kuolewa kutokana na jinsi anavyomsawiri babake Anansewa.

Mahari inapotolewa, mwanamke anatarajiwa amnyenyekee, kumtii na kumsujudia mumewe. Mawazo ya mjomba wa Mwavita anapomwuliza "kwa nini wewe kumwonyesha mumeo ujeuri? Hujui alikuoa kwa mali" (uk.35) ni dhihirisho kuwa haya ndiyo matumainio kwa mwanamke aliyelipiwa mahari. Jukumu hili linaelezwa vizuri na nyanyake Mwavita anapomsuta:-

NYANYA: Mwavita somo, kwa nini kumnyima mumeo chakula? Hiyo ndiyo kazi yako. Kumpikia bwanako na wanao. Hata kama mlevi namna gani, lazima umpe chakula (uk. 35).

Haya yote ni kwa sababu Kinaya amelipa mahari.

Akieleza hali hii, Taiwo (1984) anasema kuwa ni kutokana na umuhimu jamii kongwe inayowekea jukumu la baadaye la msichana kwamba haimruhusu kujichagulia mume. Taiwo anazidi kufafanua:-

Katika hali hii, (mwanamke) anakuwa chombo cha kunadiwa bei. Ikiwa patakuwepo mapatano na yule mwanamke anaolewa, anatazamiwa awe mtiifu na mnyenyekavu (Taiwo 1984:2).

Maoni yetu kuhusu swala hili ni kinyume na haya ya Mwachofi. Tunaamini kuwa mahari ni ununuzi. Ikiwa tutachukulia mawazo ya Mwavita na ya baraza kuwakilisha maoni ya mwandishi mwenyewe basi haiyumkiniki kuwa baraza linalomwambia Mwavita kuwa Kinaya ni mumewe aliyemuo 'kwa mali' ndilo hilo hilo linalomsuta na kumkemea Kinaya kwa kumwuliza yule aliyemfunza eti kuo ni kununua. Mwandishi hapa anaonekana kutokuwa na msimamo thabiti kuhusu swala hili la mahari.

Mwanamke katika ndoa pia anachukuliwa kuwa mtumwa na pambo kwa mumewe. Taswira hii inajitokeza kutokana na matarajia ya Kinaya kwa mkewe. Tumeshataja kuwa Kinaya daima hufika nyumbani amechelewa au wakati mwingine hafiki kabisa. Pindi afikapo hata iwe ni saa ngapi za usiku, Mwavita anawajibika kuingia jikoni kumtayarishia chakula. Isitoshe, Kinaya afikapo nyumbani, anamtarajia mkewe amlaki mlangoni na kumpokea mzigo hata iwe ni saa ngapi. Mwavita wakati mwingine anabidika kukaa macho mpaka usiku wa manane huku akimngoja mumewe. Haya yana-  
mtia Mwavita jeraha la moyo kama anavyoeleza:-

Sababu ya pili ni ulevi. Huu ndio unaotukosanisha siku zote. Kinaya haishi kulewa na kufika nyumbani usiku wa manane au hata asubuhi. Aweza pia kuketi siku mbili hatujamwona hasa mwisho wa mwezi. Nimekuwa na wasiwasi hata nikazoea. Wenzangu wakaniambia nitashikwa na ugonjwa wa moyo bure kwa ajili ya wasiwasi. Mwanzo mwanzo alikuwa akichelewa silali naona labda amepigwa na wakora wa mjini au labda amepinduka na gari. Tena siku hizo alikuwa akiomba msamaha lakini siku hizi...Nikimwuliza alicheleweshwa na nini, kutazuka kondo nipigwe nitolewe nje (uk.31).

Hapa, Kinaya anakuwa ni kama Mungu wa pili kwa Mwavita. Hisia za ubwana zimemwingia kiasi kwamba Mwavita kwake anakuwa kama mwanasesere wa kumchezesha jinsi atakavyo. Kinaya ni mjeuri kupita kiasi. Gari lake lisikikapo, lazima mkewe akimbie kumfungulia mlango hata iwe ni saa ngapi za usiku kama inavyodhihirika katika maneno yake:-

KINAYA: (nje) We mwanamke fungua mlango haraka. Wasema na nani huko Ee? Kwani hukusikia gari langu au lazima nibishe ndipo nifunguliwe? Fungua haraka ama sivyo nikiingia humo utajikuta nje bila kujua ulifikaje huko...  
...  
Jike gani hili nililoowa! Kunifungulia mlango taabu na hata niingiapo ananitamama kama niliyetapakaa mavi. Nilichobeba hatizami. Ulikuwa na nani hapa ndani nilipoanza kubisha? Ee? Sasa umemkasirikia nani Ee? Nini sasa? Una nini? (uk.2).

Vitisho vya Kinaya ni ujeuri, ukatili na unyama usio kipimo; na haya yote ni kwa sababu Kinaya amelipa mahari. Hapa, ni dhahiri kuwa mwanamke kwake ni mtumwa na kikaragosi cha kucheza atakavyo. Pengine unyama na ujeuri wa Kinaya unajitokeza waziwazi zaidi kwa jinsi anavyomchukulia bibi yake

kama pambo juu ya kuwa mtumwa. Huu ndio mwelekeo alio nao pia kwa wanawake wote. Inajiri kuwa Kinaya hakufika nyumbani siku iliyotangulia. Leo hii amefika nyumbani mwendo wa saa kumi na mbili kumchukua mkewe Mwavita wahudhurie sherehe fulani. Wakati huo Mwavita amebanwa na ugonjwa na anaugua sana. Chochote akulacho anatapika. Kichwa kinamuuma sana. Fauka ya haya yote, mawazo yake yako kwa nguo za mumewe ambazo bado hazijapigwa pasi. Anajua yale yatakayotokea mumewe akija akute hazijapigwa pasi. Haupiti muda mrefu kabla haya hayajatokea. Ijapokuwa Kinaya hakulala nyumbani, hamjulii mkewe hali. Mawazo yake yako juu ya sherehe:-

KINAYA: Mbona unalala hapo kitini na saa za kuhudhuria sherehe zimefika? Huendi? Husemi na mimi? Mbona hujajitayarisha? Ndivyo ufanyavyo siku zote ili nikuache hapa useme nawafuata wasichana shereheni. Inuka haraka kavae nguo twende (uk.48).

Baadaye anapomwuliza ikiwa yu mgonjwa ni kujitia huruma za mamba. Ijapokuwa anajionea kwa macho yake mwenyewe Mwavita akitapika, jambo linalomshughulisha zaidi ni iwapo ataandamana naye shereheni kama wafanyavyo wanaume wale wengine:-

...Sasa huendi na mimi sivyo?  
Wenzangu wote watakuwa na wake zao  
ni mimi peke yangu kama ambaye sijaoa.  
Aibu gani hii? (uk. 49).

Kinaya hana huruma hata kidogo. Anachojali zaidi ni kuonekana shereheni na mkewe au labda na 'ua' kama wanaume wale wengine. Anachoweza kumwambia Mwavita ambaye ni mgonjwa ni kuwa atajipatia maua mengine huko shereheni na abaki na 'naumwa' zake. Hachelei kumpiga Mwavita anapogundua kuwa nguo zake

hazijapigwa pasi. Huu ni ubaradhuli na uhayawani uliovuka mipaka kwa sababu Kinaya anajua kuwa Mwavita ni mgonjwa. Anatarajia hata akiwa mgonjwa sio tu amtumikie bali pia aandamane naye ili aweze kuonekana na mkewe kama wenzake. Hatuoni sababu inayomfanya Kinaya asijipigie pasi au kukosa kuhudhuria hiyo sherehe hasa wakati huu ambapo mkewe ni mgonjwa.

Mwanamke amejitokeza pia kama chombo cha kutimizia ashiki za kiume. Uwezo wa mwanamke wa kuzaa ni chombo kinachotumiwa na jamii iliyosheheni taasubi za kiume kuendeleza ugandamizaji dhidi yake. Eisenstein (1979:6) anatueleza:

Hakuna harakati zozote za kijamii anazoshiriki mwanamke zinazoweza kueleweka nje ya mahusiano ya kijamii ambayo anawakilisha na ambayo ni kionyesho cha itikadi ya jamii. Kwa mfano, kitendo cha kuzaa kinaitwa kitendo cha umama (an act of motherhood) Ikiwa kinahusishwa na ndoa na jamaa. Lau sivyo, kitendo kile kile kinaweza kuitwa "uzinzi" na mtoto anayezaliwa kuitwa "mwanaharamu".

Katika tamthilia hii, taswira ya namna hii inajitokeza kupitia kwa Tenge, Mwavita na mama yao. Kulingana na mila za Kiafrika, mwanamke anatarajiwa awafunze watoto wake wa kike ili wasiye wakacheza na wanaume na kupata mimba nje ya ndoa. Msichana akipata mimba nje ya ndoa, anaitwa malaya na mama yake ndiye anayelaumiwa kwa kutomfunza jinsi ya kujitunza. Tenge, kwa mfano, anapotiwa mimba na George, George halaumiwi. Haja yake ilikuwa tu kujifurahisha ndiposa akamhadaa Tenge. Tenge kwa upande ule mwingine anasukumiwa lawama zote. Zaidi ya hayo, anafukuzwa shuleni huku George anaachiliwa kuendelea na masomo hadi chuo kikuu. Isitoshe, mwanawe anaitwa mwanaharamu naye

Mwavita anajitoa mhanga kwa ajili ya mwanawe. Hii yake inakuwa ni ndoa yenye hatari kwa maisha yake. Huruma za mwanamke zinakuwa chanzo cha dhuluma dhidi yake. Hapa, ni wazi kuwa uzazi ni furaha kwa mwanaume na dhiki kwa mwanamke. Kwa mfano, katika ndoa hii ya Mwavita na Kinaya, Kinaya ndiye anayemfurahia Juma huku akijigamba ni mwanawe ijapokuwa hamlishi wala kumvika. Kwa Mwavita, ndoa inakuwa ni pingu ambazo hawezi kuzivunja.

Kinaya na George ni vielelezo vya jinsi jamii inavyomchukulia mwanamke kuwa chombo cha kutimizia ashiki za kiume. Inaelekea kuwa Mwavita anakuwa muhimu tu kwa Kinaya pale tu ambapo anajifurahisha naye. Huu ndio hasa mwelekeo wake kwa wanawake wote. Kwake, wanawake ni maua na hii ndio sababu anawachezea wanawake wengi mpaka mwishowe anamwambukiza mkewe ugonjwa wa zinaa. Hana hata mercury? zaibaki za uso anapomtisha Mwavita kuwa asipoandamana naye shereheni, atajipatia maua mengine huko. Kwake, wanawake ni maua ambayo yanachunwa yanaponawiri na kutupwa yakinyauka. George naye anajifurahisha na Tenge na kumkimbia huku akidai kuwa mimba si yake.

### 2:1:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii anayoishughulikia na maswala mbalimbali kuhusu jamii ile huweza kufahamika kutokana na wahusika anaowaumba. Mary Eagleton (1986:104) anatueleza:-

Mwandishi wa tamthilia wa kike hasimami jukwaani yeye binafsi na kutoa hotuba kwa sauti yake huku akitoa maoni yake bali anajishughulisha na jambo ambalo linakisiwa kuwa tisho kubwa zaidi: hutoa matini na

maana ambazo lazima wengine wazifuate. Katika sauti yake mwenyewe ambayo huonekana kupitia kwa mazungumzo ya wahusika na umbo la mchezo wenyewe, anawasiliana na hadhira yake. Anazidhibiti sauti za wengine. Anawapa wahusika maneno ambayo ni lazima wayazungumze.

Wahusika wote wa kisanaa hufinyangwa na msanii mwenyewe ili waweze kuwakilisha mawazo, falsafa na dhana fulani. Hizi dhana huwa zimetokana na tajriba yake mwenyewe katika jamii. Tunapojihusisha na fasihi ya kike, kwa maoni ya Monteith(1986:3) tunapaswa kutambua umuhimu uliopo baina ya mazingira ambapo kazi hiyo imezuka na kazi ya mwisho tunayopata kutoka kwa mwandishi na pia uhusiano wake na maswala maalumu yanayowakabili wanawake. Anachosema Monteith hapa ni kuwa kila kazi ya fasihi, na hasa fasihi ya kike, ni zao la mazingira maalumu na kwa mwandishi wa kike, mazingira na hali yake maalumu katika jamii humpa tajriba maalumu ambayo haipo kwa mwandishi wa kiume.

Maoni haya tunayaunga mkono kwani kila kazi ya fasihi ina kipengee cha uana. Katika jamii, mtu anapoitwa mwaname au mwanamke huwa amewekwa katika kitengo fulani cha kijamii. Katika kila mojawapo, kuna falsafa na itikadi zinazotawala mahusiano katika kitengo chenyewe na pia maingiliano yake na kile kingine. Katika mkabala huu, swala la mwanamke linakuwa swala la kisiasa. Mtu anaposema 'mwanamke', kuna mawazo na itikadi zinazohusishwa na 'uanauke'. Inavyobainika katika maisha ya kila siku ni kwamba wanawake wanadunishwa na kudhulumiwa katika jamii. Kutokana na hali hii, mwandishi wa kike anapoamua kuandika anaandika kama mwanachama wa kundi maalumu la kijamii ambalo linadunishwa na kudhulumiwa. Anaandika kazi

ya kisanaa ambayo imeathiriwa na ile hali ya kuwa yeye ni mwanamke na kama mwanamke jamii yake ina nafasi iliyomtengoa. McLaughlin (1990:155) anaeleza hali hii ifuatavyo:-

Dhana ya mwanamke ni dhana ya kisiasa.  
Haelezi tu uana. Inaelezea hadhi yake katika jamii.  
(The term woman is a political term.  
It does not simply describe sex or gender.  
It defines status in society).

Tunapochunguza mchezo wa Mama Ee, tutaona kuwa kupitia kwa wahusika wake, Mwachofi anazichunguza ada nyingi za kijamii na kidini katika jamii yake na kuendeleza hoja kuwa ada hizi zinamnyima mwanamke nafasi ya kuishi kama binadamu mkamilifu katika jamii ile. Kupitia kwa wahusika kama vile Mwavita, Tenge na mama yao katika uhusiano wao na wanaume kama vile Kinaya, George na mzee Tembo, mwandishi anatudokezea kuwa katika jamii anayoizungumzia, lazima mwanamke akubali nafasi ya pili nyuma ya mwanaume ambayo amewekewa na ada za jamii hiyo. Mwavita, kwa mfano, ameolewa na Kinaya na ijapokuwa hii ni ndoa ambayo haina faida kwake, jamii yake haiwezi kumkubali yeye kama mtu binafsi. Lazima ajifungamanishe na mwanaume ndipo aweze kutambulikana katika jamii ile. Asipofanya hivi, anakuwa uvundo katika jamii yake. Anapoachana na Kinaya, jamii yake inamtenga. Kwa mfano, mkazake na wanawake wenzake wanamtenga kama anavyotwambia:-

MWAVITA: ...Pili, wake wenzangu wananiona mimi mbaya. Wengi huja hapa kunishauri nimrudie Kinaya. Ati mimi ni mshindani na nina moyo wa kujivuna ambao ni mbaya mke kuwa nao ( uk. 58).

Maneno haya ya Mwavita ni ishara kuwa hata wanawake wenyewe ni waumini wa mila za kijamii ambazo zinamtaka mwanamke amvumilie na kuishi na mumewe hata ikiwa anamtesa.

Tenge naye haepuki ubaguzi wa namna hii. Anatwambia:-

TENGE: ...Wengine hunijia na kuniambia ati mwanangunimpeleke kwa George. Miaka yote mitatu na zaidi iliyopita nikataabika sasa mwanangu ajua kusema ati amekuwa wa George (uk. 59).

Kwa maoni ya mwandishi Mwavita hamhitaji Kinaya wala Tenge hamhitaji George kwa vyovyote vile. Hii ni sawa na kusema kuwa si lazima mwanamke ajifungamanishe au kumtegemea mwanaume ili maisha yake yakamilike. Hili ni jambo ambalo mwandishi ye yote wa kike aliyemakinika anabidika kufanya. Hana budi kuwasawiri wahusika wa kike ambao wanafikia upeo wa maisha yao pasipo kuwategemea wanaume ili wawe mfano kwa wanawake wenzao ambao wanadhulumwa. Mwavita kwa mfano, ametambua hali yake duni katika ndoa, jamii na dini na amefika ukingoni:-

MWAVITA: Wajua mama, wake wataendelea kunyanyaswa na mabwana kwa kutojua haki zao. Wengi washakubali kuwa wananchi wa tabaka la chini. Ati ndiyo Mungu alivyotuumba. Wake kama hao huchukua waume kama miungu. Mtu kama mimi huchukuliwa kama mwasi. Nimeasi dini gani? Kuabudu wanaume. (Kwa hasira) kuma nina zao! Simwabudu mume ye yote! ( uk. 59).

Zaidi ya kutengwa na wanawake wenzao, Mwavita na Tenge wanatengwa pia na dini. Mwavita anakatazwa kupokea sakramenti ilhali Tenge anaambiwa mtoto wake hatabatizwa. Dini kama inavyowakilishwa na padre katika tamthilia hii imejaa unafiki na uzozo wa kila namna na ni chombo kinachotumiwa kuendeleza

dhuluma dhidi ya wanawake. Hii ni dini inayompendelea Kinaya na George na kuwabagua Mwavita na Tenge. Kwa mujibu wa dini hii, mwanamke kila mara ndiye mkosa. Dini kama hii haina budi kupigwa vita iwapo ukombozi wa wanawake utapatikana.

Hapa, mwandishi anatudokezea udhia wake kama mwandishi ambao anauelekeza kwa taasisi za kiume ambazo zinayatawala maisha ya wanawake. Anafanya hivi sio tu kupitia kwa lugha anayowapa wahusika bali pia kupitia kwa wahusika binafsi anaowaumba. Kwa kusheheni hisia za uasi, Mwavita na Tenge wanaiping' hali hii ambayo imewavua utu wao na wameamua kuwa hawataubadi- lisha utu wao kwa utumwa. Kupitia wahusika hawa, mwandishi anatuchorea wanawake ambao wanaiepuka hatima waliyowekewa na jamii isiyoyajali maslahi yao. Kupitia kwao, Mwachofi anai- shambulia vikali jamii ambayo inaendeleza ubaguzi wa kiuana.

Anawaumba Mwavita na Tenge kama wanawake huru, wanaoji- tegemea kiuchumi, wanaofanya kazi na ambao wameamua wanaweza kuyaendesha maisha yao pasipo kuwategemea wanaume. Wameamua kuivunja mikatale na pingu wanazotiwa na ada za kijamii na kidini.

Mamake Mwavita katika tamthilia hii anawakilisha mwan- mke mzuri katika jamii kongwe. Anayavumilia mapigo ya mumewe mzee Tembo pasipo kulalamika ijapokuwa hana hatia. Kwa kui- kubali hali hii duni, mamake Mwavita si mfano wa kuigwa na Tenge na Mwavita. Hata baada ya kuondoka kwa Kinaya mara ya pili, mama bado anafikiria kuwa Mwavita ataolewa tena. Mwavita ambaye jina lake kijazanda linamaanisha "vita" ni kielelezo kwa

wanawake wengine ambao wanaambiwa kuwa ni lazima wazivunjilie mbali silisili zinazowafunga na kung'ang'nia uhuru wao. Pingamizi zao kuhusu jamii zao zinajengeka kutokana na mikinzano inayodhihirika katika majukumu yao kama wanawake.

Fasihi tumikizi hulenga mapinduzi ya kijamii ambayo yataleta afueni kwa wale wanaodhulumiwa. Kama anavyosema Chinua Achebe (1975:79):-

Mwandishi wa Kiafrika hawezi  
kujifanya kutojua au kutojali  
uvunjali wa haki za watu wake uliosakini.

Vivyo hivyo, mwandishi wa kike wa Kiafrika hawezi kuyakwepa au kuyapuuza maswala ya wanawake wenzake ambao wananyimwa haki zao kama binadamu na mifumo ya kiuchumi na kitamaduni iliyosakini katika jamii hizi. Je, Mwachofi anayaonaje mabadiliko ya jamii yake? Kwa maoni ya mwandishi, wanawake wanapasa kueliminishana na kuungana ili waweze kuikabili na kuibadilisha hali yao. Ili kufanikiwa katika lengo hili, hawana budi kuungana na kuwapiga vita adui zao; na adui wa kwanza ni mwanaume.

Mke I + II: ...Wanawake tuungane, mabibi  
tuungane  
Haki zetu kuzidai, tusikubali kunyonywa...  
(uk. vii).

"Umoja wa wanawake hoyee" (uk. 98) ndiyo maneno ya mwisho ya mchezo huu na ni dhihirisho la imani ya mwandishi kuwa uhuru wa wanawake utapatikana kwa kuungana na kumpiga adui wao vita kwa pamoja. Hata hivyo, sharti wanawake wazinduliwe ili waweze kutambua adui kwanza. Tenge anatwambia:-

Kabula ya kupigana, tujue zetu adui  
mmoja wa kupambana, yu ndani mwetu mui  
Ni ujinga kutubana, haki zetu hatujui  
Kwa shime tuujenge, umoja wa wanawake.  
(uk. 96).

Mwachofi katika mchezo huu anadai wanawake wapewe nafasi sawa na wanaume ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa jamii zao. Anawasawiri wahusika wa kike ambao wanafaulu kuivunja mikatale ya kiuana na kupata afua bora na zinazowaridhisha badala ya ndoa.

Hata hivyo, udhaifu mkubwa wa mchezo huu ni kwamba mwandishi anaonekana kutokuwa na msimamo thabiti kuhusu maswala fulani ya kijamii. Katika hali hii, anaonekana kukwepa kutoa msimamo wake kuhusu baadhi ya maswala haya. Swala moja kati ya haya ni nafasi ya mahari katika ndoa. Kupitia kwa mhusika wake mkuu Mwavita, tumeona kuwa mumewe Kinaya anatumia hiki kama kisingizio kumnyanyasa. Hata hivyo, Mwavita anapomwambia Kinaya kuwa mababu zao hawakufikiria kuwa kutoa mahari ni kununua, hapa inaonekana kuwa mwandishi haoni athari inayotokana na ada hii katika maisha ya mwanamke katika ndoa. Yeye haoni mahari kama mojawapo ya ada za kijamii zinazoendeleza dhuluma dhidi ya wanawake.

Jambo lingine ambalo linatatanisha katika mchezo huu ni kwamba ijapokuwa Mwachofi anaonyesha kuelewa hali ya mwanamke katika jamii yake ya barabara, haonyeshi kulishughulikia swala hili katika marefu na mapana yake. Kulichukulia swala la ugandamizwaji wa wanawake kuwa na misingi yake katika uana tu ni dhana ambayo haichambui vilivyo maswala na mifumo mbalimbali ya kijamii kama inavyobainika katika jamii mbalimbali za ulimwengu. Katika baadhi ya jamii za ulimwengu, ugandamizwaji

wa wanawake unazidishwa na jinsi jamii hizo zilivyogawanyika kutokana na athari za ukoloni, umwinyi, dini, mikoa, 'caste', na kadhalika. Athari hizi hazionekani kuwa na maana yoyote kwa Mwachofi ambaye anaonelea kuwa tatizo la mwanamke linatokana na mwanaume. Katika tamthilia yake hii, haonekani kutilia maanani mfumo wa ubepari au mifumo mingineyo ambayo inamfanya mwanamke kudhulumiwa mara mbili au zaidi. Kwa sababu mfumo wa kuumeni ni mojawapo tu ya mifumo inayotubainishia mahusiano mbalimbali katika jamii, haitoshi kusema kuwa wanaume ndio wanyanyasaji pasipo kueleza kuwa ni wanyanyasaji kwa sababu wanasimamia mahusiano katika mifumo fulani ya kijamii na kiuchumi. Kama mwanaume angeishi nje ya ya jamii ambayo inazua na kuendeleza mifumo mbalimbali, angekuwa gamba tupu. Kwa hivyo, ni lazima swala la mwanamke liambatanishwe na mifumo yote inayopatikana katika jamii na ambayo inaathiri nafasi na jukumu lake kama mwanamke.

Kwa kumalizia sehemu hii, tungependa kusema kuwa Mwachofi ana matumaini kwa mwanamke ikiwa atajaribu kujitegemea kiuchumi. Hata hivyo, anaonekana kuyumbayumba katika msimamo huu anapomuumba mhusika Kheri ambaye anakusudiwa kuwa kielelezo cha mwanaume mzuri katika jamii. Kheri amesanifiwa kama mhusika ambaye anawaheshimu sana wanawake. Tangu utotoni mwake, amekuwa akimfanyia mamake kazi ambazo huchukuliwa kuwa za kike. Mwandishi, kupitia kwa Mwavita anawambia:-

MWAVITA: ...Yeye hana fikra za wanaume wa kikwetu. Ajiheshimu na anawaheshimu sana wanawake ...

...

Kheri ajua kuwa mke ni mtu kama yeye ...

...

Mimi dada, wanaume karibu ya wote nawaona wana uhayawani. Lakini nafikiri wako wachache, wachache sana ambao macho yao ya wazi wanauona na kuuheshimu utu wa kike ... huyu Kheri naona ni mtu ana utu (kur. 86-87).

Pengine Mwachofi anamuumba mhusika Kheri kwa kutambua

kuwa mwanamke hawezi kuishi wala kuwa huru nje ya mahusiano na maingiliano yake katika jamii na mwanaume. Hata hivyo, Kheri ni mhusika ambaye ni wa kulazimishwa na haaminiki kwa sababu kadhaa. Kwanza, anazuka kutoka ughaibuni na kutoweka huko huko. Hivi ni kumaanisha ya kwamba mwandishi hajamuumba, kumkuza na kumwendeleza vya kutosha ili kuweza kulibeba jukumu hili. Pili, baada ya kutuonyesha kuwa wanaume ni wabaya na hawajali maslahi ya wanawake, Kheri hawezi kuaminika kuwa ni tofauti na wengineo kwani amebobezwa mawazo na taasubi kama wanaume wale wengine na jamii iliyomkuza. Alivyosanifiwa ni kama mhusika anayeishi katika kisiwa ambacho kimetengana na jamii hiyo. Katika mfumo wa kuumeni na mfumo wa kibwanyenye, mwanaume wa namna hii hawezi kuaminika, wala kukubalika katika jamii yake.

Kwa kumleta mhusika kama Kheri, inaonekana kuwa

mwandishi ameivunja ile imani yake kuwa mwanamke hamhitaji mwanaume ili kujiendeleza. Licha ya haya, Mwachofi amefaulu kuingiza mtindo mpya katika uandishi wa kike. Lugha na wahusika

ambao ametusanifia ni vyombo ambavyo amevitumia kwa usanifu mkubwa ili kuwasilisha ujumbe wake. Ameteua lugha ambayo inawasilisha hisia zake kama mwandishi wa kike na ambayo kwa marefu na mapana inawakilisha hisia za wanawake wanaodhulumiwa katika jamii. Kwa kuwapa wahusika wake lugha ya namna hii, Mwachofi amefaulu kuwaumba wahusika wa kimaono ambao wanawakilisha falsafa yake kama mwandishi.

2:2 S.A. RYANGA: ZINDUKO

2:2:1 HADITHI KWA UFUPI

"Mchezo huu wa Zinduko unaonyesha jinsi kukua na kuimarika kifikra kunavyoweza kusaidia kuondoa mbegu mbaya katika jamii kama vile utumiaji wa hongo ili kuwavuta wafuasi. Mwandishi amefaulu kuonyesha 'mwamko mpya wa kisiasa' na umuhimu wa kuthamini 'ukweli' na 'utu'."

Haya ni maneno ambayo yanapatikana katika jalada la nyuma la kitabu hiki. Zinduko ni mchezo ambao unasimulia kisa cha wanasisia ambao wakichaguliwa na wananchi husahau ahadi walizotoa na kuwasaliti waliowachagua. Pindi washikapo madaraka, wanachojishughulisha nacho ni kuwanyonya na kuwanyanya wananchi kupitia kwa michango ya Harambee kwa miradi ya maendeleo ambayo mwishowe haionekani. Pesa wanazozikusanya wanazitumia kujilimbikizia mali na kujinunulia magari. Kwa maneno ya Bimose:-

... Michango ya shule haiishi kila kuchapo, na shule zinazofanyiwa michango hiyo hazionekani kamwe kuendelea kwa upande wa majengo, licha ya maktaba bora ... (uk. 1).

...

... Utamuona mtoto juzi ameanza kazi na baada ya siku tatu nne hivi wasikia amepandishwa cheo na amejinunulia gari ndogo lake binafsi. Ukiuliza wasimuliwa huyo ni kansela au kamishena ( uk. 8).

Maneno ya Bimose ni kielelezo cha jinsi viongozi waliochaguliwa wanavyowafyonza wananchi bila huruma. Haya ni maudhui ambayo yameshughulikiwa na waandishi wengine wa Kiswahili kama vile Mulwa na Yahya (1984) katika Ukame na Chacha (1987) katika Wingu Jeusi. Toto, kama Mambo wa ukame na Magebo wa Wingu Jeusi ndio wanaowakilisha uozo huu miongoni mwa viongozi. Wanapopata ofisi huwa ni muhali kuwaona.

Ili kuchaguliwa bungeni, Toto anawahonga wananchi kwa pesa na bidhaa. Hata hivyo, anapochaguliwa anaenda kuishi mjini na kuwasahau sio tu wale waliomchagua bali pia familia yake. Juu ya hayo, anawaagiza "wanayusi" wake kuitisha michango ya Harambee ambayo ni ya lazima. Wale wanaokataa kuchanga wanapokonywa mali yao ikanadiwe. Kupitia kwa njama hizi, Toto amekuwa mjumbe kwa miaka ishirini na tano. Hata hivyo, wananchi wamechoka. Hawadanganywi tena. Mchezo unaanza kwa malalamiko ya wananchi kuhusu michango ya Harambee. Kwa kukinai udanganyifu wa namna hii, wameamua kumuunga mkono maskini mwenzao Bw. Faida Mbaruku ambaye ijapokuwa ni 'maskini ana utu'. Wafuasi wake hawaujali umaskini wake tofauti na wafuasi wa Toto ambao lengo lao kuu ni kuchuma kutoka kwake.

Toto, mbali na kuwasaliti wananchi, ameitupa familia yake mkono. Watoto wake wanavalia matambara, wanafukuzwa shuleni kwa kukosa karo, nyumbani ha jawajengea na chakula hajui wapatako. Mkewe amekopa mpaka hakopeshwi tena. Licha ya haya yote, Toto

pesa zake anazitumia kwa kuwahonga watu ili wampigie kura. Vile vile, anaendelea kuishi na vimada huko mjini. Mkewe, Fani, anapowasili nyumbani kwake usiku bila kutarajiwa, Toto anashtuka. Anajua waziwazi kuwa mkewe hamuungi mkono wakati huu. Majira yaliyopita alimuunga mkono lakini yeye na watoto wake waliambulia patupu.

Toto na Faida wanatofautiana katika mbinu zao za kuomba kura. Faida anafanya siasa ya kutoka nyumba moja hadi nyingine ilhali Toto anawahonga watu kwa bidhaa na pesa. Hatimaye Faida ndiye anayepata ushindi. Hili linamfanya Toto kurukwa na akili. Ingawa pesa zake zote amezitumia, haziku-msaidia chochote.

## 2:2:2 TASWIRA YA MWANAMKE

Ili kuiainisha taswira ya mwanamke katika tamthilia hii, tutawagawanya wanawake walioko katika makundi mawili. Kwanza, tutawatizama wanawake kama wafuasi wa wanasiasa na pili tutawatazama kama wake wa viongozi.

Idadi kubwa ya wanawake tunaokutana nao katika tamthilia hii ni wafuasi wa wanasiasa. Wengi wao ni wanawake wa tabaka la chini. Hawa ni wanawake ambao kijuujuu wanaonekana kuzielewa hila za mjumbe wao Toto. Wametambua kuwa Toto amekuwa akiwahadada na kuchuma kutoka kwao. Kwa mfano amekuwa akiitisha mikutano ya Harambee lakini pesa zikusanywazo haziwafaidi chochote. Kwa mfano tunaona kuwa barabara hazitengenezwi. Kwa hivyo, wanawake hawa wameungana kumwangusha mjumbe wao wa sasa na kumjaribu mwingine. Kwa maneno ya Bimose:-

Ndiyo sababu tumekutana hapa leo. Kipya Kinyemi, walisema Waswahili. Lakini ni bora hicho kuliko hao watuonao vipofu na viziwi taabani ... (kur. 9-10).

Wanawake hawa wanajichukulia wenyewe kuwa 'wakurugenzi' wakuu na shughuli za kinyumbani. Kwa hivyo, mambo ya kampeni za uchaguzi yanachukua nafasi ya pili. Bimisi anapendekeza wachukue juma moja kujitayarisha ili waache shughuli hizi katika hali njema. Katika muktadha wa kisiasa, hawa ni wanawake ambao hatuwezi kusema wana 'mwamko mpya wa kisiasa' kama inavyodaiwa katika jalada. Wanawake hawa hawaonekani kuelewa siasa na mfumo unaozingatiwa katika nchi yao na ambao umewazaa viongozi kama Toto. Hawa ni wanawake ambao wanamfuata mwana-siasa kijingajinga kwa kuwa ni 'maskini' mwenzao. Hawajamkinika kiasi cha kuweza kuelewa kuwa viongozi kama Toto ni zao la mfumo wa kibwanyenye ambao hauwezi kuondolewa kupitia kwa kura.

Zamkono, kama mfuasi wa mmoja wa wanasiasa, amesawiriwa kama kimada ambaye yu tayari kumfuata ye yote mradi tu awe na pesa. Anahusiana kimapenzi na wanaume wawili wakati mmoja ili aweze kufaidi kwa sababu 'hajasoma'. Katika mkutadha huu, amesanifiwa kama mwanamke mlaghai na malaya ambaye hawezi kushiriki katika mapenzi ya dhati na mwanaume.

Mwanamke kama mke wa kiongozi ni mwanamke ambaye anadhakilishwa. Bi. Faida kwa mfano amefanya mengi ili kuwaunganisha watu pamoja ili wamuunge mkono mumewe katika kampeni. Hata hivyo, mumewe anamchukulia kuwa mtu duni asiyepaswa kufahamu baadhi ya mambo anayoyajadili na wafuasi wake. Katika mkutano unaofanyika

nyumbani kwa Bw. Faida, tunashuhudia Faida mwenyewe akimwambia mkewe:-

Baba, nawe mke wangu, tupatieni nafasi ya faragha (uk. 21).

Hapa, tunalazimika kujiuliza ni kwa nini baada ya juhudi zote alizofanya na anazoendelea kufanya ili kufanikisha kampeni ya mumewe hawezi kuketi katika kikao cha wanaume hawa na kutoa mchango wake wa maoni. Hata hivyo, Bekone, babake Faida, ndiye anayetupatia jawabu:-

...Jamani siku zimebadilika wala hazingoji mtu. Yalionekana wapi mambo kama haya enzi zetu? Vijana sasa ndio wanaofanya mashauri, nasi wazee tunanyamazishwa kama wanawake ... ( uk. 21).

Maneno haya ya mzee Bekone yanatuelekeza kwenye taasubi za kiume ambazo zimesakini katika jamii anayoishughulikia mwandishi ambapo mwanamke hana usemi dhidi ya mwanaume na wala haruhusiwi kushiriki katika vikao vya wanaume ambapo mambo muhimu yanajadiliwa na kupitishwa.

Pengine Fani, mkewe Toto, ndiye kielelezo kizuri zaidi cha jinsi ambavyo mwanamke kama mke wa kiongozi anavyodhalilishwa. Kwanza, maoni yake hayathaminiwi. Yeye mwenyewe anaishi mashambani na anajua kuwa watu huko hawamthamini Toto tena. Kwa hivyo, yeye amemshauri mumewe asigombee kiti cha ubunge tena. Hata hivyo, maoni yake hayakutiliwa maanani:-

FANI: Ulisemalo ni fumbo. Maoni yangu nilikupatia tangu awali ulipotaja neno kampeni. Hisia zangu katu huzithamini na leo waniuliza swali hilo hilo, nijibu nini kipya? (uk. 42).

Katika uhusiano wake na mkewe, Toto ana ubwana.

Anamtarajia mkewe asikize yote ayasemayo bila ukinzani:-

TOTO: Fani tunza. Kuropoka hakufai.  
Ningekuomba unielewe na ujaribu kusaidia.  
Ndoa yetu inahalisi uyasikize nisemayo  
na kama msaidizi wangu, unatarajiwa  
ufuate maagizo na kufanya uambiwavyo.

...

Mwanamke we! Heshima kitu cha bure  
Usijaribu kuchokoza nyuki. Unaonekana  
umezisahau njia za kuongea na wakubwa  
wako. Laiti wangekufunza adabu njema!  
Elewa mimi ndiye bwana na wewe daima  
utakuwa wa kufuata maagizo unayopewa  
( uk. 45 ).

Fani anatarajiwa kuwa mtiifu na mnyenyekevu eti kwa sababu ameolewa; awe mtiifu na mnyenyekevu ijapokuwa watoto wake pamoja naye wanakufa njaa. Hii ni taasubi ya kiume ambayo inaendelezwa na jamii ambapo mwanamke hana usemi dhidi ya mumewe. Anatarajiwa akubaliane na yale yote asemayo mumewe kwa sababu yeye ni 'msaidizi' wa mumewe. Dondoo hili pia linatuonyesha dhiki anazokumbana nazo mwanamke anapoolewa na kupata watoto kisha baadaye anaachiwa wale watoto na mumewe ambaye anatorokea mjini ambako anajifurahisha na wanawake wengine.

Kwa jumla, katika tamthilia hii, wanawake wamesawiriwa kama viumbe duni ambao wanatumiwa na wanaume kuendeleza maslahi yao; viumbe dhaifu ambao hawana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao wanatarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa waume wao bila ukinzani.

2:2:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Ryanga ni mmoja wa waandishi wa kike ambao hawaonyeshi kuwaunga mkono wanawake wenzao katika harakati zao za kujikomboa kutokana na mfumo wa itikadi za kijamii na kisiasa ambazo zinawauusia wanawake kuwa wananchi wa tabaka la chini daima dawamu. Katika tamthilia hii, Ryanga anaendeleza itikadi kuwa jukumu kubwa la mwanamke ni lile la kuwa msaidizi wa nyumbani. Kwa maoni yake, jukumu la wanawake katika siasa ni kuwa wafuasi wa wanaume. Ryanga haoni uwezekano wowote wa mwanamke kugombea uchaguzi na kuwa kiongozi. Jukumu awezalo kutekeleza ni lile la kumhimili mwanaume. Swali tunalolazimika kujiuliza ni kwa nini kwa Ryanga, ambaye ni mwanamke, haiyumkiniki kwake kuwa mwanamke anaweza kuwa kiongozi. Swali hili linaweza kujibiwa kwa kurejelea hali ilivyo nchini Kenya na ulimwenguni kwa jumla.

Hapa nchini Kenya, nyadhifa nyingi za uongozi zimeshikiliwa na wanaume. Kwa mfano, katika baraza la mawaziri ambalo kwa kawaida huwa na zaidi ya mawaziri 30, hakuna mwanamke hata mmoja. Pia, katika bunge lenye wabunge zaidi ya 180 waliochaguliwa, idadi ya wanawake haizidi wawili. Hali hii inasababishwa na ukweli kwamba wanawake wengi, hasa wale walioolewa hunyimwa nafasi ya kushiriki katika siasa. Mmoja wa wabunge wanawake Bi. Agnes Ndetei, kwa mfano, alipinga vikali kura ya mlolongo huku akisema kuwa baadhi ya wanawake waliopiga mstari nyuma yake wakati wa uchaguzi walipigwa na kuumizwa vibaya na waume wao.

Pengine hali kama hii inayosababishwa na taasubi za kiume pamoja na utamaduni unaowafunga wanawake nyumbani kuwatunza watoto na waume wao ndio inayowasababisha waandishi kama Ryanga kutoona kuwa kuna uwezekano wa wanawake kutekeleza majukumu mengine nje ya yale waliyotengewa na jamii. Hata hivyo, jukumu la mwandishi sio tu kutusanifia hali halisi. Mwandishi ambaye ni mtetezi wa maslahi ya wale wanaonyimwa haki zao anawajibika kuwa mwalimu kwao; kuwaonyesha jinsi ambavyo wanaweza kuibadilisha hali hii ili waweze kupata afueni. Vasquez (1973:41) anatueleza:-

Sanaa inaweza kuwa na jukumu tambuzi, lile la kuonyesha kinachohimili hali halisi; lakini jukumu hili linaweza kutekelezwa tu kwa kuisanifu hali halisi mpya...

Anachomaanisha Vasquez hapa ni kwamba mwandishi wa kisanaa ni lazima aisanifu hali halisi na wahusika wake kwa lengo la kuonyesha jinsi ambavyo wanaweza kuibadilisha hali yao. Hata kama mwandishi ni mwanachama wa kundi linalonyimwa haki, inawezekana kwake kuubadilisha mwelekeo wake kujihusu, kuhusu binadamu wengine na ulimwengu kwa jumla. Ryanga haonekani kuwa na uwezo wa kufanya hivi. Mwandishi huyu hajamuumba mhusika wa kike hata mmoja ambaye anaweza kusimama na kumpinga mwanaume katika siasa. Zaidi ya hayo, wahusika wake wa kike ni watu ambao hawafanyi kazi wala hawajaelimika. Kwa hivyo, wanawategemea wanaume kwa mahitaji yao ya kila siku. Ulimwengu wao ni ulimwengu wa nyumbani; na kwa maoni ya Ryanga hapa ndipo wanapaswa kubakia daima dawamu. Ndiposa hajamtoa mhusika hata mmoja katika mazingira haya finyu angalau awe

kielelezo kwa wanawake wenzake. Majukumu makuu anayowapa wanawake ni yale ya mama, bibi na chombo cha kumfurahisha mwanaume.

Mfano wa mwanamke aliyepewa jukumu hili la mwisho ni Zamkono. Yeye, kama jina lake linavyoelekea kumaanisha, lazima atiwe pesa mkononi ili anayemtaka apate huduma zake. Kwa kuwasawiri wahusika wake namna hii, Ryanga anaendeleza na kutilia nguvu imani kwamba ulimwengu wa siasa ni ulimwengu wa wanaume ilhali hatima ya mwanamke ni kuzaa na kulea watoto, kuwakimu wanaume kwa mahitaji yao ya kiroho na kimwili kwa kuwa watiifu na wanyenyekevu na kuwahimili daima; huduma za namna hii zinapohitajika. Hivi ni sawa na kusema kuwa jukumu kuu la mwanamke liko jikoni na kitandani. Ndiposa tunawaona wanawake katika tamthilia hii wakijiita wakurugenzi wa mambo ya kinyumbani. Kwa kuiendeleza falsafa ya namna hii, Ryanga anashindwa kutambua kuwa wanawake ni watu walio na maslahi yao katika jamii. Usawiri wa namna hii ni wa kushangaza kwa sababu Ryanga ni mwandishi wa kike.

Je, ni kweli kuwa wanawake ni wakurugenzi wa mambo ya kinyumbani tu? Swali hili linaweza kujibiwa kwa kuiangalia picha ya mwanamke katika tamthilia ya A. Mazrui Kilio cha Haki na Tone la Mwisho ya E. Mbogo. Mbogo, kwa mfano, anatusawiria mhusika wa kike Tsitsi ambaye ni mmoja wa viongozi wa jeshi la msituni linalopigania uhuru. Picha kama hii tunaipata pia katika tamthilia ya Ngugi wa Thiong'o na Micere Githae Mugo (1976) iitwayo Mzalendo Kimathi. Katika tamthilia hii, wanatuchorea picha ya mwanamke akishiriki kikamilifu katika vita ya

uhuru nchini Kenya. Mazrui kwa upande wake anatusawiria mhusika wa kike ambaye ni kiongozi wa wafanya kazi katika shamba la Bw. Delamon. Mhusika huyu, Lanina, anatetea haki za wafanya kazi wenzake na kupambana na taasubi za kiume. Tuna-chojaribu kudhihirisha hapa ni kwamba dhana kwamba wanawake wanaridhika kuwa 'wakurugenzi' wa mambo ya kinyumbani ni dhana iliyopotoka.

Maoni yetu ni kwamba Ryanga anatuchorea picha ya kijadi ya mwanamke ambapo mwanamke huonekana kama kiumbe dhahili aliye chini ya mwanaume na ambaye hana budi kumtumikia mumewe na kumfuata kwa lolote lile asemalo. Ni kutokana na haya ambapo tunamwona Toto akigombana na mkewe anapokataa kumwunga mkono katika kampeni. Mwanamke katika falsafa ya jamii kongwe anahitajika kumnyenyekea na kumtii mumewe. Taiwo (1984:3) anaeleza kuwa utiifu wa namna hii ni kipengele muhimu cha maisha ya kijadi. Ryanga anaelekea kukubaliana na falsafa hii.

Katika tamthilia hii, Ryanga anaashiria mabadiliko ya kijamii bila kuonyesha kiyakinifu jinsi ambavyo jambo hilo linawezekana na nafasi ambayo mwanamke ataichukua katika jamii hiyo mpya. Mtazamo wake ni mtazamo wa kibwanyenye ambao unatokana na kutokuwa na itikadi maalumu ambayo inamwongoza katika uandishi wake. Aidha mtazamo wake unabobea katika itikadi ya kibwanyenye inayoendelezwa na jamii yake. Kuhubiri kuangushwa kwa viongozi ni sawa na kuiga falsafa ya viongozi wa kibepari kikasuku. Kwa kufanya hivi, Ryanga anashindwa kwa kiasi kikubwa kudhihirisha umahiri wake kama mwandishi katika kubuni kazi ya sanaa yenye mawazo mapevu na yake mwenyewe. Anachoweza kufanya tu ni kuimba itikadi zinazoimbwa na viongozi wa kibwanyenye kila siku.

Swala ambalo anajihusisha nalo ni swala ambalo ameliopoa katika msingi yake halisi. Na wala haliweki swala hili katika misingi yake ya kisiasa na kiuchumi. Zaidi ya hayo, jinsi anavyolijadili swala hili la mwanamke linajitokeza kuwa kama tiyara inayopwelea hewani. Mwishowe tunalazimika (kwa masikitiko makuu) kuiweka kazi hii katika kijopo cha kazi za 'sanaa kwa ajili ya sanaa'.

Kwa msingi wa nadharia yetu, mbali na kuonyesha jinsi hali ya unyonge ya mwanamke inavyotokana na mfumo wa kiuchumi na mfumo wa kuumeni, mwandishi hana budi kuitumia sanaa kuiwakilisha hali ya mwanamke kikamilifu kwa kueleza tajriba yake kwa uaminifu, kumsawiri mwanamke kwa njia ambayo inaonyesha analenga usawa wa kitamaduni na pia kuwachora wahusika wa kike ambao wanaweza kuigwa na wanawake wenzao. Zaidi ya hayo, mwandishi anapaswa kutumia sanaa kuwazindua wanawake kama watu wanaonyanyaswa katika jamii ili waweze kusaidia kuleta mapinduzi yatakayoondosha unyanyasaji huu. Ryanga katika tamthilia hii hajafaulu kufanya hata moja ya mambo haya. Swala la uhuru wa mwanamke halionekani kuwa muhimu katika tamthilia hii. Mwanamke kwa Ryanga ni 'kiungo' cha kutia ladha ulimwengu wa wanaume.

### 2:3 K I M A L I Z I O

Katika sura hii, tumewachambua waandishi wawili wa Kenya. Tumeona kwamba katika tamthilia zote mbili tulizozi-shughulikia, taswira zinazojitokeza ni zile za mwanamke kama

mke, mzazi, mtumwa, pambo na chombo cha kutimizia ashiki za kiume katika Mama Ee. Mwanamke kama mfuasi wa mwanasiasa na mke wa kiongozi katika Zinduko anajitokeza kama mlaghai na mwanachini kwa mwanaume. Tumeona kuwa katika majukumu haya yote, mwanamke anadhalilishwa. Pia, tumetumia taswira hizi kuchambua mtazamo wa kila mmoja wa waandishi hawa kuhusu swala la mwanamke. Tumeona kuwa waandishi hawa wanatofautiana kwa jinsi ambavyo wanaliona jukumu la mwanamke katika jamii. Tumeona kuwa Mwachofi katika Mama Ee anapinga vikali mifumo na itikadi ambazo zinamnyima mwanamke uhuru wake na kumweka katika nafasi ya pili nyuma ya mwanaume. Hata hivyo, tumeona kuwa kuna wakati mwingine ambapo mwandishi huyu anayumbayumba katika msimamo kuhusu swala hili. Kwa mfano, tumeona kuwa hana msimamo maalumu kuhusu mahari.

Kwa upande mwingine, tumeona kuwa Ryanga anajifunga na mtazamo wa kijadi kuhusu jukumu la mwanamke katika jamii. Tumeona kuwa anaonelea kuwa mwanamke hana nafasi ya kushiriki katika siasa kama kiongozi. Jukumu lake kuu ni kuwahimili wanaume. Pale ambapo mhusika mkuu katika Mama Ee anazivunja pingu zinazomfunga na kuyaunda maisha yake upya, mhusika wa kike Fani katika Zinduko anabaki kuililia hali yake tu.

Ufanisi wa Mwachofi haupo katika suluhisho analotoa katika tamthilia hii bali katika msukumo na ari anayoonyesha katika kushughulikia swala ambalo wengi huhiari kulikwepa. 'Mama Ee' si kilio cha kukata tamaa, bali ni kilio cha matumaini. Mwachofi ni mwandishi ambaye ameishi katika jamii ambayo mwanamke anachukuliwa kuwa mwananchi wa tabaka la chini; jamii

ambayo haimpi nafasi ya kujiendeleza na kufikia upeo wa maisha yake kama binadamu. Hali hii haiwezi kuendelea zaidi. Ndiposa kisanaa anaivunja kwa njia ambayo anaonelea kuwa mwafaka zaidi.

Ryanga kwa upande ule mwingine ni mwandishi ambaye haonekani kupevuka wala kumakinika kimawazo na kimtazamo. Ijapokuwa jamii alimokulia na kuishi ni jamii iliyojaa dhuluma dhidi ya wanawake, haonekani kuzipa nafasi yoyote dhuluma hizi katika kazi yake. Anapotusanifia dhuluma hizi, anaishilia kutuonyesha unyonge wa mwanamke katika kukabiliana na dhuluma hizi. Katika hali hii, anachoweza kufanya mwanamke ni kuililia hali yake tu. Hawezi kupita kiwango hicho na kutenda ili kuibadilisha hali yake. Kwa Ryanga, mabadiliko ambayo yanaweza kumletea mwanamke afueni ni jambo lisiloyumkinika. Mwishowe, Ryanga hajafanikiwa hata kidogo kutuwasilishia swala ambalo analishughulikia kwa njia ambayo ni yakinifu. Mchezo huu kwa maoni yetu unaelekea kuwa 'sanaa kwa ajili ya sanaa.'

3:0 SURA YA TATU

WAANDISHI WA KIKE WA TANZANIA: CHOGO NA MUHANDO WA AWALI  
1972 - 1976.

3:1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutawachambua waandishi wawili. Waandishi hawa ni Angelina Chogo Wapakhabulo na Penina Muhando. Tamthilia ya Chogo tutakayoichambua ni Kortini Mtu Huyu (1976) ilhali tamthilia za Muhando tutakazozishughulikia ni Hatia (1972) na Pambo (1975). Katika kuwachambua waandishi hawa, tutazingatia matukio na mabadiliko ya kihistoria, kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyokuwa yanatendeka nchini Tanzania wakati waandishi hawa walipokuwa wanaandika. Lengo letu litakuwa ni kuonyesha jinsi ambavyo waandishi hawa waliyachukulia matukio haya na jinsi walivyoiona nafasi ya mwanamke katika jamii mpya iliyokusudiwa kujengwa kupitia Azimio la Arusha la 1967.

3:2 WAANDISHI

Penina Muhando (ambaye sasa anajulikana kama Penina Mulama) ni mmojawapo wa waandishi mashuhuri sana sio tu nchini Tanzania bali pia katika Afrika mashariki na kwingineko ambako lugha ya Kiswahili inazungumzwa. Mwandishi huyu alizaliwa mnamo mwaka wa 1948 wakati ambapo utawala wa kikoloni ulikuwa umeshika kani. Alikulia na kusomea huko Kilosa. Baadaye alisomea Dodoma na Chuo cha Dar es Salaam ambako sasa anafunza kama Profesa katika Idara ya Sanaa za maonyesho ya chuo hicho. Penina sasa ndiye Chief Academic Officer wa chuo kikuu hicho. Nguzo mama hoyee! Kufikia hivi sasa, Muhando ameandika michezo

ya kuigiza tisa tuijuayo; mbili yake akiwa ameshirikiana na watu wengine. Wakati alipoandika mchezo wake wa kwanza kwa jina la Hatia, Tanzania ilikuwa imejitawala kama nchi huru kwa miaka kumi. Katika kipindi hiki, Muhando alishuhudia matukio muhimu katika nchi yake ambayo yameathiri maandishi yake. Alishuhudia mabadiliko yaliyofanywa na serikali ya Tanzania huru, mabadiliko ya kiitikadi na maisha kwa jumla hasa baada ya Azimio la Arusha la 1967. Kulingana na M.L. Balisidya (Matteru)(1987:34), Muhando, kama wanafunzi wengine na baadaye waalimu wa wakati huo waliisoma, kuitalii, kuifanyia utafiti na kuikubali itikadi mpya iliyoanzishwa kupitia Azimio la Arusha.

Penina Muhando anaamini kuwa sanaa za maonyesho ni chombo muhimu cha mawasiliano na elimu. Harakati na juhudi zake katika tamthilia na sanaa nyinginezo za maonyesho zimekusudiwa kuonyesha kuwa sanaa hizi zinaweza kutumiwa kama jukwaa la kujitambulisha, kuelezea, kujadilia na kupendekeza masuluhisho kwa matatizo yanayoikumba jamii. Kwa hivyo, tamthilia zake zinachota maudhui yake kutokana na hali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ya nchi yake (tazama Matteru 1987:34). Alipohojiwa na Lee Nichols, ripota wa 'voice of America,' Mwandiishi huyu alikuwa na haya ya kusema:

Nafikiri ninapoandika huwa ninachukua tatizo lolote ambalo linawakumba watu wa Tanzania kwa wakati wa sasa. Kwa sababu ninajiona kama niliye na wajibu wa kujaribu kusaidia jamii ama kwa kuonyesha pale ambapo matatizo yapo au kuwafanya waelewe kuwa chanzo cha tatizo hili au lile kiko hapa au pale ...

...

Naamini kwa dhambi kuwa hapa Tanzania

hatuna nafasi ya sanaa kwa ajili ya sanaa kwa sasa. Kwa sababu tuna matatizo chungu nzima kama nchi inayoendelea na hakuna nafasi ya sanaa kwa ajili ya sanaa kwa sababu msanii ana jukumu kubwa sana katika kusaidia maendeleo ( ya taifa ). (Nichols 1981:140).

Bi. Angelina Chogo Wapakhabulo kwa upande wake amepewa sifa ya kuwa 'mwandishi mashuhuri wa michezo ya kuigiza.' Chogo pia alisomea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kujipatia shahada ya B.A. Kama Muhando, Chogo pia amekuwa mwalimu katika shule mbalimbali nchini Tanzania. Falsafa yake ameleza katika utangulizi aliyoundika mwenyewe katika mchezo wake:

Mambo yaliyo kwenye mchezo huu yanahusiana na jamii yoyote ambayo ina hali au mambo kadhaa isiyopendelea. Mara nyingi katika kutatua matatizo kama haya, wale wanaohusika huangalia tu matawi bila kuchimbua mizizi ili haki iweze kutawala ... kuunda hali fulani isiyopendelea au hata uovu kwenye jamii, kwa mfano umalaya, uvaaji wa mavazi yasiyotakiwa, nywele za bandia, na kadhalika huwezi ukakuta kuwa ni mtu mmoja binafsi anayehusika na ambaye twaweza kumfuata kwa kiboko tukamchapa kwa urahisi ... kama ingekuwa yawezekana kuwapata wote wanaohusika na ili haki itawale, si ajabu na mimi mwenyewe mwandishi ningechapwa viboko.

Chogo anaamini kuwa kila mwanajamii anachangia kwa njia moja au nyingine katika kuendeleza uozo wa kijamii na ili kuyatatua matatizo yanayoikabili jamii, lazima kiini cha yale matatizo kichimbwe ili masuluhisho halisi yaweze kupatikana.

Kwa jumla, waandishi hawa wawili ni waandishi ambao wamepata elimu ya kimagharibi na wanaandika katika mazingira sawa ya kihistoria, kiuchumi, kijamii na kisiasa.

### 3:3 MAZINGIRA YA WAANDISHI

Tamthilia tunazozichambua katika sura hii zimeandikwa katikati ya 1972 na 1976. Hiki ni kipindi muhimu katika historia ya Tanzania. Kulingana na Boesen (1977:11), kipindi cha miaka mitano kati ya 1968 na 1973 kinawakilisha hatua ya kwanza ya sera ya 'ujamaa vijijini' ambapo swala la kuwashawishi watu wajiunge na vijiji vya ujamaa katika sehemu za mshambani lilitiliwa mkazo na serikali ya Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Tanzania wa wakati huo. Hatua hii ilifuatia Azimio la Arusha la 1967 ambapo serikali ya Tanzania ilianzisha siasa ya Mrengo wa Ujamaa. Matukio haya yalikuwa na athari kubwa kwa maisha ya watanzania ( Zaja Omboga 1986:85). Hili linawaweka Chogo na Muhando katika kipindi maalumu cha historia ya nchi yao.

Azimio la Arusha lililenga kujenga jamii yenye usawa wa binadamu wote kupitia vijiji hivi vya ujamaa ambako ilitarajiwa kwamba unyanyasaji, ukandamizaji na uamaji jasho wa binadamu dhidi ya mwengine ungeondolewa. Pia, ilitumainiwa kwamba kila mmoja wa wale walioishi katika vijiji hivi ange-tambua haki ya mwenzake kupata fungu analostahiki la mali ya jamii na pamoja na hayo kutambua umuhimu wa kufanya kazi pamoja ili kuzalisha mali. Kwa jumla, Azimio hili liliendeleza siasa ya ujamaa na mwito wa kujitegemea kwa kuupiga vita unyonyaji na kuleta usawa wa kiuchumi na kijamii baina ya watu wote (Nyerere 1968).

Jambo lingine la muhimu kutaja ni kwamba waandishi hawa wanaandika takribani zaidi ya miaka kumi baada ya uhuru

kutoka kwa wakoloni. Ukoloni mkongwe ulikuwa na athari kubwa katika nyanja zote za maisha ya waafrika na hasa maisha ya wanawake. Kulingana na Wanjiku Matenjwa (1984) na Micere Githae Mugo (1984), utamaduni mkongwe wa kiafrika ulikuwa unamnyanyasa na kumkandamiza mwanamke. Majilio ya ukoloni yalizidisha unyanyasaji na ukandamizaji huu maradufu kwa kuiweka mali yote mikononi mwa wanaume. Ijapokuwa wanawake ndio waliofanya kazi nyingi katika mashamba na kazi za kinyumbani, mapato yalimwendea mwanamke. Kwa maoni ya Micere Mugo, athari kubwa zaidi ya ukoloni ni kumfanya mwanamke kuikubali hali hii.

3:4 ANGELINA CHOGO (1976): KORTINI MTU HUYU.

3:4:1 HADITHI KWA UFUPI

Kortini Mtu Huyu ni tamthilia ambayo imeumbwa katika mazingira ya kimji. Mchezo unapoanza, tunakutana na Bwana na Bi. Shiba ambao ni matajiri wanaoishi maisha ya raha mustarehe mjini. Kwa jinsi ambavyo nyumba yao imepambwa na kutokana staftahi wanayokula, watu hawa ni watu waliostarehe sana. Papo hapo wakiendelea kustaftahi, anafika msichana kutoka mashambani aitwaye Hadija ambaye amekuja mjini kutafuta kazi ili kuziepuka fujo za babake. Bi. Shiba anampa kazi lakini anakataa kumpa mshahara uliowekwa na serikali wa shilingi mia tatu na arobaini. Bi. Shiba yu radhi kumpa tu chakula. Mwishowe, anakubali kumlipa shilingi arobaini kwa mwezi. Anamwambia:

Sasa nini basi? Unachotaka ni kazi,  
kazi ipo hata sasa hivi unaweza kuanza.  
Unachohitaji si chakula tu? (uk. 5).

Haya ni juu ya ukweli kwamba Hadija anatarajiwa kufanya kazi kama punda wa dobi. Kazi anazohitajika kufanya kila siku ni kuosha vyombo na kuvikausha, kufua nguo, kupiga pasi, kupanga viti, kutandika vitanda, kupiga deki na kupika chakula. Kazi hizi zote lazima azimalize kabla ya saa nane na nusu. Robo tatu ya mshahara anaoupata yambidi ampelekee babake nyumbani.

Baada ya kufanya kazi kwa miezi mitatu, Hadija anamwibia nguo mwajiri wake na kutoroka. Baadaye anaajiriwa katika 'Bar' kama mwuzaji pombe. Hapa, anaingilia maisha ya umalaya. Bi. Shiba anapogundua ameibiwa, anataka kumripoti Hadija kwa polisi lakini mumewe anamkanya dhidi ya kufanya hivyo kwani Hadija anaweza kuwashtaki kuwa wamekuwa wakimpa mshahara duni ambao ni chini ya kiwango kilichowekwa na serikali.

Bi. Shiba anamchukua mtoto wa kakake kuja kumfanyia kazi. Huyu ni msichana ambaye kama Cheja wa Hatia hajawahi kufika mjini. Siku moja, Mwaire ambaye ni mgeni mjini, anamwona msichana akiwa ameivalia vizuri sana wakati akiwa anafanya kazi zake za kawaida. Mwaire hapewi mshahara wowote na mwajiri wake. Badala yake, anapewa ahadi, kila mwisho wa mwezi kuwa atanunuliwa nguo na kulipwa mwezi ufuatao. Anachoambulia katika kazi hii yake ni nguo kuu kuu za mwajiri wake ambazo zimechanikachanika. Siku nyingine akiwa anafanya kazi zake za kawaida anaingia kijana mmoja aitwaye Msafiri pale nyumbani kwa Bi. Shiba. Kijana huyu anajidai kumpenda Mwaire. Mwaire, ambaye ni limbukeni katika maisha anazikubali hadaa za Msafiri. Hatimaye anatoroka na kuolewa naye. Miaka mitatu ya kwanza ya ndoa baina yao inakuwa ya furaha kwa Mwaire. Katika kipindi

hiki cha miaka mitatu, anazaa watoto watatu. Hata hivyo, mumewe anapata kazi na kutoroka kutoka nyumbani. Maisha ya Mwaire yanatumbukia nyongo. Anajaribu kufanya biashara ndogo ndogo ili kuyaendesha maisha yake na wanawe bila mafanikio. Wakati huo, mumewe msafiri anajistarehesha na wanawake malaya kama vile Heri na Sikujua.

Kwa kuzidiwa na mambo, Mwaire anaingizwa katika maisha ya ulevi na umalaya na jirani yake Shida. Ni katika hekaheka hizi ambapo anakutana na mumewe ambaye wakati huo wote amekuwa akifikiria yuko safarini.

Siku moja wanaingia 'Bar' kama kawaida na kuanza kunywa na Adamu na Kuwili. Kuwili ni mwanakamati wa Kamati ya Usahihishaji wa Wanajamii. Wanafumaniwa na polisi na kutiwa mbaroni. Wanapofikishwa mbele ya kamati, Mwaire anaachiliwa huru na kupewa nusu ya mshahara wa mumewe kila mwezi. Heri na Sikujua wanarudishwa vijijini ambako wataenda kufanya kazi za kuwafaidi ilhali Kuwili anaamriwa kufikishwa mbele ya mahakama ili kujibu mashtaka chini ya sheria ambayo yeye mwenyewe amesaidia kuitunga.

### 3:4:2 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Taswira kuu ya mwanamke inayojitokeza katika tamthilia hii ni ile ya mwanamke kama mdhalimu. Taswira hii inaenda sambamba na ile ya mwanamke kama mdhulumiwa. Bi. Shiba amesawiriwa kama mdhalimu, mkandamizaji na mnyonyaji wa nguvu za wanawake wenzake. Huyu ni mwanamke ambaye hayajali maslahi ya wanawake wengine. Badala yake, anadiriki tu kuwaama jasho. Kwa mfano Hadija anapoenda kuomba kazi nyumbani kwake, anagoma

kumpa mshahara uliopendekezwa na serikali. Maneno anayomwambia

Hadija yamejaa ujeuri:

Anatania tu. Watu wanatembea usiku  
na mchana kutafuta kazi hata mradi  
tu wale nao hawapati, halafu wewe  
ndiyo unatuletea bei zako hapa. Aende  
kwani nani ana shida, yeye au mimi?  
Wataka kazi wengi dada. Ukitaka  
mshahara huo safiri salama.  
(kur. 2 - 3).

Haya ni maneno ambayo Bi. Shiba anayasema kwa sababu

Hadija amejileta nyumbani kwake; na zaidi ya hayo anaona kuwa

hali yake ni duni na anaweza kuchukua chochote apewacho.

Madai ya Bi. Shiba kuwa hana shida ni kinaya kwani muda mfupi

tu uliopita, tunamwona akimnung'unikia mumewe Bwana Shiba

ifuatavyo:-

Hee, unadhani una mtumishi hapa!  
Ha, mie nimechoka. Kazi tufanye wote  
huko maafisi, nyumbani wote tunarudi  
saa hiyo hiyo moja, na wewe ukisha  
rudi mguu juu unangojea nipike ule.  
Kwani unadhani mie mashine sichoki?

...

Lazima nipate mtumishi ( uk. 1).

Ukweli ni kwamba anahitaji mfanya-kazi lakini ili

apate nafasi ya kumpunja Hadija, anajidai kutokuwa na haja ya

mfanya-kazi. Pengine udhalimu na unyonyaji wake unajitokeza

zaidi pale ambapo anaamua kumlipa Hadija shilingi arobaini

badala ya mia tatu na arobaini kwa mwezi huku akimwambia kuwa

chakula tu kinamtosha. Na hata hicho chakula kukipata ni

makeke kama anavyotwambia Hadija:-

... Hebu nipumzike kidogo.  
Maisha kweli magumu. Mwezi  
wa tatu huu nafanya kazi lakini  
nilichoambulia ni shilingi 40  
tu kila mwezi ambazo kabla ya

kuzipata lazima nikumbushwe kiasi  
ninachokula na raha nizipatazo  
ambazo wala sizioni ( uk. 7).

Haiyumkiniki jinsi mtu anayeishi raha mustarehe kama Bi. Shiba anavyoweza kufikiria kuwa binadamu mwenzake anaweza kuishi kwa shilingi arobaini tu kwa mwezi na huku hata mahali pa kulala hapati. Unyama wa bibi huyu umekithiri hadi kiwango cha kuwaama jasho jamaa yake. Anamchukua Mwaire, mtoto wa kakake, na kumfanyisha kazi kipunda. Hamlipi chochote wala kumnunulia nguo. Anachoambulia Mwaire ni nguo kuu kuu na chakula na ahadi za uongo kila mwisho wa mwezi. Bi. Shiba amesawiriwa kama mwanamke ambaye hana hisia za kibinadamu. Alichosheheni ni uroho, ubinafsi, hiana na kiburi.

Kama tulivyotaja hapo awali, mwanamke katika tamthilia hii pia anajitokeza kama mdhulumiwa. Palipo dhalimu lazima pawe na mdhulumiwa. -Hadija na Mwaire ni wafanya-kazi wa kinyumbani ambao wanaamwa jasho, kunyanyaswa na kudhulumiwa na mwanamke mwenzao. Wanalipwa mshahara punje ijapokuwa wanafanya kazi kama punda. Maisha ya umalaya wanayoyaingilia wahusika hawa wawili yana chanzo katika unyama wa Bi. Shiba.

Mwanamke anajitokeza kama mdhulumiwa pia katika taasisi ya ndoa. Mwanamke katika ndoa alizotusawiria Chogo anachukua nafasi ya pili baada ya mwanaume. Kwa hivyo, katika uhusiano wao, mwanaume anakuwa ndiye bwana na mkewe mtumishi. Kwa mfano ijapokuwa Bwana na Bi. Shiba wanafanya kazi, inabidi Bi. Shiba ampikie na kumwandalia mumewe baada ya kazi ijapokuwa wote wawili wamechoka. Bi. Shiba anapolalamika juu ya hali hii, mumewe anamjibu:-

Ndiyo maana mimi ni mwanaume na wewe ni mwanamke. Lazima kuwe na wa kupika na wa kupikiwa.

...  
Mtumishi au bila mtumishi, mimi sijali mradi nile, You see (kur. 1-2).

Hali hii imefika kiasi ambapo wanawake wengi wameikubali kuwa majaaliwa yao. Kwa mfano, katika utani baina ya Bwana na Bi. Shiba, inabainika kuwa mwanamke anamchukulia mwanaume kuwa mlinzi dhidi ya hatari zozote zinazoweza kutokea.

Ndoa baina ya Msafiri na Mwaire inaashiria hali ambapo mwanaume anachukuliwa kuwa mtunzi wa familia yake. Akiukwepa au kupuuza wajibu huu, familia yake inaishilia kuteseka kwa kukosa mtu wa kuwarukuzu. Mwanamke katika hali hii huwa amedhalilishwa kiasi kwamba maisha yake yanawekwa mikononi mwa mwanaume. Taswira hii inajitokeza hata kabla Mwaire hajaolewa na Msafiri. Tazama maneno ya Msafiri anapojaribu kumshawishi Mwaire amkubali:-

Kusudi nikusabahi; nikutake hali, nikutunze, nikutoe shidani, nikusaidie na kukufanyia lolote ambalo unastahili kufanyiwa ...

...  
sasa fuata shauri langu nalo ni kwamba fuatana nami ...

...  
Kwani unadhani mie sina nyumba? Toka nimekuona nimekuwa nikikufikiria na kukutayarishia makao. Hutapata taabu hata kidogo. Twende kwangu ukatulie, ukae vizuri, ule vizuri, uvae vizuri hadi nawe ufurahi (kur. 20-21).

Msafiri anajichukulia kama mwokozi wa Mwaire. Anafikiri kuwa bila msaada wake, Mwaire hawezi kuishi. La muhimu zaidi hapa ni kwamba anajichukulia kama Mungu pale ambapo anamwambia Mwaire amekuwa akimtayarishia makao. Haya yanatukumbusha

maneno ya Yesu katika Biblia alipowambia wafuasi wake kuwa anaenda kuwatayarishia makao kisha ataenda kuishi nao. Kwake, Mwaire ni kiumbe maskini ambaye lazima auniwe kama inavyodhihirika kutokana na maneno yake:-

Kwa nini nikudanganye kiumbe maskini kama wewe? Hivi bado hujaniamini? Unataka nifanye nini ili uniamini? Sema wewe mwenyewe. ( uk. 22).

Kama inavyodhihirika baadaye, hizi ni huruma za mamba anazojitia Msafiri. Msafiri anamtoroka Mwaire baada ya kuzaa naye watoto watatu katika kipindi cha miaka mitatu tu. Haya yanaonyesha kuwa lengo lake kuu lilikuwa kujifurahisha tu kwa mwili wa Mwaire na Mwaire anapozaa na kuwa 'tambara bovu' anamtoroka na kwenda kufuata wanawake wabichi kama vile Heri na Sikujua. Kwake wanawake ni vyombo tu vya kujifurahisha. Haiyumkiniki kuwa huyu ni Msafiri yule yule aliyejitia kumpenda Mwaire kiasi kwamba 'anapojisikia kuwa hawezi kukaa zaidi pasipo kuzungumza na Mwaire, hajali hata kumwagiwa maji ya moto usoni' ( uk. 19).

Taswira nyingine inayojitokeza ni ile ya mwanamke kama malaya. Wanawake wengi tunaokutana nao katika tamthilia hii ni wanawake ambao wanauza miili yao ili kupata pesa kwa sababu moja au nyingine. Hadija, baada ya kutoroka kutoka kwa Bwana Shiba anaajiriwa kama mwaia 'Bar' na anajiua ili kupata pesa. Shida pia ni malaya na ijapokuwa hatuelezwi kisa chake kwa urefu, tunadokezewa kuwa anajiua ili aweze kuukidhi utashi na nyege zake tu. Ijapokuwa tunaelezewa kuwa ana watoto,

mwandishi hatuonyeshi sababu zinazomfanya ashiriki umalaya. Pengine hata hao watoto amewapata katika pitapita za kukidhi ashiki zake. Shida ni mwanamke ambaye hana huruma kwa watoto wake. Tazama jinsi anavyomshauri Mwaire:-

Watoto hawa wakilala si unawafungia tu;  
hapo baadaye utaweza kuweka yaya.(uk. 27).

Kuwaacha watoto wachanga kama hawa peke yao, hasa wakati wa usiku, ni kuwaweka katika hali ya hatari. Vipo visa vingi sana vinavyoripotiwa magazetini vya watoto ambao huachwa na wazazi majumbani na kuchomeka. Katika muktadha huu basi mwanamke malaya, kama anavyowakilishwa na Shida, anavuliwa utu wake kiasi kwamba anakuwa kama mnyama. Shida hana huruma kwa watoto wake wala hajali wala kubali anapowaacha peke yao usiku kwenda kufanya umalaya.

Mwanamke mwingine malaya ni Sikujua ambaye, kama Hadija, ameondoka nyumbani kutokana na shindikizo za babake aende akatafute kazi ya mshahara ili ajitegemee na kuwatunza wao. Anapokosa kazi, anaingilia umalaya. Heri kwa upande wake anatoroka kwa dadake ili apate 'uhuru' kama anavyosema yeye mwenyewe. Inavyobainika ni kwamba wanawake hawa wote wanafanya umalaya ni wasinacho na udhaifu wa kiuchumi ndio unaowlazamisha kujiuza ili kuyaendesha maisha yao.

Inabidi tueleze pia kuwa taswira hii ya mwanamke kama malaya inamwonyesha mwanamke kama chombo cha kujitumbuiza nacho katika uhusiano wake na mwanaume. Mwanaume anamnunua mwanamke ili kujifurahisha.

Mwanamke kama mzazi ni taswira inayojitokeza katika maandishi mengi ya kifasihi na hasa fasihi ya kike. Waandishi wengi wa kike hudiriki kuonyesha shida ambazo huambatana na jukumu la mwanamke kama mzazi. Chogo katika tamthilia hii anatumbea wanawake ambao uzazi unakuwa chanzo cha shida zao. Kwa mfano tunamwona Mwaire akilazimika kuingilia umalaya ili angalau apate pesa za kuwalisha watoto wake. Inambidi pia abane kwa Msafiri ijapokuwa hana chochote apatacho kutoka kwake. Hata Shida 'anapomzulia mbinu' za kujitafutia riziki, Mwaire anachelea; kwanza kwa sababu ameolewa; na pili kwa sababu ana watoto.

Mwanamke kama kiongozi hakupewa jukumu au nafasi kubwa katika tamthilia hii. Mwanamke kiongozi tunayekutana naye ni Bi. Kamati ambaye ndiye mwenyekiti wa Kamati ya Usahihishaji wa Wanajamii. Kama kiongozi, anaiongoza kamati yake kupitisha sheria ambayo inaufanya uozo wa kijamii kama tunaokumbana nao katika tamthilia hii kutokuwa halali. Hata hivyo, baadhi ya wanaume katika kamati ile wanamdharau kwa kuwa ni mwanamke. Mazungumzo yafuatayo baina ya Adamu na Kuwili yanatuonyesha mielekeo halisi waliyo nayo wanaume dhidi ya uongozi wa wanawake:-

ADAMU: Ehe, hebu nieleze.

KUWILI: Huo mkutano?

ADAMU: Ndio, ulikuwaje?

KUWILI: (Akicheka kwa dharau) wacha tuletewe mwanamke huyo, sijui bi-bi-bi nani huko hata sikumbuki tena; eti ndiye mwenyekiti.

ADAMU: Na wanawake wakipewa tu nafasi ujue taabu(uk. 29).

Mwanamke huyu amekusudiwa na mwandishi kuwa kielelezo cha kiongozi mwelewevu anayeweza kuiongoza jamii kutatua baadhi ya matatizo yanayoyoikumba. Kwanza, kama tulivyotaja hapo awali, ndiye anayeiongoza Kamati ya Usahihishaji wa Wanajamii kupitisha sheria dhidi ya umalaya. Pili, watu wanapofikishwa mbele ya kamati hii, anataka mambo yaendeshe kwa utaratibu ili haki itendeke ( uk. 46). Kwa mfano, waliofikishwa mbele ya kamati wanapolalamika kuwa walitiwa nguvuni bila hatia, anamtaka polisi aeleze kitendo chake. Juu ya hayo anampa kila mmoja wao nafasi ya kujitetea dhidi ya mashtaka yanayowakabili. Hata hivyo, mwanamke huyu hajakuzwa vya kutosha kama mhusika ili kuweza kulibeba jukumu hili muhimu.

### 3:4:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Kama tulivyotangulia kusema, Kortini Mtu Huyu ni tamthilia ambayo imeumbwa katika mazingira ya kimji. Mazingira ya mji ni mapya kwa kiasi fulani katika bara la Afrika kwani ni jambo ambalo limezuka kutokana na majilio ya wageni hasa wa kimagharibi pande hizi. Angelina Chogo anaiandika tamthilia hii katika kipindi cha mpito. Anaandika wakati ambapo nchi yake imejire-jeshea uhuru wake kutoka kwa wakoloni. Wakoloni waliacha nyuma athari za kiuchumi na kitamaduni. Kwa hivyo, hiki ni kipindi ambapo utamaduni wa kijadi unapoteza hadhi yake na watu wanalazimika kwenda mijini kutafuta kazi ili kujipatia riziki. Kutokana na haya, hiki kinakuwa ni kipindi cha mpito pia kuhusiana na utamaduni. Hata hivyo, kuna aina nyingine ya mpito Chogo anapoandika. Huu ni wakati ambapo Tanzania ya wakati huo ilikuwa ikitekeleza Azimio la Arusha la mwaka wa 1967

ambalo liliingiza siasa ya ujamaa nchini Tanzania kwa lengo la kuleta usawa baina ya wananchi wote. Matatizo na uozo anaoshughulikia Chogo ni baadhi ya matatizo na uozo uliosakini Tanzania wakati huo. Je, wanawake waliathirika vipi na heka heka hizi? Katika tamthilia hii, wengi wa wahusika anaotusawiria mwandishi ni malaya ambao wamelazimika kuingilia umalaya kwa sababu moja au nyingine. Isipokuwa Bi. Shiba, wanawake wale wengine tunaokutana nao hawana nguvu za kiuchumi wakiliunganishwa na wanaume.

Wanaume kama vile Msafiri, Bwana Shiba, Adamu, Kuwili na mzee Bakari ni watu ambao wanajitegemea kiuchumi. Isipokuwa Bi. Shiba ambaye tunaambiwa anafanya kazi. Hata pale ambapo amejaribu kutuambia mhusika kama huyu ambaye anafanya kazi, anamweka chini ya utawala wa mumewe. Kwa kufanya hivi, mwandishi anaonekana kuendeleza imani kuwa mwanamke daima lazima amtegemea mwanaume kiuchumi na ili aendelee kupata hifadhi ya kiuchumi, lazima amnyenyekee, kumsujudia na kumtumikia mwanaume wakati wote. Kielelezo cha mwanamke wa aina hii ni Bi. Shiba. Bi. Shiba mwanamke ambaye anafanya kazi sawia na mumewe Bwana Shiba. Hata hivyo, wakitoka kazini, lazima ampikie, kumwandalia na kumtandikia mumewe. Bi. Shiba hafanyi juhudi zozote kujikomboa kutokana na idhilali ya namna hii. Anachofanya ni kulalamika tu lakini kauli ya mwisho ni ya mumewe kama inavyobainika katika maneno yafuatayo ya mumewe.

Mtumishi au bila mtumishi mimi  
sijali mradi nile, You see (kur. 1-2).

Hali kama hii pia inajitokeza katika uhusiano baina ya Msafiri na Mwaire. Wanapokutana mara ya kwanza Msafiri amesawiriwa kama mwokozi wa Mwaire kutokana na matatizo yake yote ya kiuchumi. Anakubali kuolewa na Msafiri kwa sababu ya ahadi ya maisha bora. Baadaye mambo yanapoenda kombo, juhudi anazozifanya kujihami kiuchumi hazifui dafu. Mwishowe, kutokana na ushauri wa jirani yake Shida, anaingilia umalaya. Mwandishi anaturudisha pale pale, mwanamke lazima amtegemee mwanaume kiuchumi. Ndiposa mwishowe wanapotiwa mbaroni na kufikishwa mbele ya kamati ya usahihishaji wa jamii, kamati inaamuru Msafiri akatwe nusu ya mshahara wake ili apewe mkewe Mwaire. Hapa, mwanamke anawekwa chini ya ubawa wa kiuchumi wa mwanaume ambaye hamtaki. Tazama kwa mfano jinsi (Msafiri) anavyomkana kadamnasi ya watu:-

HERI: Yaani huyu ni mke wako na ana watoto wako?

MSAFIRI: Ni mwanamke tu, ana watoto huko na huko anataka kunisakama tu. Mradi nimeshamwona mara moja anadhani mie ni nani kwake? Mtu kama huyu anaweza kuwa mke wangu kweli? (uk. 35).

Kamati inayoamuru mshahara wa Msafiri ukatwe ili kumtunza Mwaire na watoto wake imekabidhiwa jukumu la kuisahihisha jamii. Inaonekana kuwa njia ya kipekee wanayoweza kulitatua tatizo la mwanamke ni kumfungamanisha na mwanaume ili kumfanya amtegemee yule mwanaume. Hili ndilo suluhisho la mwandishi kwa tatizo hili. Mwandishi haonekani kulipinga jambo hili. Msimamo wake unawakilishwa na kamati ambayo kwake ndiyo 'Daktari' wa jamii.

Tatizo la Sikujua halitatuliwi kwa njia iliyo tofauti. Sikujua anawambia alitoroka nyumbani baada ya kuona kuwa alikuwa ananyanyaswa kila siku na wazee wake waliokuwa wakimtaka afanye kazi ili ajitegemee na kuwatunza wao. Hata hivyo, mwishowe kamati inamrudisha kwa wazee wale wale:-

BW. KAMATI: Na katika kikao hiki tunachukua hatua ya kukieleza chama cha wazazi dosari hii ya wazazi, tukitumaini wazazi wataelimishana au kupeana mawazo zaidi kuhusu wajibu wao. Sikujua utarudishwa nyumbani kwenu, na mkuu wa chama cha wazazi huko kwenu atapewa mamlaka ya kuwahoji wazee wako ili uweze kuishi nao tena na kujipatia riziki yenu kutokana na mashamba, bustani, mifugo au mengine yanayoweza kufanywa huko vijijini ... (uk. 50).

Kwa kumrudisha Sikujua kijijini, Chogo hajalitua tatizo lake. Je, ni kweli kwamba huko vijijini ataweza kujitegemea kiuchumi? Suluhisho analolipendekeza Chogo halichimbichanzo cha tatizo lenyewe bali ni la kijuu juu. Anashindwa kuona kuwa mbali na kutolitua tatizo la Sikujua la kiuchumi, hakuna uwezekano kuwa Sikujua ataheshimiwa kama mwanamke.

Heri pia anarudishwa vijijini. Tunadhani vijiji anavyozungumzia Chogo ni vijiji vya ujamaa vilivyokuwa vinaanzishwa na serikali ya Mwalimu Julius Nyerere ya wakati huo kuambatana na siasa ya ujamaa. Kuwarudisha wahusika hawa vijijini ni kielelezo cha mwandishi kuliunga mkono Azimio la Arusha. Je, hili ni suluhisho lililo na misingi yake katika hali halisi ya kiuchumi na kitamaduni?

Jambo hili tutalirejelea baadaye katika sura hii.

La muhimu kutaja hapa ni kuwa wahusika wote wa kiume hawaondoshwi mjini kama wanavyofanyiwa Sikujua na Heri. Hapa, tuna maswali kadhaa ya kujiuliza. Je, ni kweli kwamba matatizo na uozo anaotuumbia mwandishi unatokana na kukamia uhuru (kwa mfano Heri), wazazi (kwa mfano Sikujua) au wanaume (kwa mfano Hadija na Mwaire)? Tatizo hili la mwanamke linaweza kueleweka katika muktadha wa utamaduni mkongwe ambao unamtwaza mwanaume na kumtweza mwanamke na pia katika mfumo wa kibepari ambao unamweka mwanamke pamojana wadhulumwiwa wengine wote katika hali duni ya kiuchumi na kupigia bei kila kitu. Hapa, ibainike kuwa katika mfumo wa kibepari, sio wanawake wote wanaohiniwa kiuchumi. Hata hivyo, baadhi ya wanawake wale ambao ni maskini wanalazimika kujiuza kama njia ya kipekee ya kujipatia riziki. Pengine hii ndiyo sababu tunakutana na wahusika wanawake wengi malaya katika fasihi ambayo imeibuka katika mazingira ya kimji.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi anashindwa kuliweka tatizo hili katika muktadha wake halisi na hii ndiyo sababu inayomfanya atoe masuluhisho ya kijuu juu. Je, iwapo uhusiano baina ya wanaume na wanawake ni kama ule tunaoumbiwa katika ndoa baina ya Bwana na Bi. Shiba au ule baina ya Hadija na babake, kwenda kwao kuishi katika vijiji vya ujamaa kutaleta usawa baina yao katika misingi ya kitamaduni? Tunataka kutilia mkazo hoja kuwa ijapokuwa Chogo kwa kiasi fulani anachimba misingi ya uozo anaotuwasilishia, masuluhisho anayopendekeza yanatibu dalili za ugonjwa wala sio ugonjwa wenyewe.

Awali tumetaja kuwa wanawake wanarudishwa vijijini na wanaume kuachwa mjini. Katika muktadha wa Kiafrika, mijini ndiko kunakopatikana viwanda vinavyoliendesha gurudumu la uchumi hasa katika hali ambapo bidhaa zinabadilishwa kwa pesa. Mijini pia ndiko kwenye makao ya serikali na kazi nyingi za hadhi hupatikana huko. Kwa kuwarudisha wanawake hawa vijijini, mwandishi anawanyima nafasi ya kushiriki katika nyanja hizi muhimu za ujenzi wa taifa. Kwa kufanya hivi, tunaonelea kuwa mwandishi anatilia nguvu itikadi za kijadi kuwa jukumu kubwa la mwanamke liko nyumbani na jikoni.

Iwapo wanawake kama vile Bi. Kamati wamekusudiwa kuwakilisha jukumu la mwanamke katika jamii mpya, basi maoni yetu ni kuwa Chogo hajamjenga mwanamke huyu kiasi cha kuweza kulibeba vya kutosha jukumu hili kubwa alilomvisha. Kwa kushindwa kufanya hivi, inadhihirika kuwa hana msimamo thabiti kuhusu jukumu na nafasi ya mwanamke katika jamii hii ambayo inakusudiwa kujengwa kupitia Azimio la Arusha. Kwa nini tunasema hivi? Angelina Chogo ni mwandishi wa kisanaa. Pili, Angelina Chogo ni mwandishi wa kike. Kulingana na Majola Mbele (1980:50-1):

Kwa kawaida, mwandishi anapasa kuwa msemaji wa jamii, na fasihi huelezwa kama jinsi jamii inavyojieleza kisanaa ... Katika mkabala huu, inakisiwa kuwa mwandishi huendeleza ilihamu na tajriba ya pamoja ya jamii ... "jamii" ni dhana isiyoeleweka kikamilifu. (Dhana hii) inapuuza na kugubika uhalisi wa matabaka ya kijamii na maslahi ya matabaka haya ambayo daima yanapingana. Katika jamii yenye matabaka, msanii hawezi kuepuka kujihusisha na kushiriki mtazamo wa kiulimwengu wa tabaka maalumu. Kwa

hivyo, kwa sababu mwandishi haepukani na itikadi na fikra za kitabaka, anaelezewa vizuri kama msemaji wa tabaka badala ya jamii kwa jumla.

Maoni kama haya ya Mbele yametolewa na Ngugi wa Thiong'

(1981:6) anaposema:-

...Fasihi huegemea upande mmoja; na hasa katika jamii yenye matabaka... mwandishi hutokana na tabaka, rangi au taifa fulani. Yeye binafsi ni zao la harakati maalumu za kijamii-kula, kunywa, kujifunza, kupenda, kuchukia - na amepata mwelekeo wa kitabaka kuhusu harakati hizi...mwandishi anajaribu kutushawishi, kutufanya tuione hali fulani sio tu katika uhalisia fulani bali pia kwa mtazamo fulani... kwa niaba ya tabaka, rangi au taifa fulani.

Ibainike kuwa Mbele na Ngugi wanapozungumza juu ya fasihi, wanamaanisha fasihi ambayo ni tumikizi (committed Literature). Wasomi hawa wanazungumza juu ya fasihi yenye mrengo wa kijamaa kama ilivyoelezwa na Marx na waasisi wa itika ya uhalisia wa kijamaa. Tumetaja hapo awali kuwa itikadi ya Umarx haituonyeshi waziwazi jinsi ambavyo mwanamke atakombolewa kutokana na mikatale ya kitamaduni inayowaweka chini ya utawala wa wanaume. Engels ( toleo la 1985:114) anaeleza kuwa jawabu la mahusiano baina ya wanaume na wanawake litapatikana (baada ya ubepari kung'olewa) baada ya kizazi kipya kuzaliwa na kukua; kizazi cha wanaume ambacho maishani mwao kitakuwa hakijabadi-lisha pesa kwa mapenzi na kizazi cha wanawake ambacho kitakuwa hakijipeani kwa wanaume isipokuwa tu kwa mapenzi. Kwa maoni ya Marx na Engels, ukombozi wa wanawake ni wa pole pole (evolutionary) na unakuja baada ya mapinduzi au ukombozi wa kijamii.

Swali la kujiuliza ni iwapo kwa kuwasawiri wahusika wake wa kike jinsi anavyowasawiri Chogo ni mtetezi wa maslahi ya wanawake kama wadhulumiwa katika nyanja mbili tulizozia nisha. Kabla hatujatoa kauli yetu tutamrejelea Anatoly Lunacharsky (1965:ii) ambaye anasema:-

Kazi ya fasihi huonyesha ... mtazamo wa tabaka ambalo mwandishi anawakilisha au labda, kama inavyotendeka mara nyingi, huonyesha mchanganyiko wa mambo mengi ambayo kupitia kwake tunaweza kubaini athari za matabaka mbalimbali.

Kutokana na maoni haya ya Lunacharsky, tunaweza kusema kuwa mwandishi anaweza kutokuwa na msimamo thabiti kutokana na athari alizozitaja. Chogo anaelekea kuwa mwandishi wa namna hii. Ijapokuwa mwanzoni anaelekea kuwalaumu wanaume kuwa shida zinazowakumba wanawake, kwa kuwaondosha wanawake mjini mwishoni mwa mchezo, anaonekana kujipinga mwenyewe. Iwapo wanaume ndio chanzo cha uozo aliotusawiria, basi ndio wanaopasa kusahihishwa wala sio wanawake. Katika kiwango cha kisaikolojia, mwandishi anaonekana kuamini kuwa wanawake ndio wabaya.

Tunamtarajia Chogo kama mwandishi wa kike kutusawiria wahusika wa kike ambao wanawakilisha tajriba na hali halisi ya mwanamke katika jamii na kwa mtazamo wa kike. Hili ni jukumu tunalolitarajia kutoka kwa msanii yeyote anayeletea maslahi ya tabaka au kundi lake ambalo kwa namna moja au nyingine linadhulumiwa au kuhiniwa haki zake. Hoja hii inaelezwa vizuri na mwandishi wa kike kutoka Afrika Magharibi Ama Ata Aidoo (1987: 23) katika mahojiano yake na Sara Chetin anaposema:-

Swali la kujiuliza ni iwapo kwa kuwasawiri wahusika wake wa kike jinsi anavyowasawiri Chogo ni mtetezi wa maslahi ya wanawake kama wadhulumiwa katika nyanja mbili tulizoziainisha. Kabla hatujatoa kauli yetu tutamrejelea Anatoly Lunacharsky (1965:ii) ambaye anasema:-

Kazi ya fasihi huonyesha ... mtazamo wa tabaka ambalo mwandishi anawakilisha au labda, kama inavyotendeka mara nyingi, huonyesha mchanganyiko wa mambo mengi ambayo kupitia kwake tunaweza kubaini athari za matabaka mbalimbali.

Kutokana na maoni haya ya Lunacharsky, tunaweza kusema kuwa mwandishi anaweza kutokuwa na msimamo thabiti kutokana na athari alizozitaja. Chogo anaelekea kuwa mwandishi wa namna hii. Ijapokuwa mwanzoni anaelekea kuwalaumu wanaume kuwa shida zinazowakumba wanawake, kwa kuwaondosha wanawake mjini mwishoni mwa mchezo, anaonekana kujipinga mwenyewe. Iwapo wanaume ndio chanzo cha uozo aliotusawiria, basi ndio wanaopasa kusahihishwa wala sio wanawake. Katika kiwango cha kisaikolojia, mwandishi anaonekana kuamini kuwa wanawake ndio wabaya.

Tunamtarajia Chogo kama mwandishi wa kike kutusawiria wahusika wa kike ambao wanawakilisha tajriba na hali halisi ya mwanamke katika jamii na kwa mtazamo wa kike. Hili ni jukumu tunalolitarajia kutoka kwa msanii yeyote anayeletea maslahi ya tabaka au kundi lake ambalo kwa namna moja au nyingine linadhulumiwa au kuhiniwa haki zake. Hoja hii inaelezwa vizuri na mwandishi wa kike kutoka Afrika Magharibi Ama Ata Aidoo (1987: 23) katika mahojiano yake na Sara Chetin anaposema:-

(Lakini) mimi ni mwanamke. Watu mara kwa mara husema kuwa wengi wa wahusika wangu ni wanawake kama kwamba hili ni tatizo. Kuna mtu ambaye anamwuliza mwandishi wa kiume kwa nini wengi wa wahusika wake ni wa kiume? ... kama ungekuwa ukiongea na Soyinka, Ngugi, Achebe ungewauliza kwa nini wengi wa wahusika wao au mashujaa wao ni wanaume mara nyingi? Inapasa kukisiwa kuwa iwapo nitaandika juu ya matatizo, nitafanya hivi katika mtazamo wa kike kwa sababu mimi ni mwanamke (msisitizo ni wetu). (Tazama pia Moira Monteith 1986:1)

Kwa kumalizia, tungependa kusema kuwa Chogo hajamsawiri mhusika yeyote wa kike ambaye anafanya juhudi zozote kujikomboa. Hajihusishi kwa njia yoyote ile na swala la ukombozi wa wanawake. Kwa kutofanya hivi, mwandishi anashindwa kutusawiria mhusika yeyote ambaye anaweza kuigwa na wanawake wadhulumiwa katika jamii.

Pengine tatizo kubwa katika mchezo huu linatokana na jinsi mwandishi huyu anavyoyashughulikia maswala yote anayoyajadili. Mchezo huu ni dhaifu kimaudhui, kimuundo na kimtindo. Kwa upande wa wahusika, usawiri wao pia ni dhaifu kiasi kwamba tunalazimika kuiweka kazi hii katika kijopo cha kazi anazozielezea Senkoro (1987:36) ifuatavyo:-

Wakati huo huo (kazi hizi) zilitimiza masharti ya mfumo wa kibepari, kwani hazikujihusisha na matatizo halisi ya watu wanyonge; na pale zilipoyashughulikia zilipotosha ukweli na uhalisi wa matatizo hayo. Zilitoa majibu ya mkato sawa na lile la kurudi vijijini, zikashauri kuwa jawabu liko katika polisi, mahakama na jela.

Ifahamike kuwa mchezo huu unatoa majawabu haya anayozungumzia Senkoro. Kwa mfano wahusika 'wahalifu' wanatiwa mbaroni na polisi na kufikishwa mbele ya kamati ya Usahihishaji

wa jamii ambayo inaamuru baadhi yao wafikishwe kortini. Wana-  
wake wanarudishwa vijijini ili wakarekebishwe tabia. Suluhisho  
la namna hii, licha ya kuwa linapotosha lengo la vijiji vya  
ujamaa hapo hapo linashindwa kuipambanua hali halisi na kuipo-  
tosha jamii. Polisi ambao hutumiwa na watawala kuhimili tawala  
zao hawawezi kuleta suluhisho kwa matatizo yanayoikumba jamii.

### 3:5 PENINA MUHANDO (1972): HATIA

#### 3:5:1 HADITHI KWA UFUPI

Hatia ni mchezo wa kwanza katika mfululizo wa michezo  
tisa ya kuigiza aliyowahi kuiandika Penina Muhando. Matukio  
muhimu katika mchezo huu yanazunguka maisha ya Cheja; msichana  
mdogo ambaye kutokana na umaskini uliopo nyumbani kwao analazi-  
mika kuondoka kwenda Dar es Salaam kufanya kazi katika nyumba  
ya Bwana Sembuli, rafiki ya babake. Akiwa huko Dar es Salaam,  
anakutana na Juma Bakari ambaye anamhadaa kuwa anampenda na  
kufanya mapenzi naye. Cheja anachukua mimba lakini anapomju-  
lisha Juma, Juma anakana. Hata hivyo, kabla hawajaachana,  
anamshauri Cheja amsingizie mwajiri wake.

Cheja anaondoka nyumbani kwa Bwana Sembuli bila taarifa.  
Siku anapofika nyumbani kwao, babake anapata barua ya Bwana  
Sembuli ikimwarifu kuwa Cheja ametoroka nyumbani kwake na  
hajulikani alipo. Babake Cheja anamfokea sana kwa kitendo  
hicho huku akitaka kujua kilichomfanya atoroke. Cheja anamwa-  
rifu kuwa amenajisiwa na Bwana Sembuli na kwamba ni mja mzito.  
Baadaye baraza la wazee linaamua kuwa Sembuli, ambaye amefika  
pale kijijini baada ya kumtafuta Cheja kwa siku nne, aapishwe

ili kutafuta ukweli kwani amekataa kuwa alifanya kitendo hicho. Sembuli haamini mambo ya viapo. Kwa hivyo, anasema kuwa Mkami, kakake Cheja, ndiye aliyefanya hivi na ni lazima aapishwe kwanza. Jambo hili linaamsha ugomvi wa zamani uliokuwepo baina ya ukoo wa Cheja na ukoo wa Sembuli na kuwafanya wapigane na kuumizana sana. Baada ya vita hivi, Cheja anawaambia ukweli na kuomba msamaha. Haya yanatokea anaposhindwa kujinyonga. Mwishowe anaamua kujiunga na kijiji cha ujamaa cha Majogo ili aweze kufanya kazi na kujitegemea.

### 3:5:2 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Pengine kufikia hivi sasa, tamthilia ya Muhando iliyo-wahi kujadiliwa sana ni Hatia; hasa kuhusu jinsi anavyowasawiri wahusika wake wa kike. Maoni mbalimbali yametolewa juu ya swala hili. Omboga (1986) anatoa maoni kuwa katika kusimulia kisa cha tamthilia hii, Muhando anazusha maswala muhimu ya kijamii na mojawapo ya maswala haya ni nafasi ya mwanamke katika jamii. Maoni kama haya yametolewa pia na Kiango na Sengo (1974). Omboga anaeleza kuwa mwanamke katika Hatia amewakilishwa kama kitovu cha maovu yote ya kijamii. Ameonyesha kuwa kiumbe mnyenyekevu, mpumbavu na mdhaifu ambaye yu radhi kumtumikia mwanaume. Omboga anaonelea kuwa hali hii inaendelezwa katika nyingi ya tamthilia za Muhando.

Chesaina (1987) na Matteru (1987) wanatoa maoni tofauti na ya Ombaga. Chesaina anaonelea kuwa Hatia ni mchezo ambao unatupigia maswali kuhusu uhuru wa mwanamke na hasa kuhusu swala la mwanamke kujiamulia jukumu na hatima yake katika

maisha. Katika mkabala huu, Muhando analichukulia tatizo la Cheja kuwa na misingi yake katika unyonge wa kiuchumi wa mwanamke na pia katika taasubi za kiume ambapo mwanamke anaonekana kuwa chombo cha kujitajirisha, kujifurahisha, kuzaa na kiumbe mpumbavu ambaye anapasa kuchukua nafasi ya pili baada ya mwanaume. Kwa hivyo, nje na ndani ya ndoa, mwanamke anadhulumiwa na kuamwa jasho lake.

Matteru (1987) kwa upande wake anatoa maoni yanayooana na ya Chesaina. Hata hivyo, Matteru anamuona Muhando kama mwandishi ambaye yuko katika njia-panda. Anaeleza kuwa taswira za mwanamke zinazoendelezwa katika kazi za Muhando ni zile za kijadi. Anaonelea kuwa taswira hizi zina uwili. Kwa upande mmoja, zinaweza kuchukuliwa kijuu juu na hapa itaonekana kama kwamba Muhando anakubaliana na udhahilishwaji wa wanawake. Kwa upande mwingine, inabainika kuwa kwa kufanya hivi, Muhando anaikashifu jamii inayoendeleza uozo wa namna hii. Anasema:-

Kwa kusawiriwa hivi, wahusika wa Penina wanaashiria utata anaokumbana nao mwandishi. Hawezi kuwasawiri wahusika ambao wanakiuka taswira zinazoendelezwa mara kwa mara kwa sababu kwa kufanya hivi, atakuwa anapotosha uhalisi (Matteru 1987:42).

Tutayachambua maoni ya wahakiki hawa katika sehemu inayofuata. Hebu sasa tuangalie taswira za mwanamke ambazo zinapatikana katika tamthilia hii.

Mwanamke katika tamthilia hii amesawiriwa katika mazingira ya utamaduni mkongwe wa kiafrika. Katika mazingira haya, mwanamke anachukuliwa kuwa chombo cha kujifurahisha. Katika mkabala huu, msichana analelewa na kutunzwa vizuri ili

baadaye akiolewa wazazi wake waweze kuchuma kutokana na ndoa yake. Ili kuhakikisha kuwa hili linatendeka, anachungwa sana ili asipate mimba nje ya ndoa. Kwa mfano katika thamthilia hii, tunafahamishwa kuwa Mkami, kakake Cheja, 'anangoja mali ya dadake ili aoe nayo' (uk. 11). Cheja, ambaye ni limbukeni hasa katika maisha ya kimji, anapopata mimba inakuwa ni kama kwamba amewakatizia matumaini yao. Maneno ya Mkami yanaashiria ukweli huu:-

MKAMI: (Kwa haraka) Ng'ombe saba, mbuzi tisa,  
na kuku watatu.

WOTE: Kaaa! (wanacheka)

MZEE CHIMAIISI: (Huku anacheka) Babu vipi? Unataka  
ujipatie ng'ombe wa kuolea hapo hapo?

MKAMI: Ndio, kwanza huyu dadangu  
angeolewa vizuri angepata zaidi ya hizo.  
Sasa yeye kajitia kumharibu lazima alipe.  
Kwanza yeye tajiri. Mtu ana hata gari  
( uk. 18).

Tungetarajia kwamba, kwa sababu Cheja ameingia taabuni, wazee hawa wangetumia busara yao kumsaidia na kwa vile ambavyo ni msichana mdogo, wangemsaidia pia kulikabili tatizo hili kisaikolojia. Kinyume na matarajio, wanafikiria tu jinsi ambavyo watachuma kutokana na janga hili. Tazama jinsi wanavyolishughulikia swala hili chapu chapu kisha mzee Chimaisi, mzee anayeheshimika anapitisha hukumu ifuatayo:-

Haya sasa basi, kama alivyokuwa akisema mzee mwenzetu hapo mwanzo, adhabu ya Sembuli ni malipo. Na kama ilivyo jadi yetu, malipo yenyewe ni sehemu tatu yewe kwa vile ametumia nguvu. Kwanza malipo ya wazazi, Pili malipo ya msi-chana mwenyewe na tatu, malipo ya kutunza mtoto atakapozaliwa. Sasa basi, tuanze malipo ya wazazi ( uk. 18). (Msisitizo wetu).

Hapa, ni wazi kuwa malipo yanawekwa mbele ya utu.

Cheja mwenyewe hata hashauriwi.

Pengine taswira mbaya zaidi ni ile ya mwanamke kama kiumbe dhaifu na mpumbavu ambaye hana usemi dhidi ya mwanaume au juu ya jambo lolote hata lile linalomhusu. Hii ni taswira inayojikita katika utamaduni wa jamii unaoendeleza taasubi ya kiumbe. Kwa mfano haiyumkiniki kuwa Cheja, mwanamke na mtoto, anaweza kusimama mbele ya baraza la wazee na kuzungumza hata mambo yanayojadiliwa yawe yanamhusu yeye. Shauri la Sembuli kwamba Cheja aitwe aeleze kama kweli yeye Sembuli ndiye aliye-mfanyia hivyo linawagutusha wazee. Kufanya hivyo ni sawa na kuwavunjia heshima na kuwadharau wazee. Tazama maneno ya mzee I:-

Wazee sasa mwataka kujidharau wenyewe pamoja na jadi yetu. Mna maana kusema kuwa sisi wazee wote hapa na mvi zetu tumeshindwa na jambo hili hata tumwite mwanamke, tena msichana mdogo, aje aseme? Mliona wapi mambo kama haya jamani? (uk. 21) (Msisitizo wetu).

Ibainike kuwa hakuna mwanamke hata mmoja katika baraza hili. Lakini hivi si kusema kwamba wanawake hawana lolote wanaloweza kuchangia katika kulitatua tatizo hili. Kwa mfano, wanawake ndio wanaomshauri Bw. Chowe asiyafanyie mambo pupa. Wanamshauri angoje mpaka siku inayofuata ambapo anaweza kuwapa wazee wote. Vile vile, wanamshauri kuwa ni kukosa heshima kutoenda kumlaki mjombake ambaye anatazamiwa kufika siku hiyo. Ikiwa wanawake wana busara kama wanavyodhihirisha hapa, kwa nini hawashirikishwi katika baraza la wazee? Swala hili tutalichambua na kulijadili kwa undani zaidi tutakapokuwa

tunaujadili msimamo wa mwandishi.

Mwanamke anadharauliwa na kufedheheshwa katika jukumu lake kama mama. Kwa mfano mamake Cheja anapigiwa makelele na kutukanwa mbele ya wanawake wenzake licha ya kuwa ni kwa makosa ambayo si yake:-

BW. CHOWE: Acha kuniletea upuuzi hapa. Alikwambia atakuja? Kwa nini hukumwuliza? Vipi anafanya kutoroka na kuwasumbua akina Sembuli? Jambo la aibu na wewe. Walicheka kama mpumbavu. Mwhite hapa Cheja aeleze sasa hivi nini kimemtorosha. Jamani wanawake wengine kumbe wajinga. Upesi kamlete mtoto wako kabla ghadhabu yangu haijavuka kiwango. Shenzi kabisa.

BI. CHOWE: Cheja! Cheja! Sasa na mimi nimekosa nini jamani?

BW. CHOWE: Hivyo wewe unajua maana ya kwenda kuleta kitu? Nimesema nenda kamlete hapa. Punda wee. Kama kuna mambo mmeyapanga wewe na mtoto wako leo mtanieleza au mtaniona.

...  
MWANAMKE I: Yaani hiyo simu haikueleza sababu yoyote ya kutoroka kwake?

BW. CHOWE: (Hamjibu mwanamke I) Upumbavu.  
Upumbavu.

Hapa, hatuoni kwa njia yoyote ile Bi. Chowe akijizatiti kuupinga udhalilishwaji huu.

Mwanamke katika Hatia pia amesawiriwa kama chanzo cha maovu ya kijamii. Cheja analaumiwa kuwa ndiye aliyesababisha umwagikaji wa damu unaotokea kwa sababu ya kitendo chake cha kumsingizia mwajiri wake Sembuli. Ni muhimu kuzingatia kuwa mamake ndiye anayeitoa kauli hii anapomwuliza:-

Sasa Cheja, ona shida zote ulizoleta. Jambo gani hili ulilofanya? (uk. 37).

Hii ni sawa na kuonyesha kuwa wanawake wenyewe wanakubali nafasi waliyopewa na jamii. Swali la kujiuliza ni; iwapo mama yake Cheja hatamwelewa Cheja, badala yake anamlaumu kwa yaliyotendeka kama wafanyavyo watu wale wengine wote, ni nani atamwelewa? Ikumbukwe kwamba jamii hii haimpi mwanamke nafasi ya kujieleza. Pia, inapasa kuzingatiwa kwamba hata Cheja mwenyewe anaelekea kukubali kuwa yeye ndiye mkosaji. Anapoamua kwenda kuishi katika kijiji cha Majogo, anawambia:-

Kwa sababu siwezi kuishi tena  
kijijini baada ya yote yaliyotokea.  
Siwezi. Nendeni mkawaambie wote  
wanisamehe. Uuuuuui! ( uk. 31).

Huu ni uamuzi anaoufanya baada ya kutaka kujinyonga. Anataka kujinyonga kwa sababu anajiona kuwa mkosaji.

Kazi hii itakuwa haikukamilika ikiwa hatutaja kuwa mwanamke kama alivyosawiriwa hapa ni mtumwa nje na ndani ya ndoa na pia anatumwa kama chombo cha kuimarisha na kuendeleza urafiki baina ya wanaume. Izingatiwe kuwa uhusiano baina ya Bw. Chowe na Sembuli umetiliwa nguvu zaidi na hali kwamba Cheja anafanya kazi nyumbani kwa Sembuli. Anapotoroka, babake Bw. Chowe anaudhika sana kwani kufanya hivi ni sawa na kuvunja uhusiano wao na kumwaibisha baba yake. Babake anafoka:-

Hapana mama yangu. Nilifahamu hili litoto lijinga sana. Lakini limeharibiwa na limama lake. Sisi kwenye ukoo wetu hatuko namna hii. Haya yanataka yapigwe ndipo yaseme. Lakini kama ni kupiga tu kwangu si kazi hasa kwa jambo kama hili. Leo nyie, nyie! mama yangu, mimi na Sembuli tunaaminiana halafu leo hili litoto linatoroka hata bila kuaga. Kwani wamekufanyia ovu gani ambayo walishindwa kuli-

fanya miaka miwili yote uliyokaa nao?  
(Kwa sauti) Sema! au nitakung'ong'ota  
sasa hivi. (Anainua fimbo) (uk. 14).

Mbali na maneno haya kuonyesha kuwa mwanamke anachokuliwa kama chombo cha kuimarisha urafiki, yanaonyesha dhambi waliyonayo wanaume kwa wanawake. Ndani ya ndoa, dharau hii inazidi maradufu. Ndiposa tunamwona Bw. Chowe akimtisha na kumtukana mke wake kadamnasi ya watu. Wimbo wa wanawake mwanzoni mwa onyesho la pili pia ni kielelezo cha uhusiano uliopo baina ya wanaume na wanawake katika taasisi ya ndoa. Tunawaona wakiimba wimbo ufuatao:-

Mtiti mtiti chiyombeya (mara mbili)  
Awana walume chiwakole naki  
Chiwakole na mphindi ya mugwa  
Chimbeya (uk.10).

Wanachouliza wanawake hawa ni kile watakachowafunga wanaume nacho. Jawabu wanalojitolea ni kwamba watawafunga na muwa. Je, hili ni suluhisho kwa matatizo yao? Pengine taswira hii inajitokeza waziwazi zaidi kupitia kwa mazungu ya wanawake hawa wanapotwanga:-

BI. CHOWE: Ee jamani, shauri ya uzee.  
Hivyo na mwanangu Cheja mnamwona amekuwa mama mzima bado mnategemea nina nguvu za kutwanga tu. Kwanza hii yote ni shauri ya umasikini tu. Mwanangu asingekwenda kufanya kazi Dalisalama saa hizi kazi yangu ingekuwa tu ni kufanyiwa kila kazi.

MWANAMKE I: (Anaanza kupepeta) Thubutu! Angekuwa Ameshaolewa anawafanyia kazi wakwe zake na wewe ungebaki hapa hapa (uk. 10).

Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa mwanamke nje na ndani ya ndoa anatumikishwa.

3:5:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Jukumu kuu la fasihi ni kuonyesha hali halisi ilivyo na kuonyesha jinsi ambavyo hali hiyo inaweza kubadilishwa ili kuleta afueni kwa wale wanaonyanyaswa. Abdilatif Abdalla (1980: ix) anatumieza kwamba:-

Kazi ya fasihi si ya kuyaeleza yale yaliyo mema tu na yapendezayo kusikiwa bali kadhalika ina kazi ya kuyaeleza hadharani hata yale matendo maovu ili yajulikanwe na yapate kutafutiwa dawa ... mtunzi wa jamii aliyekomaa haishii kwa kuyaeleza yale yaliyoko mbele ya pazia tu bali hulifungua pazia hilo na kuionyesha jamii hata yale yatendekayo nyuma ya pazia hilo na akawa yuwauliza maswali.

Katika mkabala huu, mwandishi myakinifu anatazamiwa kuwa mkali katika harakati za kuanzisha na kuendeleza urazini wa kijamii na kisiasa. Ni jukumu la mwandishi kuona kuwa urazini huu unalenga kuwazindua wanaonyanyaswa ili waweze kujikomboa. Nadharia yetu inashikilia kuwa mwandishi ni lazima aieleze tajriba ya mwanamke katika jamii ipasavyo ili kuweza kubainisha matatizo anayokabiliana nayo mwanamke katika harakati zake za kujikomboa. Muhando katika Hatia ametuonyesha mwanamke katika hali yake halisi ya kijamii. Ametuonyesha jinsi ambavyo utamaduni mkongwe unamdhalilisha mwanamke na kumweka katika nafasi ya pili baada ya mwanaume. Swali la kujiuliza ni; Je, Muhando anatoa jawabu gani kuhusu ukombozi wa wanawake? Wahakiki wengi wanaonelea kuwa kwa kumpeleka

Cheja katika kijiji cha ujamaa, mwandishi amependekeza suluhisho la tatizo hili ( Tazama Sengo na Kiango 1974, Omboga 1986, Chesaina 1987, Matteru 1987 na Senkoro 1987).

Kwa maoni yetu, uamuzi huu wa Cheja unapasa kutazamwa katika viwango viwili:- Kwanza, kama uamuzi wa Cheja kama mhusika binafsi na pili kama kielelezo cha mwandishi kuliunga mkono Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa kwa jumla. Ni wazi kwamba hakuna uwezekano wowote wa Cheja kurudiana na Juma. Lengo la Juma lilikuwa ni kujifurahisha tu ndiposa anamkana Cheja anapomjulisha kuwa ana mimba yake. Katika kiwango hiki, uamuzi wa Cheja ni wa kufaa hasa ikikumbukwa kuwa wazee wake wako katika harakati za kumtafutia njia ya kumwauni. Jamii ambayo inamsimanga na kumekejili anapopata mimba haiwezi kumpa nafasi ya kujiendeleza. Uamuzi wake basi ni njia ya kujinasua kutokana na mtego huu wa utamaduni mkongwe.

Je, ni kweli kwamba katika kijiji cha Majogo atajii-marisha kiuchumi? Je, ni kweli kuwa katika kijiji hiki atakuwa huru kama mwanamke? Muhando ni mmojawapo wa waandishi wa Kitanzania wa wakati wake walioliunga Azimio la Arusha mkono pasipo maswali. Waandishi kama vile Ndyanao Balisidya katika Shida, Euphrase Kezilahabi katika Gamba la Nyoka, Matthias Mnyampala katika Ngonjera za ukuta miongoni mwa wengineo, ni baadhi ya waandishi ambao katika kazi zao walilisifu na kulipendekeza Azimio hili kama dawa ya ugonjwa uliokuwa unaikumba nchi yao. Katika kiwango cha kinadharia, Azimio la Arusha lilipasa kuleta usawa baina ya watu wote;

wanaume kwa wanawake. Hata hivyo, katika hali halisi, kubaguliwa kwa wanawake kuliendelea. Hali kama hii inadhihirika katika riwaya za Kezilahabi Dunia Uwanja wa Fujo (1974) na Gamba la Nyoka (1979), na tamthilia ya Muhando Heshima Yangu (1974). Kuhusu kazi kama hizi, Senkoro (1987:36) ana haya ya kusema:

Katika kazi hizi, mvutano baina ya mji na kijiji ambao ulileta matatizo ya wizi, ujambazi, umalaya, na mengine ya aina hiyo yalitolewa dawa moja: Kurudi vijijini. Jawabu hili, zaidi ya kutokuwa sahihi kwani linakwepa kiini hasa cha tatizo hapo hapo lilipotoshwa maana ya kijiji kilichotakiwa kuundwa katika jamii ya Tanzania.

Tunakubaliana na maoni haya ya Senkoro. Kwa msingi wa nadharia yetu, mapinduzi ya kijamaa pekee hayawezi kulisuluhisha tatizo la mwanamke kukandamizwa kwa misingi ya uana wake.

Swali lingine la kujiuliza ni kama Muhando anatuonyesha juhudi zozote za wanawake kujikomboa au labda kuisahihisha jamii. Wanawake wengi tunaokutana nao katika Hatia ni wanawake ambao hawajaelimika walinganishwa na wanaume. Wengi wao wanaishi vijijini na wanachojishughulisha nacho ni mbinu za kuweza kuwathibiti wanaume badala ya kujikomboa kama inavyodhihirika katika wimbo wanaoimba wanapotwanga. Wengi wao wamekubali hali yao kama majaliwa. Hata Cheja mwenyewe haonekani kuwa na urazini wowote kuhusu hali yake. Uamuzi wake wa kujiunga na kijiji cha Majogo unakuja kama jambo lililolazimishwa ili kwa njia moja au nyingine mwandishi aunge mkono Azimio la Arusha. Badala yake, Cheja anawekwa chini ya ulinzi wa Sembuli. Hili ni sawa na

kuendeleza itikadi za kijadi kuwa mwanamke lazima alindwe. Kwa kufanya hivi, tunaonelea kuwa Muhandu hana msimamo wala haonyeshi kiyakinifu jinsi ambavyo swala la mwanamke linapasa kushughulikiwa. Inaonekana kama kwamba hataki kuipinga itikadi ya jamii yake. Matteru (1987:42) anasema:-

Ijapokuwa ana (Muhandu) msukumo wa kukiuka mikatale ya jamii yake na kuingia katika nyanja nyingine, anabidika kubakia katika mazingira yake ya kijamii. Kwa kufanya hivi, anawasawiri wahusika wake katika majukumu yao ya kike ya kijadi.

Chesaina (1987) anaonelea kuwa kwa kuwasawiri wahusika wake namna hii, Muhandu 'anawakashifu; wakati mwingine kwa ukali sana, ili waweze kujirekebisha.' Kauli hii ya Chesaina na kauli zake nyinginezo tulizozirejelea hapo awali hatukubaliani nazo. Hata kama Muhandu angekuwa anamkashifu Cheja ili ajirekebishe katika Hatia, kashfa hii ingekuwa haina msingi na imeelekezwa kwa mdhulumuwa badala ya yule anayemdhulumu. Mazingira ya kimji kama yale aliyomuambia Cheja yanawavutia watu wengi. Hata hivyo, mjini, kwa maoni ya Muhandu, si mahali pa watu kama Cheja ambao hawana elimu yoyote. Ni mahali pa akina Sembuli. Lakini swali tunalojiuliza ni; Je, wanawake wana nafasi gani katika aina hii mpya ya uchumi mijini? Wanawaka wanakumbana na kupambana vipi na mazingira haya mapya? Je wanawake wana nafasi ya kutangamana na wanaume kwa usawa? Na iwapo mijini ni mahali pa watu walioelimika, je, hakuna wanawake walioelimika na walio wakakamavu vya kutosha kukabaliana na maisha ya kimji pasipo kuathirika kama afanyavyo

Cheja? Cheja anarudishwa kijijini ilhali Sembuli anabaki mjini. Hali kama hii tumeiona vile vile katika Kortini Mtu Huyu.

Maswali haya na mengine mengi yanatuelekeza katika ukweli kwamba Muhando hana msimamo maalumu kuhusu swala la mwanamke. Hata kama kwa kwenda kuishi Majogo Cheja angekombolewa kiuchumi, tatizo la mwanamke katika jamii si la kiuchumi tu. Mielekeo kuhusu wanawake ni swala linalopasa kushughulikiwa kivyake. Mielekeo ya watu kama vile Bw. Chowe au baraza la wazee itaondolewa vipi katika jamii na hasa katika vijiji vya ujamaa? Je, ni kweli kwamba haiko katika vijiji vya ujamaa?

Pengine ni kwa kutambua ukweli huu ambapo Muhando (1974) aliandika Heshima Yangu ambapo tunakutana na mama Salum aliyelazimika kuficha siri ya aliyezaa naye mwanawe Salum kwa kutishwa na mzee Isa (ambaye ndiye babake Salum) kwamba angeuawa akiitoa ile siri. Mzee Isa ni mmoja wa viongozi wa kijiji cha ujamaa.

Jambo la mwisho ambalo tungependa kulizungumzia katika sehemu hii ni masuluhisho mengine kwa matatizo yanayoi-kumba jamii anayoizungumzia Muhando; mbali na kumpeleka Cheja katika kijiji cha ujamaa. Tunataka kubainisha kama Muhando anawashirikisha wanawake katika kutafuta na kutekeleza masuluhisho haya. Suluhisho lingine analolipendekeza Muhando ni kwamba vijana kama vile Juma Bakari wanapaswa kuelimishwa juu ya ubaya wa maisha wanayoyaendesha. Mazungumzo yafuatayo baina ya wazee na Sembuli yanatuelekeza kwenye suluhisho la namna hii:-

MZEE II: Sasa huyo Juma ndio basi tena?

MZEE CHIMAIISI: Ee; basi; sasa kama mwenyewe  
kakataa sisi tufanyeje?

SEMBULI: Huyo Juma niachieni mimi.  
Hatuwezi kumwacha hivi hivi. Sina  
maana kuwa nitaenda kumkamata  
nimwadhibu au nini. Vijana hao  
hawapatikani kwa jambo kama  
hili. Lakini baada ya yote yaliyo-  
tokea hatuwezi kumwachilia Juma  
aendelea na haya maisha ya kuji-  
potosha yeye pamoja na wengine.  
Tukimwacha atarudia kwa wasichana  
wengine na kuondoa amani mahali  
pengine. Hatuwezi kumwacha.

MZEE 5: Sasa tufanyeje?

SEMBULI: Cheja akishanieleza juu ya  
kijana huyu nitafanya juu chini  
nimpate. Halafu nitajaribu njia  
zozote kumwelewesha ubaya wa  
maisha anayoyaendesha. Lazima  
aelewe kuwa maisha sio kazi,  
pesa na starehe tu. Maisha  
ni uhusiano mwema na binadamu  
wengine.

MZEE 3: Lakini kama kijana mwenyewe ni  
mhuni tu wa mjini, atayasikiliza  
maneno yako?

SEMBULI: Itachukua siku nyingi na njia  
nyingi pia kubadilisha mwenendo  
huu. Lakini penye nia na njia  
ipo ... (uk.40).

Mazungumzo haya yanaonyesha imani ya mwandishi kuwa

ili jamii iweze kusafishwa uozo unaoisakama, lazima ielimishwe.

Hata hivyo, analiwasilisha suluhisho ili kwa njia ambayo inali-

fanya lionekane finyu sana. Kwa mfano hatuoni jinsi ambavyo

kumtafuta Juma na kumwonyesha ubaya wa tabia yake kutaisaidia

jamii hii. Tatizo la Juma na Cheja sio tatizo la vijana hawa

wawili kama watu binafsi. Ni tatizo linaloikumba jamii nzima.

Juhudi za Sembuli za kumtafuta Juma 'akishapata maelezo yake'

kutoka kwa Cheja haziwezi kulisulihisha tatizo hili. Lazima

missingi halisi ya tatizo hili ichimbwe ili suluhisho lenye mantiki lipatikane. Hata hivyo swala muhimu kwetu ni jinsi ambavyo wanawake wanashirikishwa katika juhudi za kutafuta suluhisho hili ambalo linawahusu moja kwa moja.

Kwa maoni yetu, wanawake hawashirikishwi hata kidogo. Jukumu hili linapewa Sembuli; mwanaume. Kwa kufanya hivi, Muhando anaonekana kutokuwa na msimamo thabiti kuhusu nafasi ambayo wanawake wanaweza kuchukua katika kutafuta masuluhisho kwa matatizo yanayowakumba na yanayoikumba jamii yao. Anae-ndeleza imani kuwa masuluhisho ya matatizo yote ya kijamii yanaweza kutolewa tu na wanaume. Hivi ni sawa na kusema kuwa wanawake, kama usemi uendavyo, wanapasa 'kuonekana tu wala sio kusikilizwa.'

### 3:6 PENINA MUHANDO (1975): PAMBO

#### 3:6:1 HADITHI KWA UFUPI

'Pambo ni kitabu kinachotoa mfano kamili wa dhamira ya mgongano unaowapata baadhi ya vijana. Mwandishi anatumia mfano wa kijana Pambo kwa kueleza tatizo hili kwa namna inayovutia sana. Tatizo hili ni kuwa baadhi ya vijana waliohitimu katika elimu ya juu mara nyingine wao huwa na mawazo kuwa elimu ya juu waliyoipata itakuwa ni ufunguo wa kila kitu katika maisha.' (Maelezo katika jalada la nyuma la kitabu).

Mchezo huu unapoanza, tunakutana na Maua, 'mpenziye' Pambo, ambaye amefika nyumbani kwa Pambo. Anamkuta Pambo 'amekaa kimya; ameduwaa na wakati mwingine anapinduapindua macho yake na pengine kuyatoa sana sana' (uk. 1). Ukutani

pametundikwa cheti cha shahada ya digrii na joho la sherehe ya kupata shahada. Maua, ambaye amengojea gari kwa muda wa masaa matatu amekasirika. Haoni sababu yoyote iliyomfanya Pambo asinunue gari, friji, kupata nyumba nzuri na kumstarehesha jinsi wasichana wengine wanavyostareheshwa na 'wavulana' wao. Anamwambia Pambo:-

Basi nakwambia kweli, nimechoka na wewe. Kila siku unajidai utanunua gari, lakini gari lenyewe silioni. Mimi nisingelikwa napata taabu za mabasi namna hii. (kur. 1-2).

Pambo, ambaye wakati huo wote hajazungumza anaanza kuropokwa kama mtu mwenye kichaa. Mambo yale mengine tunayo-yaona kupitia kwa Pambo yanatendeka kichwani mwake. Mwishowe, Pambo na watoto wawili, Raha na Pesa, wanatoroka na kukimbilia msituni. Wakati huo huo kuna mabishano baina ya Maua na Wema ambao ni wapenzi wa Pambo.

Sehemu ya pili ya michezo huu inaonyesha juhudi za kuwatafuta Pambo, Raha na Pesa, kuwaganga na kuwarudisha nyumbani.

### 3:6:2 MAUDHUI KWA UFUPI

Mchezo wa Pambo ni mchezo ambao unajadili jukumu la wasomi katika jamii zao; mathalani wasomi katika nchi za kiafrika. Kupitia kwa mchezo huu, ambao ni wa hali ya juu kimuundo (taz. Sengo 1977:46), Muhando anatuonyesha migogoro na migongano inayotokea baina ya wasomi na jamii zao. Elimu ya kimagharibi inawakengeusha na kuwapotosha wasomi wa kiafrika

kutoka kwa jamii zao (Rodney 1989). Pambo ambaye ni wahusika wawili kwa pamoja amesawiriwa kama kielelezo cha ukengeushi huu. Yeye anaichukulia elimu kuwa pambo. Kulingana na Sengo (1977:47) hali ya maisha imekuwa pambo. Hali hii ndiyo isababishayo watu kuwa na mawazo mengi mazito ambayo hayahusu matatizo ya jamii zao bali yanahusu matatizo yao binafsi. Pambo ni kielelezo cha wasomi ambao waliamini na bado wanaendelea kuamini kwamba al-muradi mkoloni ameondoka, wao ndio wanaostahiki kuchukua nafasi zao. Wasomi hawa ambao mtazamo wao ni wa kimagharibi huwa na pupa ya kujilimbikizia mali ilhali wananchi wa kawaida na ambao ndio wazalendo halisi waliopigania uhuru na kuwaelimisha vijana kama hawa, wanaishi maisha yaliyojaa dhiki ya njaa na umaskini.

Katika mkabala huu, Muhando anatusawiria kijana Pambo ambaye ana kichaa kwa sababu ya kiu ya pesa, kiu ya raha, kiu ya cheo na kiu ya starehe; magari, nyumba kubwa, pombe, wasichar na kadhalika. Izingatiwe kuwa marafiki wake wakubwa ni Raha na Pesa ambao kijazanda wanawakilisha mambo yaliyojazana kichwani mwake na kumpa kichaa.

Mategemeo ya Pambo baada ya kuhitimu elimu ya chuo kikuu ni kupata kazi ya madaraka itakayomwezesha kupata pesa nyingi, gari, wasichana na anasa za kila namna. Kwa bahati mbaya, mfumo wa jamii na hasa mfumo wa kiuchumi hauwaruhusu kabisa vijana kama hawa kupata maisha wayakamiayo.

3:6:3 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Kwa maoni yetu, Pambo ni mchezo ambao una mawazo na maudhui mazito sana hasa ukilinganishwa na michezo ya awali ya Muhando kama vile Hatia (1972), Tambueni Haki Zetu (1973), Heshima Yangu (1974) na Talaka Si Mke Wangu (1974). Kama tulivyosema hapo awali, katika tamthilia hii, Muhando anajadili jukumu la wasomi katika nchi yake na Afrika kwa jumla hasa baada ya nchi hizo kujirejeshea uhuru. Ibainike kwamba huu ni mchezo ambao Muhando aliuandika takriban miaka 14 baada ya Tanzania kujipatia uhuru na takriban miaka 8 baada ya Azimio la Arusha. Mfumo ulioanzishwa na Azimio hili haukuwaruhusu watu binafsi kujilimbikizia mali. Hali hii imewakilishwa katika maandishi mengi kutoka Tanzania ya wakati huo. Maandishi kama vile Mashetani (E. Hussein 1971), Dunia Uwanja wa Fujo na Gamba la Nyoka (E. Kezilahabi 1974 na 1979) yanatuonyesha miparuzano na migongano iliyokuwepo baina ya watu (Wasomi miongoni mwao) waliotaka kujilimbikizia mali na jamii zao. Hata hivyo, swala tunalojishughulisha nalo ni jinsi Muhando anavyowawakilisha wanawake katika mgongano huu.

Mwanamke katika tamthilia hii amesawiriwa kama mtu mchoyo na mpenda anasa ambaye hawezi kushiriki katika mapenzi ya dhati bali katika mapenzi ya chati tu. Katika muktadha huu, ameonyeshwa kama mtu mlaghai ambaye anamfuata na kumnyonya mwanaume kile alichonacho na kiishapo yu tayari kumwonyesha kisogo. Taswira hii ya mwanamke inaendelezwa kupitia kwa Maua; mhusika mkuu wa kike katika tamthilia hii ambaye pia

amepewa jina la kimajazi. Maua ni mpenda pesa na raha na anawafuata wanaume kwa kile tu anachoweza kuchuma kutoka kwao. Kama msemu wendavyo, anamfuata nyuki ili ale asali. Taswira hii inajitokeza kupitia kwa uhusiano wake na Pambo. Uhusiano huu umejengeka juu ya ahadi za raha na anasa alizoahidiwa na Pambo. Pambo amemwahidi kuwa atamnunulia gari, friji, rediogramu na kumjengea nyumba nzuri. Kadiri muda upitavyo ndivyo Maua anapotambua kuwa Pambo hataweza wala hafanyi juhudi zozote kuzitimiza ahadi hizi alizompa. Imefika hata kiwango cha kuaibika mbele ya marafiki zake anapokosa kinywaji cha kuwaandalia. Hayuko tayari kuivumilia hali hii na yu radhi kuondoka wakati wowote na kuchumbiana na 'mvulana' ambaye atamtimizia mahitaji yake. Anamwambia Pambo:-

Basi nakwambia nimechoka kweli;  
nimechoka na wewe. Kila siku unajidai  
utanunua gari, lakini gari lenyewe silioni ...  
Tangu umeanza kufanya kazi miaka sita sasa ...  
Hivyo hutaki twende sinema leo kama  
tulivyopanga ... kama huna hela sasa  
hivi toka ukazitafute ... Baba wewe  
aibu uliyonitia juzi! ... wageni wana-  
kuja wanakuta hamna hata chupa moja  
ya bia; hata soda nayo ... Niambie  
sasa hivi Pambo, wapi gari? Wapi nyumba?  
wapi friji? wapi rediogramu? wapi pesa?  
wapi pesa, wapi pesa? ... mimi na wewe  
basi Pambo ... (kur. 1-4).

Ili kuweza kukidhiwa mahitaji haya yake, lazima Maua ajinopoe na kujipamba ili ampendeze Pambo.

Taswira hii inaendelezwa pia kupitia kwa wahusika wa kindoto Suzie, Salome na Hadija. Wahusika hawa ambao tunakutana nao kupitia kwa mchezo-ndani-ya-mchezo ni wanawake ambao wanamfuata Pambo kwa sababu anawapeleka 'auti', kuwanu-

nulia nguo na viatu na kuwatembeza katika majumba ya starehe. Kama Maua, inawabidi pia wajipambe ili waweze kumpendeza Pambo.

Taswira hii inaenda sambamba na ile ya mwanamke kama chombo cha kutimizia ashiki za kiume na inaendelezwa kupitia wahusika wale wale katika uhusiano wao na Pambo. Pengine jambo hili linabainika wazi zaidi tunapouzingatia mwelekeo wa Pambo kwa wahusika hawa ambao unabainika kupitia kwa nyimbo anazoiimba:-

8

Pambo Pambo mkubwa mie  
Hakuna anayenizidi  
Wa wa wa ewaa

Wasichana kwa Pambo mie  
Tele tele tele  
Wa wa wa ewaa

Niingie baa Pambo mie  
wote rafiki wa Pambo  
Wa wa wa ewaa

Pambo hata gizani mie  
Nami asinitambue?  
Wa wa wa ewaa ( uk. 9).

Kwa Pambo, wanawake ni mojawapo ya viungo vya kuikamilisha raha yake. Wasichana kwake ni Maua ambayo lazima yachunwe yanapochipua. Ndiposa tunamwona akihusiana kimapenzi na wanawake wengi kama vile Maua, Wema, Suzie, Salome na Hadija kwa wakati mmoja huku akiwahadaa kwa kuwaita 'baby' na 'Good girl'. Wasichana hawa, isipokuwa Wema, wanaamini kuwa jukumu lao kubwa ni kumtumbuiza na kumfurahisha Pambo. Uchoyo na utashi wao, hasa wa Maua ni mojawapo ya mambo yanayomfanya Pambo kushikwa ni kichaa kwa sababu hawezi kutimiza mahitaji yao. Hadija kwa mfano anataka kupelekwa 'auti' Africana,

Salome anataka kupelekwa kuwaona Afro-70 ilhali Suzie anataka anunuliwe viatu na kupelekwa 'auti' akaone sinema ya 'The Godfathers'. Kwa kuwaita 'baby' na 'Good girl' Pambo anafanikiwa kuwahadaa wasichana hawa kuwa anawapenda. Hii ni mbinu inayotumiwa na wanaume wengi kuwahadaa wanawake ili wajifurahishe kwa miili yao. Jina 'baby' linaashiria ule ulainifu wa ngozi ambao huashiria mwanamke kama kiumbe cha kutamaniwa na kumezewa mate. Mbali na kuwa taswira hii inamdhalilisha mwanamke, wakati huo huo inaendeleza ile hali ambapo wanaume hupenda kutembea na wanawake wabichi. Katika mkabala huu, wanawake wanalazimika kutumia madawa ya kubambua ngozi ili waonekane wachanga.

Mwanamke pia anajitokeza kama kiumbe ambaye hawezi kujieleza wala kujiendeleza pasipo kujifungamanisha na wanaume. Katika muktadha huu, hitilafu yoyote itokeayo katika maisha ya mwanaume inalaumiwa kwa mwanamke. Kwa mfano Wema na Mama Doto wanamlaumu Maua kwa kichaa cha Pambo huku wakimsuta kuwa ama amemloga au amemtupia jini. Kwa sababu lazima mwanamke afungamanishwe na mwanaume ndipo aweze kujieleza, Muhando anamfungamanisha mwanamke aliyemkusudia kuwa kielelezo cha mwanamke mwema na Pambo. Wema, ambaye ameshehenezwa sifa za uzuri anaishilia kumpigania Pambo.

### 3:6:4 MTAZAMO WA MWANDISHI

Wahakiki wengi ambao wameuchambua usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Penina Muhando wameukwepa mchezo wa Pambo kwa madai kuwa mchezo huu haujihusishi moja kwa moja na maswala ya kike ( taz. Matteru 1987 na Chesaina 1987).

Pengine sababu halisi inayowafanya kuukwepa mchezo huu ni kwamba Pambo ni mojawapo ya michezo ya mwandishi huyu ambayo inaendeleza taswira mbaya sana za wanawake pasipo kupendekeza suluhisho lolote kwa tatizo hili.

Kama tulivyoonyesha hapo awali, mojawapo ya taswira za mwanamke zinazojitokeza katika tamthilia hii ni ile ya mwanamke kama mtu mchoyo na mpenda anasa amfuataye mwanaume ili aweze kuchuma. Taswira hii, tulitaja, inaendelezwa kupitia kwa Maua, Wema, Suzie, Hadija na Salome. Kwa upande wa mwandishi hatuoni kukua kwa wahusika hawa wala hatuoni wanawake hawa wakijizatiti na kujikomboa kutokana na hali hii. Kile wanachoishilia kufanya ni kutukanana, kupigana na kuondoleana heshima ili kila mmoja wao aihifadhi nafasi yake.

Tazama kwa mfano jinsi Maua na Wema wanavyotukanana:-

MAUA: Lione! Mshenzi mkubwa. Kwanza una uzuri gani wa kumvutia Pambo? Shika adabu zako.

...

Mbwa wee! kumbe ndiyo wewe unayeni-vurugia mambo! mbwa wee!

WEMA: (Anaanza kushikwa na hasira) Unanitukania nini? Kwanza wewe nani?

MAUA: (Anamgeza) 'Kwanza wewe nani?' Mbwa wee! Mimi Maua. Nione, Maua kweli. Na hata ufanye nini, huwezi kushinda. Huna uzuri wowote. Afadhali nguruwe.

WEMA: Kumbe wewe ndiye Maua. Mimi sitaki ugomvi, lakini nakwambia usinitukane.

MAUA: Huna adabu. Pambo ananifanyia visa. Kumbe sababu ya wewe. Pambo hana hela za kwenda sinema, hana hela za kununua gari - hata pombe hanunui - Kumbe wewe ndiye unayemvuruga? Wewe ndiye unayemaliza pesa zetu. Umefuata nini hapa? Nyama, wee!

WEMA: (Kapandwa na hasira) Nyama mwenyewe; Shetani mkubwa. Haikutosha kumfilisi Pambo mpaka umloge na kumloga.

MAUA: Wee unatoka wapi lakini? Unadhani mtu akipendwa ndiyo ameloga? Vipi unaona hupati pendu la Pambo unaanza kufikiria kuloga. Bure dada; uchawi wa mapenzi uzuri. Mradi huo uzuri huna, pumzika. Nakwambia utoke hapa ndani. Pambo hawezi kupenda lijitu kama wewe. Lione kwanza! Vinywele kama kupe, wameng'ang'ania kichwani. Hata shepu hauna. Unadhani Pambo anaweza kukupeleka auti lijitu kama wewe? Nyooo!

WEMA: (Amekasirika kabisa. Anasimama) Mwenyewe! Wewe unadhani manywele yako ya bandia ndiyo uzuri. Kwanza na miwanja hiyo, unaonekana kama nyani. Ungekuwa unajiamini mzuri usingehangaika na mawigi na mapodozi. Kazi yako ...

MAUA: Koma, nakwambia koma. Toka hapo mbwa wee!

...

Koma nyama wa porini! Kumbe kama si hela zake, wewe unafuata nini kwa Pambo. Si na wewe unataka upate Krimplin, unataka wigi. Kuona wenzio tunashaini, na wewe fyekafyeka unajileta kwa Pambo! Toka hapa kabla sijakupiga ...

WEMA: Wewe unaacha Pambo anapata kichaa (Anamrukia) ... Shetani! Mchawi wee!

Baada ya ugomvi huu baina ya Maua na Wema wahusika hawa wawili wanatoweka. Muhando hajawakuza wahusika hawa ili labda kutuonyesha mabadiliko yao kitabia ili waweze kuwakilish mwanamke anayeweza kuigwa. Kwa kumsawiri mwanamke namna hii, swali tunalolazimika kujiuliza ni kile anachokielekezea Muhando.

Lengo kuu la fasihi ni kuzindua fikra na mawazo ya binadamu kwa madhumuni ya kuleta mabadiliko yafaayo katika jamii (Kazungu 1984: viii). Kuhusu fasihi inayoendeleza taswira mbaya za wanawake pasipo kutuonyesha jinsi ambavyo anaweza kujitoka katika unyonge huu, Kazungu (1984: viii)

anazidi kutueleza:-

Kwa kuendelea kumsanifu mwanamke kwa sifa kama: mwenye shingo ya upanga, mwendo wa maringo ama kumfananisha na ndege au tunda kwa kusudi la kusifia uzuri wake tu, kumepotosha na kugubika ukweli wa maisha wanayoyaishi wanawake katika jamii nyingi za Kiswahili (au za kiafrika kwa jumla). Na kumeendeleza ile dhana kwamba wanawake ni viumbe wa kutazamwa na kusitaajabiwa kwa uzuri wao tu wala sio kama binadamu wenye akili na maarifa na wanaostahili haki sawa katika mahusiano yao na wanaume au hata wanawake wenzi wao. Basi fasihi inayoendeleza mambo kama haya ina nafasi gani katika jamii yetu ya kileo?

Maoni yetu ni kwamba Muhando katika Pambo haonekani kuyajali maslahi ya wanawake. Kwa kutofanya hivi, anaonekana kutokuwa na msimamo maalumu kuhusu swala la mwanamke katika jamii na jukumu analoweza kutekeleza nje ya yale majukumu ya kijadi aliyowekewa na jamii ambayo yanamdunisha.

Kama alivyofanya Muhando katika tamthilia nyingine tulizozichambua, wanawake anaotusanifia katika Pambo ni wanawake ambao hawajaelimika; ambao maisha yao yamezungukwa na kutawaliwa na wanaume na ambao wako kando ya jamii. Hatuambiwi kwa mfano kama Maua, Wema, Mama Doto, Suzie, Salome au Hadija na wanawake wengine katika mchezo huu wamepata elimu ya kiwango chochote kile. Mwandishi haonekani kutoa malalamiko yo yote dhidi ya hali hii katika Pambo. Hatuonyeshi hata kidogo chanzo cha tabia za wasichana kama kina Maua. Je, ni kweli kwamba katika jamii anayoizungumzia Muhando wanawake wote hawajaelimika na jukumu lao kubwa na kutia ladha maisha ya wanaume kama wafanyavyo kina Suzie, Hadija, Salome, Maua na Wema pasipo

kujali? Ni kweli kwamba elimu ya kimagharibi iliyolenga kumkengeusha mwafrica haijamwathiri mwanamke kwa njia yoyote kama tunavyoonyeshwa na Muhando? Ni kweli kwamba wanawake wanajivunia maisha ya 'akina pangu pakavu patie mchuzi' kama afanyavyo Maua?

Jawabu la maswala haya linaweza kupatikana kwa kuangalia jukumu la wanawake kama lilivyosanifiwa na waandishi wengineo wa kiafrika. Tukiwachukua wahusika kama vile Penda, NDeye Touti na Adjibiji wa God's Bits of Wood, kwa mfano, tutaona jinsi ambavyo Sembene Ousmane amewafinyaga wahusika wake wa kike kwa lengo la kuashiria jukumu na nafasi ya mwanamke katika Afrika huru ambalo ni tofauti na lile atekelezalo katika jamii kongwe. Adjibidji kwa mfano ni kielelezo cha kizazi kipya cha wanawake ambao hawatakubali utumwa wa wanawake wa kijadi hasa akilinganishwa na mamake Assitan. Penda na NDeye Touti kwa upande mwingine ni wanawake ambao wameenda kinyume cha matarajio ya jamii; kila mmoja kwa njia yake. Hata hivyo, mwandishi anatuonyesha jinsi wanavyobadilika na kuanza kutekeleza majukumu muhimu katika harakati za ukombozi wa jamii yao. Sawia na wanaume, wanawake wanapewa jukumu kubwa katika harakati za kuupiga vita utawala wa kikoloni. Mabadiliko yanayotokea katika wanawake hawa yanapatikana katika maneno ya

Mama Sofi:-

utaona - wanaume watatushauri kabla hawajafanya mgomo mwingine. Kabla ya haya, walikuwa wakifikiri wanaumiliki ulimwengu eti kwa sababu walitulisha, na sasa ni wanawake wanaowalisha. (Ousmane 1962:72).

Hata hivyo, kuna tatizo hapa kuhusu jinsi Ousmane anavyoyaona mahusiano baina ya wanaume na wanawake katika jamii hii mpya. Suluhisho analolipendekeza Ousmane halileti afueni kwa wanawake katika hali halisi. Badala yake, linawarudisha wanawake pale pale walipokuwa. Kwa mfano; ijapokuwa baada ya mgomo huu wameanza kuwa na mwamko wa kijamii na kisiasa, Ousmane anawarudisha nyumbani kutekeleza majukumu yale yale waliyokuwa wakitekeleza kabla ya mgomo. Katika hali halisi, uwezo wa kiuchumi bado unamilikiwa na wanaume. Kwa maoni yetu, wanawake bado wataendelea kuwategemea wanaume. Maswali ya kujiuliza ni; Je, kazi wanazozifanya nyumbani zitakuwa na manufaa yoyote ya kiuchumi Kwao? Je, kuna usawa wa kiuana baina ya wanaume na wanawake katika jamii inayotokea baada ya mgomo huu? Hatuamini kwamba usawa huu upo. [ Ousmane ni mwandishi wa kiume, na ijapokuwa anaamini kwa dhati kuwa lazima kuwepo na mapinduzi ya kijamii yatakayoleta afueni kwa wadhulumiwa wote, anakumbwa na tashwishi inayowakumba waandishi wengi wa kiume wanapoandika juu ya wanawake.

Pengine tatizo la usawiri wa wahusika wa Muhando linatokana na hali ya kutokuwa na itikadi maalumu anapoandika; hasa akilinganishwa na mwandishi kama vile Sembene Ousmane ambaye kazi zake zimejikita katika misingi ya itikadi ya Kimarx.

Kwa kuikamilisha sehemu hii, hatuna budi kuangalia suluhisho analolitoa mwandishi ili kuisafisha jamii yake. Kama tulivyosema hapo awali, Muhando ni mwandishi ambaye huji-chukulia kuwa jukumu la kuionyesha jamii pale ambapo jawabu

au suluhisho la matatizo yanayoikumba jamii linapatikana. Katika Pambo, Muhando anapendekeza kwamba jamii ijaribu kuwaelewa vijana kama Pambo. Hii ndiyo sababu mganga anasisitiza kwamba lazima waimbe wimbo wa akina Pambo. Anaonelea kuwa ni lazima watu katika jamii washirikiane ili kuwaokoa watoto wao. Hili anaonelea linawezekana kupitia kwa kuwaelimisha vijana upya kama inavyodhihirika katika wimbo wa vikundi:-

KIKUNDI A: (Kwa sauti kubwa) Basi gari la Pambo  
gari la Pambo  
Modeli nchini hakuna  
Tonesha gari ya mkubwa  
usingizi fo fo fooo  
lakini gari Yangu (mkazo)  
Nyie wote hakuna kupanda (mkazo zaidi)  
Pambo! Pambo! Pambo!

KIKUNDI B: (Mganga naye anasema kwa nguvu)  
Nitake gari anasa ee  
Lakini nini Pambo mie la nini  
Ninunue gari mie  
Faida apate mzungu  
Nizurure mitaani Pambo - Pambo gani  
Bibi chakula hapati  
Wa wa wa ewaa.

Mganga katika mchezo huu, kwa maoni yetu, ni kielelezo cha falsafa na itikadi ya Azimio la Arusha. La muhimu kwetu ni kwamba jukumu hili limekabidhiwa mwanaume na wanawake hawajashirikishwa. Kwa mfano hatumwoni mamake Raha wala mamake Pesa. Tunawaona tu baba zao wakishirikiana na mganga ili kumponya Pambo; kijazanda kuisafisha jamii kutokana na uozo unaoletwa na watu wenye nia kama za akina Pambo. / Kwa mara nyingine tena, mwandishi analiweka jukumu la kuikosoa jamii mikononi mwa wanaume na kuwaweka wanawake kando / Kwa kufanya hivi, mwandishi anawanyima wanawake nafasi ya kushiriki katika harakati za kuikosoa na kuiendeleza jamii yake. Wanawake

wanabaki kuwa watazamaji tu katika sarakasi hii. Kwa kufanya hivi, mwandishi anaendeleza imani na itikadi kuwa mahali pa mwanamke ni nyumbani na hasa jikoni, mwanamke ni Pambo kwa mwanaume na kwamba mwanaume ndiye mtendaji; mwanamke ni mpokezi tu.

3:6:5 K I M A L I Z I O

Katika kumchambua Angelina Chogo katika Kortini Mtu Huyu na Penina Muhando katika Hatia na Pambo, imebainika kuwa waandishi hawa wawili wanaandika katika kipindi maalumu cha historia ya jamii yao na wanaonyesha kuunga mkono siasa ya ujamaa ya nchi yao iliyoletwa na Azimio la Arusha la 1967. Pia, imebainika kuwa waandishi hawa hawana msimamo thabiti kuhusu jukumu na nafasi ya mwanamke katika jamii zao ndiposa wanatusawiria wahusika ambao hawawezi kuigwa.

Tumeona kuwa jambo hili linatokana na waandishi kutokuwa na itikadi maalumu inayowaongoza katika uandishi wao. Kwa kukosa itikadi, wameishilia kuliunga mkono Azimio la Arusha kikasuku pasipo kuonyesha wanaelewa kuwa kinadharia lililenga kuleta usawa hasa wa kiuchumi miongoni mwa watu wote; wanaume kwa wanawake, lakini katika hali halisi, lengo hili halikufanikiwa.

Pia, tumesema kuwa kwa kukosa itikadi maalumu, waandishi hawa wameshindwa kuchimba misingi halisi sio tu ya mata-tizo wanayoyashughulikia bali pia misingi ya tatizo la mwanamke. Kwa sababu hii, taswira za mwanamke zinazojengeka katika kazi zao zina misingi yake katika utamaduni mkongwe na badala ya

kuashiria kumkomboa mwanamke zinamrudisha katika utamaduni ule ule ambapo hana nafasi ya kujikuza na kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa sababu yuko chini ya utawala wa mwanaume. Kwa sababu hii, tumesema waandishi hawa wako katika njia-panda.

4:0

SURA YA NNE

PENINA MUHANDO: 1982 - 1984

4:1 U T A N G U L I Z I

Katika sura hii, tutajishughulisha na tamthilia mbili za Penina Muhando ambazo aliziandika kati ya 1982 na 1984. Tamthilia hizi ni Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984). Kazi hizi, kwa maoni yetu, zinawakilisha mabadiliko ya kimtazamo kwa upande wa mwandishi sio tu katika maswala yanayohusu siasa na uchumi wa nchi yake bali pia maswala yanayohusu wanawake.

Kipindi hiki pia kina umuhimu wa kihistoria. Wakati huu nchi ya Tanzania ilikuwa inakabiliwa na matatizo mengi na magumu ya kiuchumi; hasa baada ya vita vya Kagera vya mwaka wa 1978-1979. Katika vita hivyo, jeshi la Tanzania lilijiunga na jeshi la kichini chini la aliyekuwa Rais wa zamani wa Uganda Dkt. Milton Obote katika juhudi za kumng'oa mamlakani nduli Idi Amin Dada ambaye alishika hatamu za uongozi mnamo mwaka wa 1971 baada ya kuipindua serikali ya Dkt. Obote.

Ni katika kipindi hiki hiki ambapo bei za mafuta zilianza kuongezeka na kufikia kiwango ambacho nchi nyingi za kiafrika na 'ulimwengu wa tatu', ambazo hazina mafuta yao, hazingeweza kukigharamia kwa pato haba la pesa za kigeni lililotokana na mazao kama vile kahawa na chai. Ubepari wa kimataifa nao ulikuwa unazidi kupanua mirija yake na chumi za nchi nyingi zenye siasa ya mrembo wa kushoto, zikiwemo nchi kama vile Tanzania na nchi za Ulaya Mashariki, zilianza kuzorota.

Siasa ya ujamaa ambayo ilikuwa imeendelezwa kwa zaidi ya miaka kumi nchini Tanzania ilikuwa imeanza kupigiwa maswali hasa kuhusiana na utekelezaji; watu wa kawaida walikuwa wamehamishwa na kupelekwa kwenye vijiji vya ujamaa; wakati mwingine kwa nguvu, ilhali viongozi waliishi mijini na baadhi yao wakajilimbikizia mali kwa kutumia vibaya mali ya umma.

Tukio lingine muhimu katika kipindi hiki ni kwamba Umoja wa Mataifa ulikuwa umetangaza kipindi cha kuanzia 1975-1985 kuwa mwongo wa akina mama ulimwenguni kote. Kipindi hiki kilikuwa na maendeleo makubwa kwa maisha ya akina mama. Maisha yao yote yalikuwa yanapigiwa darubini katika ulimwengu wote kwa jumla. Penina Muhando aliombwa kuandika tamthilia ili kuushe-rehekea mwongo huu; ndiposa akaandika Nguzo Mama. Matukio haya yote yalikuwa na athari kubwa kwa maisha ya Watanzania na ni katika kipindi hiki ambapo Muhando aliandika tamthilia zake mbili tunazozichambua katika sura hii. Lengo letu kuu katika sura hii ni kuchambua usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia hizi ili kuona jinsi ambavyo Muhando anashughulikia na kuziwakilisha athari za matukio haya kwa maisha ya wanawake.

4:2 PENINA MUHANDO: NGUZO MAMA (1982).

4:2:1 HADITHI KWA UFUPI

Nguzo Mama ni tamthilia inayochambua matatizo yanayowakabili kina mama katika juhudi zao za kuendesha harakati hizi za kujikomboa. Matukio muhimu katika tamthilia hii yameumbika kuzunguka shughuli za kuinua nguzo-mama ambayo imetolewa na wahenga ili kuwatoa Wapatata mashakani. Mchezo unapoanza,

tutamwona kila mmoja wa wale mabibi akijaribu kuiinua nguzo-mama peke yake lakini anashindwa. La mgambo linapolia kuwatangazia watu wa Patata kuwa wamepewa nguzo-mama na wahenga kwa hivyo waje kuiinua, wanaume wanakataa kushiriki kwa sababu nguzo-mama ina jina la kike. Badala yake, wanarudi vitandani na kulala. Jambo hili haliwau moyo wanawake. Wanaamua kuiinua nguzo-mama peke yao. Hata hivyo, kunatokea migawanyiko baina yao. Kwa mfano, kuna mgogoro juu ya uongozi baina ya Bi. Nne na Bi. Nane. Bi. Nne ambaye ni mpenda makuu anakataa kusikiliza maoni na mawazo ya Bi. Nane kwa sababu anafikiri Bi. Nane anataka kumpokonya wadhifa wa uongozi wa kina mama.

Mambo yao ya kibinafsi pia yanawafanya kina mama wasiungane ili kuiinua nguzo-mama. Mwandishi anatuambia kupitia kwa Bi. Msimulizi:-

Huko mbele ya safari  
Zogo likatokea  
Huyu tufanye hivi  
Huyu tufanye vile  
Patata ikapamba moto  
Kila mtu akafanya lake  
Akiamini lile alifanyalo  
NGUZO-MAMA litaiinua (uk. 13).

Bi. Pili kwa mfano, anaamua kupika pombe ilhali wale wengine wanaamua kufuma vitambaa vya kupamba nyumba. Shughuli hizi zote hazifanikiwi. Haya yanapofanyika, wanawake wale wanakaa chini na kushauriana. Mwishowe wanaamua kuungana tena. Anasema Bi. Msimulizi:-

Vurugu zilipozidi  
Chini walikaa mashauri wakafanya  
Jamani umoja ni nguvu  
Utengano ni udhaifu

Twendeni sote pamoja  
Nguzo mama kuisimamisha  
Kwa nguvu zetu wenyewe  
Hata kwa jasho la damu  
Ndipo wakaivamia  
Hiyo yao NGUZO-MAMA  
Kazi wakaianza. (kur. 33-34).

Hata hivyo, juhudi hizi mpya za kuwaunganisha wanawake hazifanikiwi. Mambo yao ya kibinafsi yanawafanya waisahau nguzo-mama. Bi. Moja, kwa mfano, anaacha kuiinua ili amfuate mumewe ampe pesa za kununua kanga asiachwe na 'meli hii mpya.' Bi. Pili kwa upande wake anaacha kuiivuta kamba na kwenda kumshughulikia mwanawe anayelia, Bi. Sita anaacha ili kumfuata Maganga (mumewe Bi. Tano) na hili linamfanya Bi. Tano pia kuacha kuiivuta kamba ili kumpigania mumewe. Bi. Tatu anaondoka anapoiana Volvo ya mumewe ili waende wakajitayarisha wahudhurie sherehe ilhali Bi. Saba anaacha ili kukinga vitu vyake vya mwisho visichukuliwe na kaka za mumewe baada ya mumewe kufa. Kiongozi wao Bi. Nne naye anaondoka ili kuhudhuria mkutano wa kamati ambapo yeye ndiye mwenyekiti. Mwishowe anabaki Bi. Nane peke yake lakini baada ya kuvuta kidogo anaona kuwa anapoteza nguvu zake bure.

Mwishowe, La mgambo linapotangaza kuwa wamepewa siku tatu zaidi kuiinua nguzo-mama lau sivyo itachukuliwa na kupeleleka mahali pengine, wale kina mama wanajumuika tena kuiinua. Hata hivyo, hawafanikiwi katika siku za mwanzo mbili kwa kutotumia maarifa. Kwa mfano wanapuuza ushauri wa busara wa Bi. Nane. Mchezo unapoisha, tunaamkia siku ya tatu ambayo ndio siku ya mwisho waliyopewa.

4:2:2 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Katika tamthilia hii, Muhando anajaribu kutuonyesha matatizo na vikwazo ambavyo vinawakumba wanawake wa kiafrika katika jitihada na harakati zao za ukombozi. Muhando anafanya hivi kwa kuwasawiri wahusika wote katika tamthilia hii kwa njia mbili. Kwanza, anawasawiri wahusika kijazanda na pili, anawasawiri wahusika wake kiaina. Hapa, tunamaanisha kuwa kila mhusika binafsi amesawiriwa kuwakilisha tabaka, sifa na tabia fulani za wanawake wa namna mbalimbali katika jamii. Kama tulivyosema hapo awali, maudhui muhimu katika mchezo huu yamejengeka kupitia kwa harakati za kuinua nguzo-mama ambayo imetolewa na wahenga kwa watu wa Patata. Kwa kutumia jazanda hii, Muhando anatuonyesha umuhimu wa wanawake katika jamii. Wanawake ndio nguzo na msingi wa jamii; ndiposa tunu hii kutoka kwa wahenga ikaitwa 'NGUZO - MAMA.'

Hata hivyo, umuhimu wao hautambuliwi katika jamii hii. Kupitia kwa Bi. Msimulizi, Muhando anatudhihirishia hali hii. Bi. Msimulizi anawambia:-

... Kijiji kilistawi tena kilistawi  
Watu wake wema wa roho  
Wakazaliana, wakaongezeka  
Patata ikasifika, pande zote za dunia  
Kwa nje iling'ara  
Kwa vicheko vya wake wana  
Wengi wakautamani Upatata kuupata.

Lakini Patata wake wana  
Vilema vyao walivijua  
Vurugu na matata Patata vikajikita  
Maendeleo Patata yakawa hatarini  
Kwani wabeba wana vibaya walinyanyasika  
Wakaonekana si watu  
Igawa jamii waliikuza  
Vipi mambo hivyo yakawa

Hakuna aliyejua  
Ila hapo kwao Patata  
Vurugu zilizidia  
Maendeleo ya Patata  
Hatarini yakaingia  
Siku moja asubuhi na mapema  
Wapatata usingizi wakiupiga  
Likalia la Mgambo (uk. 4).

Hapa, kupitia kwa Bi. Msimulizi, Muhando anatwambia kuwa ijapokuwa nchi hii imestawi, kwa kuwapuuza na kutowashirikisha wanawake maendeleo ya Patata yako hatarini. Hivi ni sawa na kusema kuwa pasipo mchango wa wanawake, jamii haiwezi kupata maendeleo.

Kupitia jazanda hii ya Nguzo-mama, Muhando anatuonyesha nyanja mbalimbali za maendeleo ya kitaifa ambazo wanawake huchangia. Kwa mfano, wanawake ndio wanaoleta kizazi kipya katika jamii. Kielelezo kizuri cha jukumu hili ni Bi. Pili ambaye anakumbana na dhiki na taabu za kila namna ili kuwakimu wanawe. Hata hivyo, kutokana na jukumu hili la wanawake kama wazazi, wanaume wanawadharau:-

BI. MSIMULIZI: ... lakini baba wa wao wana  
macho walitumbua  
Vicheko wakaangua  
"Waoneni wapumbavu" wengine walisema  
"Tangu lini wabeba wana kuwa watu  
Ndipo leo ya pili kuwa?" (uk.46).

Wanawake wa Patata wananyanyaswa. Hawaonekani wala kuchukuliwa kuwa binadamu. Hata hivyo, swali la La Mgambo linatuonyesha umuhimu wa majukumu haya wanayoyatekeleza:-

LA MGAMBO: ...matokeo yake mwajua  
wote Wapata NGUZO MAMA KUKOSA  
Kwani bila NGUZO MAMA  
Nyumba gani ilisimama?

Yatupasa pia tuzingatie uana wa nguzo mama. Nguzo mama katika tamthilia hii imepewa uana wa kike. Hii ni njia moja Muhando anayotumia kuonyesha umuhimu wa wanawake katika jamii tofauti na mielekeo ya jamii ambayo inaudhalilisha na kuudunisha uke kama inavyoonekana kupitia kwa wanaume ambao wanapotambua kuwa nguzo mama ni ya kike, wanarudi vitandani na kulala eti kwa sababu nguzo hii imepewa jina la 'nguzo mama' ambalo ni la kike. Hii ni kinyume na yale tunayoambiwa na La Mgambo kuwa nguzo mama imeletwa ili kuwatoa Wapatata mashakani. Anasema:

LA MGAMBO: ...Nguzo mama tumejipatia  
Kututoa mashakani  
Amkeni Wapatata  
Wahenga wameamua  
Nguzo mama kuwapatia  
Matatani kuwaondoa  
Basi hima amkeni  
Nguzo mama simamisheni  
Leo leo sasa hivi  
Mashakani tuondoke  
Maendeleo tujipatie...(kur. 4-5).

Muhando pia ametumia jazanda ya Nguzo mama kutubainishia baadhi ya matatizo yanayowakumba wanawake katika juhudi zao za kujikomboa kama wanawake. Kupitia juhudi za wanawake hawa za kuinua nguzo mama na vikwazo vinavyowakwaza, Muhando anaonyesha kuwa tatizo kubwa miongoni mwa wanawake ni la mielekeo baina yao wenyewe, mielekeo ya wanaume dhidi yao pamoja na kutokuwa na umoja miongoni mwao. Kupitia kwa mhusika Chizi ambaye ndiye hasa sauti ya mwandishi katika tamthilia hii; tunaambiwa:-

CHIZI: ...labda tuite njaa  
Kama hii inayoniama  
Naiona hivi hivi  
Njaa kamwe hainiishi  
Wananambia ni mvivu  
Lakini si langu kosa  
Nilifunzwa kuzurua  
Tangu ziwani kwa mama  
Tuseme hii ni njia iliyoingia Patata  
Njaa ya kukosa umoja  
Kukose ushirikiano  
Kuoneana na wivu na uzembe kuzidia(kur. 31-32).

Kiaina, wanawake katika tamthilia hii wamesawiriwa hivi kwamba kila mhusika anawakilisha tabaka lake na watu wa aina yake kama tulivyotaja. Kwa mfano Bi. Nne, ambaye ni kiongozi, anawakilisha viongozi wa aina yake katika jamii ambao huchukulia mawazo ya busara kutoka kwa wengine kama tisho kwa uongozi wao. Kwa njia hii, watu ambao wangechangia katika maendeleo ya jamii wananyimwa nafasi hiyo. Hili linafanywa kwa kutumia hila kama zile anazotumia bibi huyu dhidi ya Bi. Nane. Bi. Nane ambaye anawakilisha wasomi katika jamii ana mawazo yenye busara na umahiri na ambayo yakizingatiwa nguzo mama inaweza kuinuliwa kwa urahisi. Hata hivyo, Bi. Nane hayuko tayari kuyapokea. Anafanya njama na mwenyekiti wa kamati ya mashauri ili kumshtaki na kumhukumu na kwa njia hii awe ameondolewa ili asiwe tisho tena kwa uongozi wake. Kwa njia hii, wanawake hawa wawili wanawakilisha mikinzano iliyopo baina ya viongozi kwa upande mmoja na wasomi kwa upande mwingi.

Mitafaruku baina ya Bi. Tano na Bi. Sita pia ni kielelezo cha jinsi wanawake wanavyowaachia wanaume kuingilia umoja wao na kuwavuruga. Bi. Sita ni malaya na anawakilisha wanawake ambao, ili kutimiza ashiki zao, wanawafuata wanaume wa wanawake wenzao na kwa njia hii kuwafanya wasishiriki

kikamilifu katika juhudi za kujiendeleza na kujikomboa.

Mhusika huyu ametumiwa kuonyesha jinsi ambavyo wanawake wanaa-  
ngukia kwenye hila za wanaume na kuwafanya wasahau wajibu wao  
katika jamii. Hata Chizi hana maneno mwafaka ya kumwelezea  
Bi. Sita. Anasema:-

CHIZI: ...Sitaki kusimulia  
nisije anza kulia (uk. 54).

Bi. Moja kwa upande wake anawakilisha wanawake ambao,  
pasipo sababu maalumu; mathalani kwa kutaka kufuata mitindo  
mipya ya mavezi na urembo wanajidhalilisha mbele ya wanaume na  
kuusahau wajibu wao. Anapoziona kanga mpya, anaacha juhudi za  
kuinua nguzo mama na kwenda kumgombeza mumewe amnunulie zile  
kanga. Pengine Bi. Pili ndiye kielelezo bora zaidi cha jinsi  
mwanamke anavyoupa kisogo wajibu wake katika juhudi za kujiko-  
mboa na kuliendeleza taifa lake na badala yake kujidhalilisha  
mbele ya mwanaume ambaye hata hana haja naye. Bi. Pili anazia-  
cha jitihada za kuiinua nguzo mama na kwenda kuanza kupika  
pombe. Hata hivyo, pesa azipatazo zote zinachukuliwa na mumewe  
Bwana Sudi ambaye anaenda kulewa kwingineko. Juu ya hayo,  
mapigo kwake hayaishi. Hata hivyo, hafanyi juhudi zozote  
kujikomboa kutokana na maonevu haya. Nyumbani kwake anakuwa  
ni mtumwa kwa mumewe kama inavyodhihirika katika dondoo  
lifuatalo:

SUDI: Ulikuwa wapi saa zote hizi? Mimi  
nimekuja zamani hapa, mtoto analia  
tu, analia tu; sijui wewe uko wapi.

BI. PILI: Jamani kwani umeshindwa nini  
Kumbembeleza?

SUDI: Nani ambembeleze, mtoto ana njaa

BI.PILI: Mbona chakula chake kipo kwa nini hukumpa?

SUDI: Wewe una kazi gani. Kwanza lete chakula upesi mimi nina njaa (Bi. Pili analeta chakula). Ile nguo yangu umekwisha fua? Ilete hapa nataka kuivaa niende kutembea.

BI.PILI: Haijakauka.

SUDI: Eee! Haijakauka tangu asubuhi?

BI.PILI: Nimeifua mchana huu. Asubuhi si nilidamkia shambani. Kurudi shambani kwanza nikapikia watoto, maji hakuna, nikaenda kuyachukua.

SUDI: Kelele! Sasa mimi nitavaa nini. Utaikausha kwa moto hiyo nakwambia. Mimi nataka kurudi nilikotoka nimeacha pombe kafiri, Unataka wenzangu waimalize? Kausha hiyo kabla sijakupiga (Bi. Pili anaondoka). Lete na maji ya kunywa. (uk. 36).

Bi. Pili anafanya kazi kama punda wa dobi lakini anahiari kutumikishwa. Mwandishi anawakashifu wanawake wanaoukubali udhaifu wa namna hii kupitia kwa Chizi:-

CHIZI: ...Siku moja nitamwuliza Bwana Sudi  
Dawa gani aliyompa Bi. Pili  
Ili na mie nikabahatika  
Mke kujipatia awe kama Bi. Pili  
Ambaye taabu yote atakubali  
Watoto anizalie na pia anilelee...(uk. 49).

Labda wanawake kama Bi. Tatu ndio waliokubali unyonge zaidi ya Bi. Pili. Bi. Tatu anajidhalilisha kwa sababu ya pato analolichuma kutoka kwa mumewe. Aionapo tu Volvo ya mumewe ambaye ni mwanasiasa juhudi za kuiinua nguzo mama anaziacha.

Msichana ambaye ni mwanamke wa umri mdogo ni mwakiliishi wa kizazi kichanga ambacho kinalemazwa akili na kuzongwazongwa na mikinzano baina ya wanawake wenyewe kwa wenyewe kiasi

kwamba hakijui ni lipi la kuchagua na kwa njia hii harakati za ukombozi wa kizazi cha kesho zinatatizika. Pindi aingiapo, kila mmoja wa wale wanawake anamwita kwenda upande wake:-

SAUTI-BI.MOJA: Wewe njoo huku!

SAUTI-BI.PILI: Njoo huku njoo!

SAUTI-BI.TATU: Huku wewe husikii!

SAUTI-BI.NNE: Njoo, njoo upesi!

SAUTI-BI.TANO: Njoo huku, huku!

SAUTI-BI.SITA: Kimbia, njoo huku!

SAUTI-BI.SABA: Wewe mtoto husikii! Njoo huku (uk.10).

Jambo la mwisho ambalo tungenda kutaja katika sehemu hii ni kwamba kwa kutowapa majina maalumu wahusika hawa, Muhando anafaulu kutusawiria wahusika ambao wanawakilisha kwa njia mufti kabisa tabaka na aina mbalimbali za wanawake na tabia zao katika jamii kama tulivyotaja hapo awali.

#### 4:2:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Nguzo Mama ni tamthilia ambayo ni ya kisiasa.

Tamthilia hii inawakilisha hatua muhimu, kwa maoni yatu, katika kukua kifalsafa na kimtazamo kwa upande wa mwandishi. Ni maoni yetu kuwa Muhando amevuka kiwango ambapo yeye kama mwandishi alikuwa akionelea Azimio la Arusha kama suluhisho kwa matatizo yote ya jamii yake; tatizo la mwanamke likiwemo. Hii ni tamthilia ambayo inaonyesha umuhimu wa mzinduko wa kisiasa kwa upande wa wanawake ndiposa mwandishi akachagua kulishughulikia tatizo hili kwa matazamo wa kike kwa kuwatumia wahusika wengi wa kike ambao wanajisimamia wenyewe kama wahusika binafsi na wale wa aina yao katika jamii.

Jazanda ya "nguzo mama" ambayo imepewa umuhimu mkubwa sana katika tamthilia hii imekusudiwa kuonyesha umuhimu wa wanawake katika maendeleo ya nchi zao. Jazanda hii inaashiria pia ukombozi wa wanawake ambao ni muhimu ikiwa wanawake watatekeleza wajibu wao kikamilifu katika jamii. Kwa kuitumia jazanda hii kama alivyoitumia, Muhando anadhamiria kuonyesha kwamba ukombozi wa wanawake utatokana na juhudi zao wenyewe.

Muhando anaitumia jazanda hii ambayo ni ya kawaida kwa njia isiyo ya kawaida sio tu kuonyesha matatizo yanayowakabili kina mama bali pia kuwahimiza wanawake waungane ili kujikomboa na zile itikadi za jamii zinazowafunga daima kuwa wanachini kwa wanaume. Kupitia kwa mhusika Chizi, Muhando anazisimanga itikadi hizi kwa kutufunulia mawazo na hofu za kila mmoja wa wanawake wote anaowaumba. Msimamo wake ni kwamba iwapo wanawake wanataka kujikomboa, ni lazima waungane. Ni lazima wakome kujishughulisha na mambo ambayo badala ya kuwakomboa kama wadhulumiwa yanawadhalilisha. Kwa mujibu wa nadharia yetu kama ilivyoielezwa na Eagleton (1986:171), lazima fasihi ya mrengo huu isaidie kukuza hisia za umoja miongoni mwa wanawake ambao kama wadhulumiwa wa kiuana, hawana budi kuungana na kupambana ili kujikomboa. Hakuwezi kupatikana ukombozi wowote wenye maana kwa binadamu pasipo kuwepo uhuru wa kijamii kwa wanawake na usawa baina ya wanaume na wanawake.

Kwa kutusawiria wahusika ambao wanawakilisha wanawake wa aina, hali na matabaka mbalimbali, Muhando anaonyesha kwa ufasaha mkubwa kuwa wanawake wote, kama kundi la kijamii, ni wadhulumiwa na wanaunda kundi ambalo linabaguliwa kama kundi.

Papo hapo, wanachama wa kundi hili wanaishi kwa urafiki zaidi na wale wanaowadhulumu kuliko jinsi wanavyoishi wao kwa wao.

Msimamo wake kama unavyoelezwa na Bi. Nane ni kwamba katika harakati zao, ni lazima wawashirikishe wanaume. Katika kufanya hivi, wanaume wasishirikishwe kama wakubwa wao bali kama binadamu sawa. Nguzo mama, yaani ukombozi wa wanawake, una manufaa kwa wote. Msimamo wa mwandishi kama unavyojitokeza hapa ni kwamba lazima kila mwanajamii, awe mwanaume au mwanamke, apewe nafasi ya kutoa mchango wake kwa maendeleo ya taifa pasipo ubaguzi wowote.

Jambo lingine ambalo haliwezi kupuuzwa ni nafasi Muhando anayowapa wanawake kama wasanii katika jamii zao. Ni muhimu kuzingatia kuwa msimulizi katika tamthilia hii ni mwanamke kwa jina Bi. Msimulizi. Wanawake, kama wasanii walitekeleza majukumu muhimu katika jamii kongwe za kiafrika. Kama watambaji, waimbaji na walezi wa watoto, wanawake walihifadhi na kuupitisha utamaduni, maadili na amali za jamii zao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Muhando anatambua ukweli huu na kuusanifu vilivyo katika tamthilia hii.

Chizi, ambaye pia ni mwanamke, anatumiwa kama kielelezo cha jukumu la msanii katika jamii. Mhusika huyu amesanifiwa kama mhusika mwenye kichaa kichaa. Hii ni mbinu ya mwandishi ya kuweza kumbebesha jukumu alilombebesha. Aghalabu, wasanii wausemao ukweli pasipo kuficha chochote ndivyo wanavyochukuliwa na jamii ambayo haiko tayari kuwakubali. Si nadra kwao kuitwa wendawazimu. Muhando, kwa usanifu mkubwa anamtumia Chizi kuwahakiki wahusika wake wote. Kwa kuwasanifu wanawake hawa wawili,

Chizi na Bi. Msimulizi, jinsi alivyowasanifu, Muhandu anaonyesha nafasi ya kihistoria ambayo wanawake wasanii walikuwa wakishikilia na bado wanaendelea kushikilia kama jicho la jamii.

Hata hivyo; tatizo kubwa la mchezo huu ambalo linamfanya mwandishi kuonekana kuyumbayumba katika mtazamo wake ni jinsi unavyoishia. Ijapokuwa kutoka mwanzo Muhandu amesisitiza umuhimu wa wanawake katika jamii kwa kuitumia jazanda ambayo ni taashira ya umuhimu huu; ijapokuwa kutoka mwanzoni amesisitiza haja ya wanawake kuungana pamoja na kuupigania uhuru wao; ijapokuwa ameonyesha vikwazo vinavyowazuia wanawake kuungana ili kutetea maslahi yao katika jamii, muungano anaoupendekeza haujapatikana mwishoni mwa mchezo. Bado wanawake wanaendelea kuzongwazongwa na mikinzano baina yao ambayo haisaidii kuleta ukombozi. Hata ingawa mwishoni mwa mchezo ni wazi kwamba kuna mwamko miongoni mwa wanawake, mwandishi anaonekana kutokuwa na matumaini makubwa. Mchezo unamalizika hivi:-

BI. MSIMULIZI: Kwa vile Chizi kakimbia  
Hadithi tamalizia

Wakainua, wakainua,  
Siku ya kwanza ikapita  
NGUZO MAMA Pale pale

Wakainua, wakainua,  
Usiku na mchana  
Siku ya pili ikapita  
NGUZO MAMA Pale pale

Sasa leo ni siku ya tatu  
(Kwa hadhira) Niendelee, Nisiendelee  
Niendelee, Nisiendelee  
( Kimya )

HADITHI YANGU IMEKWISHA

Mkarara: Nguzo mama, Nguzo mama  
Tukupambeje Maua  
Tukupambeje Maua.

Kimalizio hiki kinaonyesha matumaini madogo sana kwa upande wa mwandishi. Haina hakika kuwa mbinu zinazopendekezwa na Bi. Nane zitatiliwa maanani kwani ukinzani bado unaendelea baina yake na Bi. Nne. Hii ndiyo siku ya mwisho waliyopewa na wahenga wainue nguzo mama au wapokonywe. Hii kwetu ni ishara kuwa mwandishi bado hana msimamo thabiti kuhusu swala la mwanamke.

4:3 PENINA MUHANDO (1984): LINA UBANI

4:3:1 HADITHI KWA UFUPI.

'Lina Ubani ni tamthilia ya kisasa ambayo maudhui yake yamechipua kwenye matatizo ya kiuchumi na kijamii yaliyojitokeza baada ya vita vya kagera vya mwaka wa 1978-1979. Vurugu, migogoro na mikanganyiko inayosawiriwa katika tamthilia hii inadhihirisha wazi kwamba jamii hii ina uvundo' ...(taz. jalada la nyuma la kitabu hiki).

Penina Muhando katika mchezo huu anatumia mbinu za fasihi simulizi ili kuendeleza matukio muhimu katika mchezo huu. Kupitia kwa mtambaji, mwandishi anatupitisha katika vidato mbalimbali vinavyoyajenga maudhui ya tamthilia hii. Mchezo unapoanza, tunakutana na bibi, mamake Huila na Daudi. Daudi ameuawa katika vita dhidi ya Dyamini. Tukio hili linampokonya bibi mwanawe aliyemtegemea sana baada ya mwanawe mwingine kumwoa Mchusa. Bibi anaamini kuwa Wachusa si watu wazuri. Anamwambia Mota:-

Shangazi ya baba yako kaenda mjini, kaolewa na Mchusa. Basi mwanaume huyo! Mbogo si Mbogo, kifaru si kifaru! Merina akakonda akawa mifupa mitupu. Wakianza kumtukana, mume, mama, mkwe, wafi zake na shemeji zake wanasaidia kumpiga. Hili si kabila. Baba yako nilimwambia muoe melina. "Ooh! mie nimempenda huyu huyu (uk. 28).

Bibi hawezi kumsamehe Huila kwa kumwoa Mchusa. Katika mchezo mzima, analalamika kuhusu mabaya anayotendewa na Sara. Kifo cha Daudi kinamvuruga akili mpaka mwishowe anakufa.

Kwa upande mwingine, Huila, ambaye ni mtaalamu katika mambo ya nishati, anahudhuria mkutano Nairobi akiwa na mkuu wake kazini Bwana Zoeni. Katika mkutano huu wa kimataifa kuhusu nishati, Huila na Zoeni wana mpango wa nishati ambao walikuwa wameutayarisha kuuwasilisha kwa sababu unafaa nchi yao. Hata hivyo, Zoeni hazingatii haya na wanatofautiana vikali na Huila. Zoeni ambaye ndiye kiongozi wa ujumbe wa nchi yake anafanya mipango ya 'nuclear energy' na Bwana Robbins na pia mpango wa kupewa mafuta na mwarabu mmoja kwa bei rahisi pasipo kumshauri Huila. Hii ni kinyume kabisa na mpango ule waliokuwa wameutayarisha. Isitoshe, anafanya mpango na mjumbe Philipines ili kununua mbegu za Hanga ambazo huzalisha mafuta.

Huila analazimika kurudi nyumbani kabla mkutano hauja-isha anapopokea simu inayomwarifu kuwa ndugu yake Daudi amekufa na mama yake ni mgonjwa sana. Huko nyumbani, akiwa anajishughulisha na ugonjwa wa mamake, Zoeni anajitayarisha kuuwasilisha mpango wa "windmills" mbele ya kamati. Katika mpango huu, kila kijiji kinatakiwa kuwa na "windmill" na tayari wamepata "wind-

mills" mia nane. Huila, ambaye anauona mpango huu kuwa wa kipumbavu na usio na misingi ya kitaalamu, anatarisha mpango mwingine ambao una misingi ya kitaalamu. Anafanya mpango na katibu wa kamati ili kile kikao cha kamati kiahirishwe ili kumwezesha kupata muda wa kutosha kutayarisha mpango huu mpya. Hata hivyo, hafanikiwi kwani wakati huo huo mama yake anazidiwa na ugonjwa na kuifariki dunia.

Kupitia kwa mtambaji, mwandishi pia anatusimulia historia ya Tanzania kuanzia pale ambapo wananchi wanahamia katika vijiji vya ujamaa, vita vya kagera na athari zake na mwishowe mwamko wa kisiasa wa watu kutaka kubadilisha hali yao.

#### 4:3:2 KUSAWIRIWA KWA MWANAMKE

Mwanamke katika tamthilia hii amesawiriwa katika jukumu lake kama mzazi. Taswira hii inajitokeza kupitia kwa Bibi na Sara. Bibi ni mhusika ambaye tunaweza kumtazama katika viwango viwili. Kwanza, ni mhusika binafsi na pia kijazanda ni mwakilishi wa watu wa kawaida. Katika kiwango hiki cha pili, anakuwa ni kielelezo cha dhiki zinazowakumba watu wa kawaida, hasa wanawake katika vipindi mbalimbali vya historia ya Tanzania. Watu wa kawaida, wakiwemo wanawake, hawaziepuki athari zinazosababishwa na matukio na mabadiliko haya ya kijamii.

Taswira hii inaendelezwa kupitia kwa Bibi katika uhusiano wake na wanawe Daudi na Huila. Daudi, mwanawe mdogo, anauawa katika vita ambayo wananchi wa kawaida kama Bibi, hawajui inahusu nini. Anapoenda kuuliza habari zake, anaambiwa kuwa Daudi mwanawe ni shujaa. Hili ni jambo ambalo halielewi.

Kutokana na kifo cha mwanawe ambaye alikuwa anamtegemea, Bibi huyu anarukwa na akili. Dhiki na uchungu wa mama kwa kumpoteza mwanawe unawakilishwa kupitia kwake. Katika kiwango hiki, anatumiwa kuwakilisha dhiki na uchungu wa watu wa kawaida ambao walipoteza wanao katika vita hii ambayo sababu yake hawakuujua wala hawakushauriwa katika uamuzi wa kuianzisha. Katika kiwango kingine, Bibi anaiwakilisha nchi ya Tanzania ambayo kwa kujii-ngiza katika vita hii, kunatokea vurugu, migogoro na migongano ya kiuchumi na kijamii ambayo inatisha kuiangamiza nchi ile. Vita ya kagera inaiachia nchi hii njaa, ukosefu wa bidhaa muhimu na pupa ya kujilimbikizia mali miongoni mwa viongozi.

Ikizingatiwa kwamba mwishoni mwa mchezo huu Bibi anakufa, tunaweza kusema kuwa kifo chake ni taashira ya athari za vita hizi kwa nchi ya Tanzania.

Sara kwa upande wake anatuonyesha taabu zinazowakumba kina mama katika jukumu lao kama wazazi. Sara ana mtoto mmoja Mota lakini amewajibika kumtafutia chakula Bibi na mumewe Huila. Ili kuweza kuilisha jamaa yake, anazunguka huku na huko akita-futa chakula hasa wakati huu wa upungufu. Mwishowe anaposhindwa kufanikiwa, anakatalia dukani mpaka apewe chakula kama wale matajiri anaowaona wakiingia na kutokana makatoni ya vyakula. Tazama jinsi anavyong'ang'ania atendewe haki:-

SAUTI: (Kutoka ndani) Wewe mama bado upo?  
Umengoja nini?

SARA: Nimesema siondoki mpaka nipate mchele,  
Sukari, Unga wa ngano, na sabuni.

SAUTI: Lakini kwa nini husikii? Nakwambia  
hakuna.

SARA: Na mie nakwambia vipo kama vile nimeviona.

SAUTI: Haya makatoni haya yote yanakwenda mikoani.

SARA: Na hao wanaoingia na kutoka na makatoni wanatoka mikoa gani?

SAUTI: Usilete ubishi. Hii ni resheni ya mikoani.

SARA: Kwani mimi sio mtu kama wa mikoani? Au mikoani wananunua kwa dhahabu sio shilingi hii hii?

SAUTI: Basi kaa hapo mpaka utakapochoka

SARA: Ndiyo nitakaa mpaka mtakaponipa chakula. Msiponipa leo, kesho nitakaa na kesho kutwa. Nikiondoka bure nitao-ndoka na mtu.

SAUTI: Huyu mama ana wazimu.

SARA: Nitukane kama unavyotaka. Mimi ninachotaka ni chakula.

Hapa, Sara anawakilishwa kama mwanamke mkakamavu ambaye yuko tayari kuing'ang'ania haki yake mpaka aipate.

Mwanamke katika tamthilia hii amepewa jukumu la kuielimisha jamii, hasa kizazi kipyaa. Kupitia kwa uhusiano baina ya Bibi na mjukuu wake Mota, Muhando anatuonyesha jinsi ambavyo mwanamke kama mtu mwenye ujuzi wa matukio ya kijamii, anavyoweza kuwa mwalimu kwa kizazi kipyaa kinachowakilishwa na Mota. Wakati mwingi Bibi anapokuwa na Mota, anamhadithia hadithi za Dyamini. Hadithi hizi zinakuwa ni kama kumsimulia Mota historia ya nchi yake. Mwishowe, Mota anapoambiwa na mwalimu aandike ngonjera, ngonjera anayoiandika ni juu ya Dyamini. Hata hivyo, hairudii hadithi hii kama alivyoipokea kutoka kwa Bibi bali anahaisha kivyake kwa kuonyesha kuwa Madyamini wamejaa kila mahali hata darasani mwake.

Taswira nyingine ya mwanamke tunayoipata ni ile ya mwanamke kama kielelezo cha mwamko wa kijamii na kisiasa. Taswira hii imeoanishwa na ile ya mwanamke kama msanii na ime-wasilishwa kupitia kwa Bibi na Mota. Katika tamthilia hii, bibi anatusimulia matatizo yanayowapata watu katika vijiji vya ujamaa na kutupigia maswali mazito mazito kama inavyodhihirika katika mazungumzo yake na Mota:-

BIBI: Hebu niambie basi, zamani sana ulikuwepo Utumwa - nasikia walikuwa wakipita vijijini kwetu wanapelekwa pwani. Utumwa ukaisha. Ukaja ukoloni, wazungu wakaja kukaa pale kwetu. Halafu ukoloni ukaisha, wazungu wakahama. Halafu ukaja uhuru, wakaondoa machifu. Babu wa baba yako, huyo Daudi akaa-mbiwa yeye siyo chifu tena. Uhuru ukaisha. Halafu ndio tukasikia ujamaa, ujamaa. Huu ujamaa mwalimu anasema utakwisha lini?

MOTA: (Anacheka) Ujamaa hawezi kwisha Bibi.

BIBI: Yaani siku zote tutaendelea na hizi vurugu zake? Kijijini ujamaa, nikadhania huku mjini afadhali, kumbe wapi. Ujamaa ujamaa! Baba yako na mama yako kila saa ... tena mie sitaki kunifungulia redio linanipigia kelele.

Kupitia kwa Bibi, tunaelezwa pia jinsi watu wanavyo-himizwa kupanda pamba vijijini lakini hiyo pamba haichukuliwi; vile watu wanavyoamua kupanda vyakula ambavyo hata visiponunu-liwa wanaweza kula na jinsi ambavyo serikali inapitisha sera zinazowaathiri wananchi kwa namna mbalimbali pasipo kuwashiri-kisha wananchi wenyewe.

Kama tulivyotaja hapo awali, jukumu la bibi katika mchezo huu limeoanishwa na lile la msanii katika jamii kupitia kwa uhusiano wake na Mota. Kwa kufanya hivi, Muhando anatwambi

kuwa msanii aliyemakinika lazima aielewe barabara historia ya jamii yake ili aweze kuielewa hali ya sasa ya jamii yake.

Tazama Mota anavyoitamba upya hadithi ya Dyamini:-

MOTA: ... Hapo zamani za kale  
Zamani za sasa

SARA: Mota! Ngonjera hazianzikama hadithi.

MOTA: Kwani vibaya? Basi nitafuta. Sikiliza basi.  
Walikuwepo Madyamini  
Kaniambia bibi yangu mpendeka  
Eti wana meno makali  
Wanaonea wenzao.

SARA: Mota! Ngonjera gani hiyo? Haina hata vina?

MOTA: Kwani vibaya? (Anaendelea kusoma na kutamba kwa bidii)  
Nawaambia ndugu zangu  
Hata leo madyamini wapo  
Hapa hapa shuleni.  
Kama yule fulani anakaa deski la mbele  
Kachukua machungwa ya wenzake  
Tena kwa nguvu  
Au kuwadanganya watazame pembeni  
Halafu kuwaibia karanga zao

...

Ni wale tunawajua  
Tena ni wachoyo  
Wakileta keki zao wanakula peke yao  
Tena wanaringa kuwa wana kila kitu  
Eti hawaji shule kwa miguu  
Wanavaa raba mtoni

...

(Anaendelea na ngonjera yake).  
Hata kijijini yapo  
Kanambia bibi yangu mpendeka  
Hata na mijini yapo  
Kasema mama na baba  
Madyamini shuleni  
Madyamini vijijini  
Madyamini mijini ...

...

Madyamini kila mahali  
Hakika kuna uvundo  
Tena kuna ubani. (kur. 55-57).

Katika dondoo hili, tunaweza kubaini msimamo wa

Muhando kuhusu jukumu la msanii chipukizi katika jamii.

Muhando anaonyesha kuwa msanii chipukizi hana budi kufichwa uozo wowote wa kijamii mahali ulipo pasipo woga au pasipo kuzongwazongwa na sheria au kaida za kisanaa. Ndiposa, licha ya kuwa ngonjera ya Mota haifuati kaida za ngonjera, papo hapo inawashambulia wanafunzi wenzake pale darasani ambao wana tabia au mie nendo isiyopendeza.

Muhando pia anaonyesha kuwa msanii ana wajibu wa kuizindua jamii na kuionyesha kuwa kuna matumaini ya kesho yatakayoiletea jamii ile afueni. Ndiposa ngonjera ya Mota inaisha kwa maneno yafuatayo:-

Madyamini kila mahali  
Hakika kuna uvundo  
Tena kuna ubani.(uk. 57)

#### 4:3:3 MTAZAMO WA MWANDISHI

Kama tulivyotaja hapo awali, Lina Ubani ni mojawapo ya michezo ya Muhando ambayo inaonyesha jinsi ambavyo amebadilisha msimamo na mtazamo wake kuhusu baadhi ya maswala ya kijamii. Katika Hatia na Pambo, tulitoa kauli kuwa Muhando analiunga mkono kikasuku Azimio la Arusha. Katika Lina Ubani Muhando analishambulia vikali Azimio hili na hasa unafiki wa viongozi ambao "Wanahubiri maji na kunywa divai". Swali la kujiuliza ni iwapo kubadilika kwa mtazamo wake kuhusu siasa ya nchi yake pia kunaonyesha kubadilika kwa msimamo kuhusu maswala ya wana-wake.

Ili kuweza kulijibu swali hili kikamilifu, tutaanza kwa kuliangalia jukumu la msanii katika jamii kongwe za kiafrika kwa sababu mojawapo ya maswala muhimu anayoyazusha katika

tamthilia hii ni jukumu la msanii katika jamii. Kulingana na Taiwo (1984:1) wanawake katika jamii kongwe za kiafrika walitoa mchango mkubwa katika elimu na fasihi ya jamii. Sanaa yao ilikuwa kupitia kwa njia ya mdomo na lengo kuu lilikuwa kuelimisha kupitia kwa hadithi, ngano, mazungumzo na nyimbo za namn mbalimbali. Hali kadhalika, walisaidia wanajamii wachanga katika harakati za kujifunza kuwa wanajamii. Kwingineko katika kitabu hiki, Taiwo anaeleza kwamba mchango wa wanawake wa kiafrika katika fasihi na jamii ulikuwa unahusiana na majukumu yao kama mabibi, wazazi na washirika katika mambo ya kinyumbani.

Kutokana na maelezo haya, inaweza kuonekana kwamba wanawake, kama wasanii, wamekuwa wakitekeleza jukumu kubwa sana. Jukumu hili, kwa maoni yetu, ndilo analoliashiria Muhando kwa kumsawiri bibi jinsi alivyomsawiri katika uhusiano wake na Mota. Kwa kufanya hivi Muhando amerekodi na kushangilia jukumu hili muhimu ambalo wanawake wamekuwa wakilitekeleza katika jamii kongwe na jamii ya sasa. Katika jamii kongwe, wanawake walitekeleza jukumu kubwa kama wasanii kwa kuwa walihifadhi utamaduni na historia za jamii zao na kupitisha historia na utamaduni huo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jukumu hili ndilo linalotekelezwa na bibi katika Lina Ubani. Kwa kumsanifu bibi hivi, Muhando anatuonyesha kuwa wanawake ni muhimu katika uhifadhi wa tamaduni na historia za jamii zao.

Jambo lingine ambalo Muhando amelitilia mkazo ni jukumu la msanii katika jamii ya kisasa. Mota ndiye anayemwaki-lisha msanii chipukizi na anakuwa ni kielelezo cha jukumu la msanii chipukizi katika jamii. Mota ni mtoto mdogo ambaye anae-

limishwakuhusu historia ya jamii yake na Bibi na pia anapata elimu ya kimagharibi pamoja na elimu ya kisiasa shuleni. Kwa kumsawiri Mota namna hii, Muhando anaonyesha kuwa wasanii wa kike wanaweza kutekeleza jukumu muhimu katika jamii zao. Pengine Muhando anafanya hivi kwa kutambua kwamba katika jamii yake na Afrika kwa jumla, kuna wasanii wachache sana wa kike. Pengine hii ni njia moja ya kuwahimiza watambue umuhimu wao.

Ngonjera za Mota zinawakilisha msimamo wa Muhando kuhusu dhima ya fasihi katika jamii. Kwanza, anaonyesha kuwa mwandishi hapaswi kuzongwazongwa na sheria za utunzi wa sanaa al-muradi sanaa yake ni yakinifu. Ndiposa kila mara Sara anapomwambia Mota Ngonjera zake hazina vina au hazianzi jinsi ngonjera zinavyopaswa kuanza, Mota anamwuliza "kwani vibaya" (kur. 55-57). Pili, anaonyesha kuwa mwandishi katika Bara la Afrika ana mengi ya kujifunza kutokana na historia ya nchi yake na fasihi simulizi ya nchi yake. Ngonjera za Mota zimetokana na hadithi anazotambiwa na Bibi lakini zinapewa uhai mpya. Kwa kumsanifu Mota hivi, Muhando anaonyesha kuwa msanii wa kiafrika ana jukumu la kuihaisha historia na maudhui ya fasihi simulizi ya jamii yake.

Juu ya hayo, Muhando anaonyesha kuwa lazima sanaa ionyeshe tatizo lilopo na kuashiria kesho yenye matumaini kwa wale wanaodhulumiwa. Hii ndiyo dhima ya fasihi katika jamii. Chambilecho Ebrahim Hussein (tazama Abdilatif Abdalla 1980:xii)

... Si lengo la mshumaa uungue  
na giza lizidi. Lengo ni  
kwamba mshumaa utoe nuru mpaka  
nuru ipatikane.

Muhando anaamini hili ndilo jukumu kuu la fasihi yakinifu katika jamii. Lazima fasihi wakati wote ionyeshe chanzo cha matatizo ya jamii na ionyeshe jinsi ambavyo matatizo haya yangeweza kutatuliwa. Ndiposa tunaonyeshwangonjera za Mota zikiishia:-

Madyamini kila mahali  
Hakika kuna uvundo  
Tena kuna ubani (uk. 57).

Ni muhimu kuwa imani hii ya Muhando inawasilisha kupitia msanii wa kike. Msimamo wake ni kuwa wanawake kama wasanii hawana budi kuipa jamii matumaini.

Jambo lingine ambalo ni muhimu katika Lina Ubani ni kwamba Muhando ameanza kuwatoa wanawake wake nyumbani. Katika tamthilia hii, tunakutana na wanawake kama vile Sara, mkewe Huila, na Mota bintiye ambao wamepata elimu sawia na wanaume. Ijapokuwa hatuambiwi kiwango cha elimu cha Sara wala kazi anayoifanya, hatuna shaka kuwa si mwanamke wa kinyumbani tena ambaye hatima yake lazima iamuliwe na mwanaume. Katika mkabala huu, Mota pia yuko shuleni ambapo anapata elimu. Tuliona hapo awali kuwa wengi wa wahusika wake wa kike hajasoma kama walivyofanya wahusika wa kiume. Pia, tuliona wahusika wake wa kike kama vile Cheja katika Hatia wakifungika na majukumu yao kama wazazi. Katika Lina Ubani Muhando anatusawiria wahusika tofauti. Ijapokuwa Sara kwa mfano anatekeleza wajibu wake kama mama, hafungiki nyumbani kwa sababu ya wajibu huu. Sara anafanya kazi ya Ofisini kama mumewe Huila.

Sara na bintiye ni wanawake wakakamavu ambao wako tayari kwa vyovyote vile kuupinga uozo uliosakini katika jamii yao. Sara kwa mfano, anagoma kuondoka kutoka ofisi ya ugawaji mpaka apewe chakula kama wanavyopewa wale wengineo wenye nguvu za kiuchumi. Anamwambia mgawaji:-

Na hao wanaoingia na kutoka na  
Makatoni wanatoka mikoa gani?

...

Kwani mimi sio mtu kama hao wa  
mikoani? Au mikoani wananunua kwa  
dhahabu sio shilingi hii hii?

...

...nitakaa hapa mpaka mtakaponipa  
chakula (uk. 37.38)

Sara hatishiki. Yu tayari kuing'ang'ania haki yake. Mota naye katika ngonjera zake anawashambulia hata walioko darasani mwake.

Hata hivyo, tatizo la jinsi Muhando anavyowasawiri wahusika hawa hasa katika uhusiano wao na Huila linatokana na jinsi ambavyo Huila amepewa jukumu kubwa la kutekeleza katika ngazi ya kitaifa. Huila ni mtaalamu wa mambo ya nishati. Wakati mwingi tunamwona akishughulika na mambo ya kitaifa. Sara kwa upande wake anaonekana kuwa "mtaalamu" wa mambo ya kinyumbani. Wakati mwingi tunapokutana naye, anashughulika na mambo ya chakula au ungonjwa wa mamake Huila. Juu ya huyo, ukakamavu wa Sara ni finyu ukilinganishwa na ule wa Huila katika mikinzano yake na Zoeni. Maoni yetu ni kuwa Sara hajakuzwa kimawazo kama alivyokuzwa Huila.

Kwa kuwasawiri wahusika hawa wawili hivi, ijapokuwa Muhando anaonekana kuanza kubadilisha mtazamo wake kuhusu

wanawake, inaonekana bado hajitokezi waziwazi. Kwa hivyo, Ijapokuwa 'kuna ubani' bado Muhandu anayumbayumba kuhusiana na swala hili. Anashindwa kumsawiri mhusika ambaye anaweza kuwa kielelezo kwa wanawake wengine. Katika mkabala huu, hatuonyeshi uhusiano uliopo baina ya Sara na Huila pale nyumbani kwao. Kwa kutofanya hivi, anakuwa bado hajatubainishia kama anaashiria usawa wa kiuana au la.

Bibi kama mwanamke anawakilisha itikadi na mielekeo ya kijadi kuhusu wanawake; hasa wa kabila tofauti na lake. Kwa mfano, hampendi Sara kwa kuwa ni Mchusa na anaamini kuwa Wachusa ni wabaya. Kila mara anamwita 'Yule mwanamke' ili kuonyesha kinyongo alichu nacho juu yake. Mbali na hayo, hadithi nyingi anazompa Mota zinaonyesha ubaya wa wanawake. Anamwambia:-

BIBI: Ee Mota mjukuu wangu, wewe mtoto mdogo. Lakini walimwengu wabaya. Hawapendi kuona wenzao wakistareheka na kuneemeka. Ndiyo. Kama yule mwanamke wanamwita sijui Lijino. Ndugu zake za akina kata nasikia. Basi yule mwanamke katufanya kitendo. Wenyewe tulistarehe kule kwetu Malalo. Chakula kila aina. Wewe ulikuwa mdogo sana mlipokuja na mama yako. Malolo ndizi! Viazi! Miwa! Mmoja humalizi.

MOTA: Namaliza bibi.

BIBI: Humalizi nakwambia. Na uroho wako wote humalizi muwa unakuwa mrefu mpaka unapinda. Ndizi mkungu kimo chake. Njaa sie tunasikia tu. Basi kaja huyo Lijino huyo! Mmh! Mwanamke yule! Nasikia ana watoto lakini utafiki-kiri hukuzaa. "Mtahama! Amri moja! Kwa hiari mmekataa. Sasa amri moja! Basi kwenda kutuweka nyikani pale, udogo hauoteshi kitu. Daudi mwanangu akipenda miwa ... (kur.17-18)

Hadithi hizi za bibi, ijapokuwa kwa undani wake zinaonyesha ukinzani dhidi ya utekelezaji wa siasa ya ujamaa, kwa kiwango kingine zinatonyesha mielekeo ya kijadi dhidi ya wanawake.

Ni muhimu tuzingatie kuwa mwishoni mwa mchezo Muhando anamuua mhusika huyu. Kwa kufanya hivi Muhando anaiondoa mbegu mbaya anayoipanda katika akili changa ya Mota. Kifo chake kinashabihiana na cha Niakoro katika God's Bits of Wood. Je, Mota naye atakuwa mwanamke na msanii wa aina gani? Katika ngonjera za Mota, hatuoni kukizuka maswala yoyote yanayohusiana na swala la mwanamke. Wala hatuonyeshwi Mota akikuzwa kisanaa na mwandishi kukua kuwa mwanamke ambaye amejikomboa kimawazo kutokana na itikadi za kijadi za jamii yake. Kwa kutomkuza Mota kisanaa, ijapokuwa Muhando anajitokeza kuwa na mtazamo yakinifu kuhusu maswali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya nchi yake, anaonekana kutokuwa na msimamo hakika kuhusu swala la mwanamke. Bado hajajitokeza moja kwa moja kutetea maslahi ya wanawake. Hata hivyo, kuna matumaini kwa sababu ameanza kuwapa wanawake majukumu yaliyo nje ya yale ya kijadi.

#### 4:4 K I M A L I Z I O

Katika sura hii, tumesisitiza kuwa Muhando kama mwandishi wa kisiasa amebadilisha mtazamo na falsafa yake kuhusu siasa ya ujamaa. Tumesema kuwa amevuka kiwango ambapo alikuwa akionelea kuwa masuluhisho ya matatizo ya nchi yake yako kwenye Azimio la Arusha. Katika uandishi wake wa miaka

ya themanini, anaanza kutuonyesha udhaifu wa siasa ya ujamaa tofauti na uandishi wake wa miaka ya sabini.

Katika Nguzo Mama, Muhando, tumeonyesha, ametusawiria wanawake katika hali halisi na kutuonyesha umuhimu wao kupitia kwa jazanda ya nguzo mama. Tumeona kuwa mtazamo na msimamo wake ni kwamba ijapokuwa kutoka nje jamii yake inaonekana kuwa nzuri, ndani ina uozo; wanawake wananyanyaswa na kutothaminiwa ijapokuwa wao ndio wanaoiendeleza jamii. Anaonelea kuwa suluhisho la tatizo hili liko katika mwungano wa wanawake. Hata hivyo, tumesema kuwa falsafa yake ni kuwa jamii yenye haki inaweza kujengeka tu ikiwa kuna uasawa baina ya wanaume na wanawake. Pia, tumeona kuwa Muhando anaonekana kutokuwa na matumaini makubwa. Mwishoni mwa mchezo, mwungano anaotetea haujapatikana. Kwa kufanya hivi, tumesema, Muhando anaonekana kuyumba kimtazamo na kimsimamo.

Pia, tumeona kuwa Lina Ubani ni tamthilia inayoonyesha kutoridhika kwake sio tu na swala la ujamaa bali pia na jinsi ambavyo viongozi wa nchi yake wanayaendesha maswala ya kitaifa. Anaukashifu sio tu utekelezaji wa Azimio la Arusha bali pia ubinafsi na tamaa ya kujilimbikizia mali ambayo imeota mizizi miongoni mwa viongozi ambao wanaipora mali ya umma. Katika mkabala huu, tumesema kuwa Muhando anatuonyesha jukumu la mwanamke katika jamii. Wahusika wake wa kike wanasawiriwa katika majukumu yao kama wazazi na wasanii. Kwa kufanya hivi, ameonyesha sio tu umuhimu wao bali pia mchango ambao wamekuwa wakitoa na wanaweza kutoa katika jamii zao.

Jambo lingine ambalo amefanya ni kuwatoa wahusika wake 'jikoni'. Hapa, ametusawiria wahusika wa kike waliosoma na ambao wanafanya kazi sawia na wanaume iwapokuwa hajatuambia kazi wanayofanya au kiwango chao cha elimu. Hata hivyo, tumesema kuwa kwa kumpa Huila jukumu na nafasi kubwa aliyompa ikilinganishwa na Sara, Muhando anaonekana kutokuwa na msimamo thabiti kuhusu kiwango ambacho wanawake wanaweza kushiriki katika harakati za ujenzi wa taifa.

5:0

SURA YA TANO

5:1 H I T I M I S H O

Katika tasnifu hii, tumejaribu kuchunguza jinsi amabvyo waandishi wa kike, ambao huandika tamthilia katika lugha ya Kiswahili, wanalishughulikia swala la mwanamke katika tamthilia zao. Ili kufanikisha lengo letu, tumezichambua tamthilia mbili ambazo zimeandikwa na waandishi wa Kenya katika kipindi cha miaka ya themanini. Hizi ni Ryanga (1986) Zinduko na Mwachofi (1987) Mama Ee. Aghalabu tumetaja kuwa kila mmoja wa waandishi hawa Ryanga na Mwachofi ameandika tamthilia moja. Pia, tumewachambua waandishi wawili wa Tanzania. Hawa ni Angelina Chogo na Penina Muhando. Tamthilia ya Chogo tuliyoichambua ni Kortini Mtu Huyu (1976) ilhali za Penina Muhando tulizozihakiki ni Hatia (1972), Pambo (1975), Nguzo Mama (1982) na Lina Ubani (1984).

Katika sura ya kwanza, tumezungumza kwa muhtasari kuhusu somo letu la utafiti, sababu zilizotufanya kuchagua somo hili, yale ambayo kufikia sasa yameandikwa kuhusu somo hili na nadharia ambayo tumetumia kama kigezo cha kuwachambua waandishi hawa. Tumeonyesha pia upeo wa kazi yetu na njia ambazo tumetumie kuufanya utafiti huu. Tumeonyesha kuwa kilichotupa hamasa na msukumo wa utafiti huu ni madai ya wahakiki wengi waliolishughulikia swala la usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi kuwa taswira mbaya zinazopatikana katika nyingi ya kazi hizi zinatokana na ukweli kwamba wengi wa waandishi hawa ni wa kiume. Kwa hivyo, wanapowasawiri wahusika wao wa kike huwa wanawakilisha

na kuendeleza falsafa za jamii zao kuhusu wanawake ambazo hazimpi hadhi mwanamke. Kutokana na kauli hizi, tumepata hamu ya kutaka kuangalia jinsi wanawake wenyewe wanavyoyashughulikia maswala yanayowahusu wanawake wenzao.

Katika sura ya pili, tumewashughulikia waandishi wa Kenya mmoja baada ya mwingine. Tumesema kuwa Mwachofi katika Mama Ee anaipiga darubuni nafasi ya mwanamke katika jamii ya sasa kama inavyodhihirika katika taasisi ya ndoa. Kupitia kwa wahusika wakuu wa kike kama vile Mwavita, Mamake Mwavita na mdogo wake Tenge, mwandishi amefanikiwa kuonyesha kuwa wanawake wote, pasipo kujali umri, kiwango cha elimu, tabaka wala cheo, wanakumbana na dhiki zinazotokana na uana wao. Tumedhihirisha kuwa jamii anayoishughulikia Mwachofi ni jamii ambayo imesheheni taasubi za kiume. Kutokana na haya, jamii inamtunukia mwanaume jukumu la kiungu. Katika mkabala huu, mwanamke anatarajiwa awe mtiifu kwa mumewe, amsujudie na kumnyenyekea. Mwanamke kama mali ya mwanaume ni lazima aikubali hali hii ya utumwa. Hata hivyo, tumeonyesha kuwa kupitia kwa Mwavita na Tenge, mwandishi anaishambulia vikali mifumo inayomvua mwanamke utu wake na kumdunisha namna hii huku akionyesha kuwa kuna uwezekano wa wanawake kujikomboa na iwapo watalifikia lengo hili, lazima waelimishane, waungane na kumpiga vita adui yao ambaye kwa maoni ya Mwachofi ni mwanaume.

Katika kuihakiki kauli hii ya mwandishi, tumesema kuwa mwandishi ameshughulikia kipengele kimoja tu cha tatizo la mwanamke ambacho ni mielekeo inayotokana na mfumo na utamaduni wa kuumeni (Patriarchy) ambao unamweka mwanaume mbele na

kumdunisha na kumdhalilisha mwanamke. Mfumo wa kibepari, ambao unachangia sehemu kubwa ya matatizo ya wanawake, umepuu- zwa na mwandishi. Kwa maoni yetu, mifumo hii miwili ni pande mbili za sarafu moja. Inategemeana, kuhimiliana na kuimarisha- na. Ikiwa wanawake watajikomboa na ukombozi huu uwe na maana kwao, lazima mifumo yote miwili ipigwe vita kwa pamoja.

Lazima tukariri kuwa Mwachofi ameonekana kuyumbayumba kintazamo. Tumeonyesha kuwa msimamo wake kuhusu ulipaji wa mahari unapotosha. Juu ya hayo, tumetaja kuwa kwa kumchora mhusika Kheri, Mwachofi ameivunja ile imani aliyokuwa ameijenga hapo awali kuwa mwanamke hamhitaji mwanaume ili kuyaendesha na kufikia upeo wa maisha yake. Pengine amefanya hivi kwa kuta- mbua kuwa katika jamii ambapo wanaume na wanawake wanaishi na kushirikiana katika nyanja mbalimbali za maisha lazima wategeme- ane. Kwa maoni yetu, ushirikiano na uhusiano wa namna hii ni wa lazima. Hata hivyo, unapaswa kuwa umejengeka katika misingi ya ubinadamu na usawa wala sio katika hali ambapo mmoja wao atam- tumikisha, kumnyanyasa na kumdhulumu mwenzake.

Katika sura hii, pia tumeuchambua mchezo wa Ryanga wa Zinduko. Hapa, tumeona kuwa Ranga anajishughulisha na unafiki wa viongozi kama vile Toto. Tumeonyesha kuwa Ryanga hajapevuka kimawazo kwa jinsi anavyolishughulikia swala hili hasa akili- nganishwa na waandishi wengine kama vile David Mulwa na A.S. Yahya katika Ukame au Chacha Nyaigotti-Chacha katika Wingu Jeusi. Kwa vile kazi yetu imeegemea sana upande wa swala la mwanamke, tumedhihirisha kuwa Ryanga ametusawiria wanawake ambao hawaja- pevuka kimawazo na kisiasa.

Wahusika wake wa kike ni wanawake ambao wanajiamini kuwa 'wakurugenzi' wa maswala ya kinyumbani na ambao wanawafuata wanasiyasi kijingajinga. Kwa kufanya hivi, tumemtazama Ryanga kama mwanamke anayeamini na kuhubiri kwamba mwanamke ni msaidizi wa mwanaume na hawezi kushiriki kwa usawa na mwanaume katika mambo yanayohusu maendeleo ya taifa lake. Daima atabakia kuwa chini ya mwanaume. Ndiposa tunakutana na wanawake kama vile Bi. Faida ambaye licha ya juhudi zote alizofanya kumsaidia mumewe katika harakati zake za kuomba kura, halalamiki kwa kufukuzwa kutoka kikao cha wanaume pale nyumbani kwake. Pia kuna Fani, mkewe Toto ambaye, licha ya yote aliyotendewa na mumewe Bw. Toto, anachoweza kufanya ni kuulilia hali yake tu. Kwa kuhubiri imani hii, Ryanga anawadhalilisha wanawake wenzake hata zaidi ya wafanyavyo baadhi ya waandishi wa kiume hasa ikizingatiwa kuwa yeye ni mwanamke ambaye anapaswa kufahamu barabara kuwa maisha ya wanawake, kama wanavyoyaishi katika ulimwengu wa sasa si ya kutamaniwa kamwe.

Kauli tunayoweza kuitoa kuhusu Ryanga kama mwandishi ni kwamba yeye ni mwandishi wa kibwanyenye ambaye amelisaliti kundi lake la wanawake wanaodhulumiwa na kuhiniwa.

Sura ya tatu imejikusisha na waandishi wawili wa Tanzania katika kipindi cha 1972-1976. Hawa ni Angelina Chogo (Kortini Mtu Huyu) na Penina Muhando, Hatia na Pambo. Tumesema hiki ni kipindi maalumu katika historia ya Tanzania huru hasa kuhusiana na siasa ya ujamaa ambayo ilikuwa ikitekelezwa wakati huo. Mazingira haya ya kihistoria yamewaathiri waandishi hawa kimau-

dhui na athari hizi zimebainika katika kazi hizi, hali ambayo inajitokeza katika maandishi mengi ya Tanzania ya wakati huo. Jambo ambalo limedhihirika ni kwamba kazi hizi zina maudhui yaliyobobea katika mazingira ya kimji. Katika Kortini Mtu Huyu, tumeona kuwa wahusika wengi wa kike wamesawiriwa kama malaya na suluhisho linalopendekezwa na mwandishi ni kwamba wanawake hawa wanapasa kurudishwa vijijini ili waweze kurekebishwa tabia. Hili tumeliona kuwa suluhisho ambalo, mbali na kupotosha lengo na maana ya vijiji vya ujamaa, halishughulikii ipasavyo nafasi ya mwanamke katika vijiji hivyo. Kwa hivyo, kwa kuwarudisha vijijini, mwandishi amajishughulisha zaidi kuonyesha imani yake katika siasa ya ujamaa pasipo kuuchambua mfumo huu ili kubainisha nafasi ya mwanamke. Imani yetu ni kwamba ujamaa peke yake hauwezi kumkomboa mwanamke.

Kuhusu maandishi ya Muhando tuliyoyashughulikia katika sehemu hii, tumeonyesha kuwa Muhando anawaumba wahusika wake katika mazingira ya utamaduni mkongwe. Kwa hivyo, taswira tunazozipata katika Hatia ni zile za mwanamke kama chombo cha kujitajirisha, chombo cha kujifurahisha, chanzo cha maovu na mtumwa kwa mwanaume. Tumeonyesha kuwa Muhando anaihubiri siasa ya ujamaa kikasuku. Haya anayafanya kwa kumpeleka mhusika wake mkuu Cheja kwenye kijiji cha ujamaa cha Majogo. Tumeshikilia kuwa suluhisho hili ni la kijuujuu mno na halilisuluhishi tatizo la Cheja. Tumependekeza kuwa pengine ni kwa kutambua ukweli huu ambapo Muhando aliandika Heshima Yangu na Talaka Si Mke Wangu ambazo ni tamthilia zinazoonyesha maisha ya kutoridhisha ya wanawake katika vijiji vya ujamaa.

Katika kuzingatia Pambo, tumeonyesha kuwa huu ni mmojawapo ya michezo mipevu sana kimtindo na kimaudhui aliyowahi kuandik Muhando kufikia hivi sasa. Katika tamthilia hii, tumeonyesha kuwa anajishughulisha na athari za elimu ya kikoloni kwa waafrika kupitia kwa mhusika Pambo. Elimu hii inawakengeusha walio-pokea na kusheheneza hisia za ubinafsi katika akili zao kiasi kwamba wanashindwa kushughulikia matatizo halisi ya jamii zao. Badala yake, inawajaza tamaa iliyokithiri; tamaa ya anasa, cheo na mali na kuwafanya washikwe na kichaa. Kichaa hiki ni taashira ya utengano wao na jamii. Hata hivyo, tumeonyesha kuwa Muhando anaamini kwa dhati kuwa ili jamii iweze kubadilika, lazima jamii yenyewe ielimishwe.

Kuhusu wanawake, jambo ambalo limeshuhirika waziwazi ni kwamba wanawake wengi wa Muhando ni wanawake ambao hawajasoma na kwa hivyo hawawezi kushiriki kikamilifu katika juhudi za ujenzi wa taifa lao. Jukumu hili limeachiwa wanaume. Huu tumeona kuwa ni udhaifu kwani Muhando ameshindwa kuiwakilisha ipasavyo hali halisi. Tumeshuhirisha kuwa Muhando hana msimamo thabiti kuhusu swala la mwanamke na wakati mwingine, hasa katika Pambo anaendeleza taswira ambazo zinaishusha hadhi ya mwanamke hasa kwa kupitia kwa wahusika Maua, Salome, Suzie na Hadija. Hawa ni wanawake ambao katika uhusiano wao na Pambo wanamzidisha kichaa. Kwa kutusawiria wahusika wa namna hii, Muhando anawonyesha wanawake kama mashetani wanaou vuruga ulimwengu mtulivu wa wanaume na kusababisha maafa.

Katika sura ya nne, tumezichambua tamthilia mbili za Muhando ambazo ni Nguzo Mama na Lina Ubani. Hizi ni tamthilia ambazo ameziandika katika miaka ya themanini. Tumedhihirisha kuwa katika kipindi hiki, Muhando amebadilisha msimamo wake hasa kuhusu siasa ya ujamaa na pia amepevuka na kukomaa kimawaz Ujamaa sio suluhisho la matatizo ya kijamii tena. Badala yake, anatumfichulia hiana na unafiki wa viongozi ambao umewafanya watu wa kawaida waanze kuupigia maswali ujamaa.

Mambo kadha wa kadha yanayotendeka katika kipindi hiki yanamwathiri mwandishi huyu kimtindo na kimaudhui. Matukio kama vile kutangazwa kwa mwongo wa kina mama ulimwengu kote na vita vya Kagera yameonyeshwa kuwa na athari ya moja kwa moja katika uendelezaji wa maudhui ya tamthilia hizi. Nguzo Mama kwa mfano ni tamthilia ambayo ina wahusika wengi sana wa kike. Hii ni kwa sababu Muhando anauandika mchezo huu ili kusheherekea mwongo huu. Katika tamthilia hii, Muhando anaonyesha matatizo yanayowakumba wanawake katika juhudi zao za kuungana pamoja na pia umuhimu wao katika ujenzi wa taifa lao. Anafanikiwa kufanya hivi kupitia kwa jazanda ya "Nguzo Mama" na pia kwa kuwasawiri wahusika wake kiaina na kijazanda. Hata hivyo anaishilia kuonyeshakuwa hakuna matumaini ya kuziondosha tofauti za kibinafsi baina ya wanawake ili waweze kujikomboa. Ndiposa mwishoni mwa mchezo, nguzo mama bado haijainuliwa.

Katika Lina Ubani, Muhando anaonyesha matumaini yake kuwa kuna uwezekano wa kuisafisha jamii kutokana na uozo ulio-sakini; uozo ambao unatokana na uongozi mbaya unaoyaweka maslah

ya kibinafsi mbele ya maslahi ya umma. Jambo la muhimu kukumbuka hapa ni kuwa Muhando katika Nguzo Mama na Lina Ubani amebadilisha msimamo wake kuhusu wasomi-teule. Ilhali hapo awali alionelea kuwa wamezisaliti jamii zao, sasa anaonelea kuwa jamii hizo ndizo zinazowasaliti wasomi kama vile Bi. Nane na Huila.

Kuhusu wanawake, la muhimu kubainisha ni kuwa Muhando ameanza kuwatoa wanawake wake 'jikoni' na kuwashirikisha katika harakati za ujenzi wa taifa. Katika Nguzo Mama na Lina Ubani, tunakutana na wanawake ambao wamesoma na wanafanya kazi. Hata hivyo, bado wanaume wanawekwa katika nafasi ya mbele. Pengine hii ndiyo hali halisi katika jamii nyingi za ulimwengu. Hata hivyo, lengo la fasihi sio tu kutuchorea picha ya hali halisi na kutuacha hapo. Lazima kazi hiyo isaidie kubadilisha hali hiyo kwa lengo la kuleta afueni kwa wale wote wanaonyanyaswa. Kulingana na Fischer (1972:159):

Ni jukumu la msanii, sio tu kuonyesha hali halisi, bali pia, kusaidia kuibadilisha hali hiyo..

Ndipo tunaonelea kuwa Muhando kama mwandishi ameshindwa kusimama kama mtetezi halisi wa maslahi ya wanawake wenzake. Fasihi inayolenga usawa wa kitabaka na kiuana lazima itusawirie wabusika ambao wanaweza kuigwa na wadhulumiwa wenzao; katika muktadha huu, wanawake wenzao. Hili ni jambo ambalo halijitokezi moja kwa moja katika Nguzo Mama na Lina Ubani. Kwa sababu hii, tunaonelea kuwa ijapokuwa Muhando katika Lina Ubani anasisitiza kuwa kuna matumaini ya kuuondosha uozo uliojikita katika jamii yake, swala la mwanamke halionekani

kuwa muhimu katika mkabala huu. Kwetu, hili ni dhahirisho kuwa Muhando bado yuko katika njia-panda.

5:2 KAZI KWA JUMLA

Tamthilia zote ambazo tumezishughulikia katika tasnifu hii zinadhahirisha tofauti za kimaudhui, kimtindo na kimtazamo. Kila mmoja wa waandishi hawa anaiwakilisha hali halisi kama anavyoiona. Hata hivyo, jaribio la kuonyesha uhusiano uliopo baina na utamaduni mkongwe, uchumi, siasa na swala la mwanamke linazusha matatizo ambayo kila mmoja wao amejaribu kuyatolea suluhisho analoliona kuwa mwafaka. Katika kuyachambua na kuyahakiki masuluhisho haya, inabidi tuzingatie kuwa waandishi hawa wanaandika ama katika mazingira tofauti au kwa sababu tofauti. Mwachofi na Ryanga wanaandika katika mazingira ya kibepari ilhali Muhando na Chogo wanaandika katika mazingira ya ujamaa. Tofauti hizi zinasababisha tofauti za kimaudhui, uendelezaji wa maudhui na masuluhisho wanayoyapendekeza. Hata hivyo, wote wameyachota maudhui yao katika jamii za binadamu ambapo wanaume na wanawake wanaishi kwa ushirikiano katika maisha yao ya kila siku. Ndiposa tunaonelea kuwa katika kila mojawapo ya kazi hizi, swala la uhusiano baina ya makundi haya mawili linatokea kuwa la kimsingi. Hata pale ambapo mwandishi ameamua kushughulikia maswala ya kisiasa na kijamii, uhusiano baina ya wanaume na wanawake unajitokeza kuwa jambo muhimu. Mfano mzuri ni tamthilia za Muhando za Pambo na Lina Ubani. Katika tamthilia hizi, mwandishi haku-dhamiria kulishughulikia swala la mwanamke moja kwa moja lakini

uhusiano baina ya wanaume na wanawake unatokea kuwa muhimu katika kuyaendeleza maudhui makuu ya kazi hizi. Kwa sababu hii, tunaonelea kuwa ijapokuwa waandishi hawa wanaandika katika mazingira tofauti na kutoa masuluhisho tofauti, kila mojawapo ya kazi hizi, pasipo kujali kiwango chake cha kisanaa, inatoa mchango mkubwa katika kuendeleza na kufanikisha au labda kutinga maslahi ya wanawake na katika kuanzisha na kuendeleza kile ambacho tuna-weza kukiita utamaduni wa kisanaa wa kike.

Hatuwezi, wala hatutaki, kudai kwamba mtazamo wa kike (the woman's point of view) umepewa nafasi muhimu katika kazi ambazo tumezishughulikia. Hili linatokana na, kama tulivyosema hapo awali, ukweli kwamba kila mmoja anaisanifu hali halisi kama anavyoiona. Hata hivyo, jambo linalodhihirika ni kwamba wanatamthilia hawa wote wanaishambulia mifumo ya kijamii inayo-endelezwa katika jamii zao. Wanaushambulia hasa mfumo wa kuu-meni, uchoyo na unafiki wa viongozi wanaowanyanyasa wananchi na mifumo mingineyo ya kijamii ambayo haiendelezi maslahi na amali za kibinadamu. Katika hali hii, mwanamke yuko katikati ya mambo yote yanayotendeka na ni katika hali hii ambapo waandishi wa kike, hata wale wanaopotosha kama Ryanga, wanapata msukumo na mshawasha wa kuandika.

Jambo lingine linalodhihirika katika kazi hizi ni kwamba kwa maoni ya waandishi hawa, wanaume na wanawake wanategemeana katika kufanikisha maisha yao ya kila siku. Ndiposa tunaona kwamba wote wanatetea, kwa njia moja au nyingine, usawa baina ya wanaume na wanawake ili kila mojawapo ya makundi haya liweze kufikia malengo yake pasipo kugandamizwa na lingine.

Kwa mfano ijapokuwa Mwachofi amejaribu kuonyesha ubaya wa wanaume katika Mama Ee, mwishoni anatuambia mhusika Kheri, ambaye ni kielelezo cha mwanaume anayeweza kuufanikisha uhusiano mzuri baina ya wanaume na wanawake kama wanajamii.

### 5:3 MATATIZO NA MAFANIKIO

Kila kazi ya utafiti haikosi kuwa na vikwazo. Katika tasnifu hii, tatizo kubwa tulilokumbana nalo ni kuzipata tamthilia zenyewe. Baadhi ya tamthilia tulizozishughulikia katika kazi hii ama hazipatikani hapa nchini Kenya au zimeacha kuchapishwa. Hata hivyo, kwa msaada wa marafiki, tulifanikiwa kuzipata baadhi ya kazi hizi.

Tatizo lingine ambalo tumekumbana nalo ni kwamba ijapokuwa tulikuwa tunatarajia kufanya mahojiano na baadhi ya waandishi hawa, hatukufanikiwa kutokana na sababu mbili. Kwanza, uhaba wa fedha za utafiti haungeturuhusu kuwafikia waandishi hawa hasa wale wa Kitanzania. Pili, waandishi wawili wa Kenya tuliowashughulikia kwa wakati huu wako nje ya Kenya na kwa sababu hii hatukuweza kuwafikia. Ilitubidi basi kutegemea baadhi ya mahojiano ambayo baadhi ya waandishi hawa kama Penina Muhando wamefanyiwa na watu wengine.

Licha ya matatizo haya, tumejaribu kuonyesha jinsi wanawake hawa wanavyowasawiri wahusika wao wa kike na pia kubainisha mitazamo yao kuhusu swala la mwanamke kama inavyodhihirika katika kazi hizi. Hii imekuwa mojawapo ya kazi ambazo zimelishughulikia swala la mwanamke katika tamthilia za kike za Kiswahili.

5:4 M A P E N D E K E Z O

Kazi hii imejikita katika kuchunguza usawiri wa wahusika wa kike na mitazamo ya waandishi wa kike kama inavyodhihirika katika kazi hizi. Kuna mambo ambayo kutokana na upeo wa tasnifu hii hatukuyashughulikia kwa undani sana. Mambo kama vile maudhui makuu katika kazi hizi na kazi za wana-wake kwa jumla ni jambo ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti. Vile vile, mitindo na lugha wanayoitumia waandishi hawa ili kufanikisha kazi zao ni jambo ambalo linapasa kufanyiwa utafiti zaidi.

M A R E J E L E O

- Abdalla, A. (1981): Utangulizi wa Sikate tamaa kilichoandikwa na S.A. Mohammed, Nairobi, Oxford University Press.
- Achebe, C. (1975): Morning Yet on Creation day, London, Heinemann.
- Adagala, K.(1985): Wanja of Petals of Blood: The woman question and Imperialism in Kenya, Nairobi, Derika Associates.
- Aidoo, A.A. (1987): Katika mahojiano na Sarah Chetin yaliyo-chapishwa katika WASAFIRI; journal of African, Caribbean and Black British Literature.
- Aidoo, A.A. (1988): "To Be an African Woman Writer - an Overview and a Detail" Katika Criticism and Ideology, 2nd African writers conference, seminar proceedings no.20, S.I.A.S.
- Amadiume, I. (1987): Male daughters, Female husbands, London, zed Publishers Ltd.
- Arvon, H. (1973): Marxist Esthetics, London, Cornell University Press.
- Balisidya, N. (1974): Shida, Nairobi, Foundation Books (Kazi zote alizoandika baada ya kuolewa zimetokea kwa jina Matteredu M.N.L.B.
- Boesen, J.S. et. al(1977): Ujamaa: Socialism from above, Uppsala, Scandnavian Institute of African Studies.
- Bouchier, D. (1983): The Feminist Challenge, London, Macmillan Press.

- Brown, L.W. (1981): Women writers in Black Africa, Westport, Connecticut, Greenwood Press.
- Chacha, C.N.(1984): "Mazingira ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili: Rosa Mistika wa Keilahabi", katika MWAMKO Vol.3; Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- \_\_\_\_\_,(1990): "Gender Oppression in the arts: A Comment on women characterisation in Kiswahili Literature," karatasi iliyo-wasilishwa katika 2nd Pan-African Association of Anthropologists, Nairobi.
- \_\_\_\_\_,(1987): Wingu Jeusi, Nairobi, Heinemann.
- \_\_\_\_\_,(1988): Modern Swahili Literary texts, (part 2) BSW 201 Lecture series, University of Nairobi, College of Education and External Studies, Faculty of External Studies, Department of Education, Nairobi, University of Nairobi Press.
- Chafe, W.H. (1977): Women and Equality: Changing Patterns in American Culture, New York, Oxford University Press.
- Chesaina, C. (1987): "Women in African Drama: Representation and Role." PhD Thesis, School of English, University of Leeds, (Haijachapishwa).
- Chogo, A. (1976): Kortini Mtu Huyu, Nairobi, Foundation Books.
- Davies, C.B.  
Graves, A.A. (1986) Wahariri: Ngambika: Studies women in African Literature, Trenton, New Jersey, Africa World Press.

- Eagleton, M. (1986)(Mhariri): Feminist Literary Theory: A reader, New York, Basil and Blackwell.
- Eisenstein, Z (1979)(Mhariri): Capitalist Patriarchy and the Case for Socialist feminism, New York, Monthly Review Press.
- El Saadawi, N. (1980): The Hidden face of Eve: Women in the Arab World, London, Zed Press.
- Emecheta, B. (1988): "Feminism with a small 'f'!" Katika Criticism and Ideology, 2nd African Writers' Conference, Seminar Proceedings No.20, S.I.A.S.
- Engels, F. (1972): The Origin of the family, Private property and the state, London, Penguin Books.
- Fanon, F.(1969): The Wretched of the earth, Paris, Presence Africaine.
- Figes, E.(1978): Patriarchal Attitudes, London, Virago Press.
- Fischer, E.(1972): 'The origins of Art' katika Marxism and Art: Writings in Marxist aesthetics and criticism Kilichohaririwa na Lang, B. na Williams, F., New York, David Mckay Co. Inc.
- Freeman, J. (1983 Edition)(Mhariri): Women: A feminist perspective, Mayfield Publishing Co.
- Gakwandi, A.S. (1977): The Novel and Contemporary experience in Africa, London, Heinemann.

- Garskof, M.H. (1971): Roles women play: Readings towards Women's Liberation, Belmont, California, Brooks/Cole Publishing Co.
- Gikandi, S. (1987): Reading the African Novel, Nairobi, Heinemann.
- Heywood, C.(1971): Perspectives on African Literature, New York, Africana Publishing Corporation
- Hussein, E. (1971): Mashetani, Nairobi, Oxford University Press.
- Iglitzin, L. & Ross, R.(1976): Women in the World: A Comparative Survey, Santa Barbara, California, Clio Books.
- Jefferson, A & Davies, C.B.(1982): Modern Literary Theory, New Jersey, Totiwa Barnes and Noble Books.
- Kezilahabi, E. (1975): Dunia Uwanja wa fujo, Arusha, Eastern Africa Publications.
- \_\_\_\_\_, (1979): Gamba la Nyoka, Arusha Eastern Africa Publications.
- Kiai, G.(1987): "Symbolism and Imagery: An analysis of Bessie Heads fictional works," *Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi*. (Haijachapishwa).
- Kieti, M. (1991): "From oral to Modern women Literature in Africa; The woman question in Africa", *Karatasi iliyowasilishwa katika Psycholog Institute, Gothenburg University, Sweden* (Haijachapishwa).

- Lang, B. & Williams, F. (1972) (Wahariri): Marxism and Art: Writings in Marxist aesthetics and Criticism, New York, David McKay Co. Inc.
- Little, K. (1973): African Women in towns, London, Cambridge University Press.
- \_\_\_\_\_, (1980): The Sociology of Urban women's Image in Literature, London, MacMillan Press.
- Lugano, R.S. (1989): "Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Lukács, G. (1962): The Meaning of Contemporary realism, London, Merlin Press.
- Lunacharsky, A. (1965): On Literature and Art, Moscow, Progressive Publishers.
- Matenjwa, W. (1982): "The effects of Colonialism on the status of the African Woman," Karatasi iliyowasilishwa katika World Student Christian Federation, Limuru Conference Centre.
- Matteru, M.L.N.B. (1987): "Sex and gender construction in Penina Muhando's Plays", Katika KISWAHILI Vol.54/1 na 54/2; Jarida la taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mazrui, A. (1981): Kilio Cha Haki, Nairobi, Longman.
- Mbele, M. (1980) (Mhariri): Viewpoints: Essays on Literature and Drama, Nairobi, Kenya Literature Bureau.

- Mbiti, J.s. (1969): African Religions and Philosophy,  
Nairobi, Heinemann.
- Mbogo, E. (1981): Tone la Mwisho,  
Dar es Salaam, Dar es Salaam  
University Press.
- Mbughuni, P. (1982): "The Image of the Woman in Kiswahili  
Prose Fiction" Katika KISWAHILI Vol.49/1  
Machi; Jarida la Taasisi ya uchunguzi  
wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es-  
Salaam.
- Mclaughlin, A. & Braxton, A. (Wahariri)(1990): Wild Women  
in the whirlwing: Afro-American Culture  
and Contemporary Literary Renaissance,  
New Brunswick, Rutgers University Press.
- Mies, M. (1981): The Social origins of Sexual division  
of labour, The Hague, Institute of Social  
Studies, Occasional Paper No.85, 1981.
- Mitchel, J. (1984): Women: The longest Revolution: Essays  
in Psychoanalysis, feminism and Litera-  
ture, London, Virago Press.
- Monteith, M. (1986)(Mhariri): Women's writing: A Challenge  
to theory.  
Sussex, Harvester Press.
- Mugambi, J. & Kirima, N. (1976): The African Religious Heritage,  
Nairobi, Oxford University Press.
- Mugo, M.G. (1978): Visions of Africa,  
Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- Muhando, P. (1972): Hatia,  
Nairobi, East African Publishing House.

- \_\_\_\_\_, (1973): Tambueni Haki Zetu,  
Dar es Salaam, Tanzania Publishing  
House.
- \_\_\_\_\_, (1974): Heshima Yangu,  
Nairobi, East African Publishing  
House.
- \_\_\_\_\_, (1974): Talaka si Mke Wangu,  
Nairobi, East African Publishing  
House.
- \_\_\_\_\_ ; (1975): Pambo,  
Nairobi, East African Publishing  
House.
- \_\_\_\_\_, (1982): Nguzo Mama,  
Dar es Salaam, Dar es Salaam  
University Press.
- \_\_\_\_\_, (1984): Lina Ubani,  
Dar es Salaam, Dar es Salaam  
University Press.
- \_\_\_\_\_, Lihamba, A. na Balisidya, N. (1981): Harakati  
Za Ukombozi,  
Dar es Salaam, Tanzania Publishing  
House.
- Mulwa, D.K. na Yahya, A.S. (1984): Ukame, Nairobi,  
Longman.
- Mwachofi, A.K. (1987): Mama Ee,  
Nairobi, Heinemann.
- Ndungo, C.M. (1985): "Wanawake na mabadiliko ya Kihistoria"  
Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha  
Nairobi (Haijchapishwa).

- Ngara, E. (1985): Art and Ideology in the African Novel,  
London, Heinemann.
- Ngcobo, (1988): "African Motherhood: Myth or Reality."  
Katika Criticism and Ideology, 2nd Africa  
Writers' Conference, Seminar Proceedings  
No.20, S.I.A.S.
- Ngugi wa Thiong'o (1981): Writers in Politics,  
Nairobi, Heinemann.
- \_\_\_\_\_, na Mugo, M.G. (1976): Mzalendo Kimathi,  
Nairobi, Heinemann.
- Nichols, L. (1981): Conversations with African Writers,  
Washington D.C., Voice of America.
- Nyerere, J.K. (1968): Ujamaa: Essays on Socialism,  
Dar es Salaam, Oxford University Press.
- Omboga, Z. (1986): "The short distant runners: A case study  
of Penina Muhando's and Jay Kitsao's Play  
katika MWAMKO Vol.3, Jarida la Chama cha  
Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ousmane, S. (1962): God's Bits of Wood,  
London, Heinemann.
- Palmer, E. (1983): "The feminine point of view: Buchi  
Emecheta's, "The Joys of Motherhood" katika  
African Literature Today na. 13  
Kilichohaririwa na Palmer E., na Jones, K
- \_\_\_\_\_, na Jones, e. (1983)(Wahariri): African Literatu  
Today no.13, New York, African  
Publishing Company.
- Petersen, K.H. (1988): Criticism and Ideology, Second African  
Writers' Conference, Seminar Proceedings  
no.20, Scandnavian Institute of African  
Studies.

- Pollitt, H. (1975): Women and Communism,  
London, Greenwood Press Publishers.
- Reed, E. (1970): Problems of Women Liberation: A Marxist  
Approach,  
New York, Pathfinder Press.
- \_\_\_\_\_, (1975): Womens, evolution: From Matriarchal to  
Patriarchal Family,  
New York, Pathfinder Press.
- Rodney, W. (1989): How Europe underdeveloped Africa,  
Nairobi, Heinemann.
- Ruthven, K.K. (1984): Feminist Literary Studies: An Introduc-  
tion, London Cambridge University  
Press.
- Ryanga, S.A. (1986): Zinduko,  
Nairobi, Oxford University Press.
- Satre, J.P. (1978): What is Literature,  
London, Methuen.
- Sengo T.S.Y. na Kiango, S.D. (1974): Ndimi Zetu,  
Dar es Salaam, Longman.
- Sengo, T.S.Y.(1977): "Pambo" Katika MULIKA Na.11, Jarida la  
Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili,  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Senkoro, F.M.E.K(1982): Fasihi,  
Dar es Salaam, Press & Publicity Centre
- \_\_\_\_\_,(1987): Fasihi na Jamii,  
Dar es Salaam, Press & Publicity Centre
- Sutherland, E. (1987 edition): The Marriage of Anansewa,  
London, McMillan Publishers.

- Taiwo, O. (1984): Female Novelists of Modern Africa,  
London, MacMillan Publishers.
- Vasquez, A.S.(1973): Art and Society,  
New York, Monthly Review Press.
- Wall, A. C. (1989): Changing Our Own words: Essays on  
Criticism, theory and writing by black  
women,  
New Brunswick, Rutgers University Press.